# Nipashe

Jumatano Juni 19, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579948

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Vijana waitaka NEC kuwekwa kamera vituo vya kupiga kura

UKURASA 2



UCHAMBUZI: Waandishi Zanzibar waazimia kukemea wenye kauli chochezi

Kimataifa

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

AfCFTA kutimiza ndoto za soko huru Afrika

BAADA YA MIAKA 55

Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano

Rais wa zamani wa Misri azikwa baada kufariki dunia mahakamani

Vita yanukia eneo la Ghuba baada ya kushambuliwa meli kubwa za mafuta Ukurasa 20

UKURASA 13

# Maofisa TRA mbaroni kwa tuhuma za rushwa

UKURASA 2



Wakazi wa Jiji la Dodoma, wakiangalia mabehewa mawili ya treni ya abiria, yaliyoanguka baada ya kugongwa na lori aina ya Isuzu lenye namba za usajili T 860 APW (picha ndogo), katika makutano ya Barabara ya Hazina na njia ya reli, jijini humo juzi usiku. **Habari Uk. 9.** **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**MUHIMBILI YAFANYA UPASUAJI UVIMBE KWENYE UBONGO**

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili-Mloganzila kwa mara ya kwanza imeanza kufanya upasuaji mkubwa...

**UKURASA WA 4**

**CUF WAJIPANGA KWA UCHAGUZI MKUU, MITAA**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimeanza kujiandaa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka kesho...

**UKURASA WA 4**

**SABABU KESI YA ZITTO KUKWAMA**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya uchochezi inayomkabili Mbunge wa Kigoma Mjini...


# Mbunge ataja sababu zinazoimaliza Kariakoo

**BASHE** awapa somo mawaziri wa fedha, viwanda kuhusu biashara...*Endelea ukurasa wa 2*

## Watumishi saba Nida waingia matatani

UKURASA 3


**MICHEZO** MSOLLA ATOA MKAKATI MABADILIKO YANGA SC UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Maofisa TRA mbaroni kwa tuhuma za rushwa

**Na Renatus Masuguliko, GEITA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Geita, inawashikilia maofisa watatu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani hapa kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa.

Maofisa wanaoshikiliwa kwa tuhuma hizo ni Sadick Lutenge, Hamza Rugemalira na Elias Msula.

Kaimu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Geita, Mwamba Masanja, alisema jana ofisini kwake kuwa watuhumiwa hao wanatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote, ili kusomewa maelezo ya awali katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita.

Masanja alisema uchunguzi umebaini kwamba mshtakiwa wa kwanza na wa pili, wakiwa katika utekelezaji wa majukumu yao, kwa pamoja walimwomba rushwa Alphonce Mringo ya Sh. milioni 30, ili wamfanyie makadirio ya chini ya kodi ya biashara.

Alisema katika uchunguzi wao, pia wamebaini kutokana na ushawishi huo, mshtakiwa wa kwanza anadaiwa kupokea Sh. milioni 10 ikiwa ni sehemu ya kiasi walichoomba.

Aidha, katika kipindi cha kati ya Januari 2 na Machi 30, mwaka huu, mtuhumiwa wa kwanza na wa tatu kwa pamoja waliomba Sh. milioni 75 kutoka kwa Bertha Magandula na Makoye Shiyunga ambao ni wakurugenzi wa Makoye Hospital Co. Limited.

Masanja aliongeza kwamba Aprili 8, mwaka huu, watuhumiwa kwa pamoja wanadaiwa kupokea Sh. milioni 50 ikiwa ni sehemu ya fedha za rushwa walizoziomba kutoka kwa Magandula na Shiyunga.

Pia alisema Juni 14, mwaka huu, Msula anadaiwa kujaribu kupokea Sh. milioni 10 ikiwa sehemu ya fedha za rushwa ya Sh. milioni 30 alizoomba kutoka kwa Mringo.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kulia), akiangalia trekta jipya baada ya kukabidhiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Prof. Damian Gabagambi (wa pili kushoto), katika eneo la Mbande, Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma jana. **Habari Uk. 22. PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge ataja sababu zinazoimaliza Kariakoo

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

MJADALA umeibuka bungeni kuhusu mazingira ya uendeshaji wa biashara nchini, utitiri wa kodi na tozo zilivyochangia kuua soko la kimataifa la Kariakoo, jijini Dar es Salaam.

Baadhi ya wabunge waliochangia kuhusu hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2018 na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20 na mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2019/20, wameitaka serikali kuja na mkakati wa kurejesha biashara ya kimataifa katika eneo la Kariakoo.

Mbunge wa Mvomero (CCM), Sadiq Murad ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, alisema soko la Kariakoo limepotea katika ramani ya biashara, licha ya kuwa Tanzania ilishafanikiwa kuziteka kibiashara nchi za Burundi, Rwanda, Malawi, Uganda na DRC.

"Leo Kariakoo imepotea kwenye mtandao haipo na sababu za kupotea zipo nyingi ikiwamo suala la namna ya kupeleka fedha za kigeni Dubai, China na nchi nyingine. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti tulikwenda Uganda, unafika unawauliza wafanyabiashara wa Uganda, mbona siku hizi hamji kuchukua mzigo? Wanakwambia sasa hivi wa Dar es Salaam wanakuja kwetu, Malawi wanakuja kwetu, Rwanda wanakuja kwetu, haya ndio majibu tuliyopewa.

"Wale bahari hawana, bandari hawana, BoT (Benki Kuu ya Tanzania) tujiulize kuna nini hapo, TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania)

INAENDELEA UK. 8


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
18/06/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya IJUMAA tarehe 21/06/2019 kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEAS CONSTRUCION** & INVESTMENT itapita bila mizigo kutoka KABANGA kuelekea SUMBAWANGA gari hilo lenye namba za usajili
**T349 BNT /T646 BCJ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
**Urefu - mita 20.0**
**Upana - mita 3.0**
**Kimo - mita 2.90**

3. Njia itakayotumika **KABANGA hadi SUMBAWANGA** kupitia **MPANDA** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00Jioni).

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115281902


# Waitaka NEC kufunga CCTV vituo vya kura

**Na Enock Charles**

WADAU wa uchaguzi wameishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kufunga kamera fiche (CCTV) kwenye vituo vyote vya kupiga kura ili kuepusha malalamiko ya kuibiwa kura yanayoibuka kila unapofanyika uchaguzi nchini.

Akizungumza katika mkutano wa tume na wawakilishi wa makundi maalum ya vijana, walemavu na wanawake uliofanyika Dar es Salaam jana, mwakilishi wa Kongamano la Msaada wa Kisheria kwa Vijana, Ramadhani Juma, aliishauri tume kutumia kamera fiche ili kudhibiti wizi wa kura wakati wa uchaguzi.

"Pamekuwa na malalamiko sana ya kura kuibiwa, je, tume haioni umuhimu wa kuweka CCTV Camera kwenye hizi 'polling stations' (vituo vya kupiga kura) ili kuweka ulinzi wa kura na kuondoa malalamiko?" Ramadhani alihoji.

Akijibu hoja hiyo, Mwenyekiti wa NEC, Jaji Semistocles Kaijage, alisema sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa katika kusimamia uchaguzi nchini, zikitumiwa vizuri zinajitosheleza kwa ulinzi wa kura.

"Sheria zetu, kanuni zetu na taratibu zetu kama zitazingatiwa, uchaguzi wetu ni shirikishi na hakutakuwa na sura hiyo ambayo inaonekana.

"Tatizo ni kwamba tunaacha hivi vyombo vyenyewe, tunatafuta namna zingine zisizofaa, Jaji Kaijage alisema.

Katika mkutano huo, mwakilishi wa Taasisi ya Elimika Tanzania, aliyejitambulishwa kwa jina la Masawiri, alihoji msimamo wa NEC kuhusu wananchi kukaa ama kutokaa umbali wa mita 200 kutoka kwenye vituo vya kupiga kura baada ya kuwa wamepiga kura.

Hoja hiyo ni moja ya mapendekezo ya vyama vya upinzani vikiamini kwa kufanya hivyo, kutakuwa na ulinzi imara wa kura.

Akijibu hoja hiyo, Jaji Kaijage alisema: "Baada ya Uchaguzi Mkuu 2015, mtakumbuka palikuwa na kesi ya Kibatala iliyofunguliwa kuhusu masuala hayo na uamuzi ulitolewa ni kwamba mara baada ya watu kupiga kura, wanarudi nyumbani. Huo ndiyo uamuzi wa mahakama na ndiyo sheria. Sasa hivi, hakuna cha mita 100, 200 wala 300."

Mkutano huo ni sehemu ya mikakati ya NEC kukutana na wadau mbalimbali wakati ikijipanga kwa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

## HABARI KITAIFA

# Watumishi Nida wanaswa tuhuma wizi mali mil. 15/-

**Na Romana Mallya**

WATUMISHI saba wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), wanashikiliwa na polisi Mkoa wa Pwani kwa tuhuma za wizi wa vifaa vya mamlaka hiyo vyenye thamani ya Sh. milioni 15 ambavyo inadaiwa wameviiba na wamekuwa wakiviuza.

Vifaa hivyo ni pamoja na kompyuta mpakato mbili, nyaya zake na vitambulisho vya taifa boksi moja lililokutwa likiwa na vitambulisho 15,000.

Kamanda Polisi wa Mkoa huo, Wankyo Nyigesa, aliwaeleza waandishi wa habari jana kuwa

INAENDELEA UK.5




## Muhimbili yafanya upasuaji uvimbe kwenye ubongo

**Na Beatrice Shayo**

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili-Mloganzila kwa mara ya kwanza imeanza kufanya upasuaji mkubwa wa kuondoa vivimbe katika mishipa ya damu kwenye ubongo.

Upasuaji huo ambao umechukua muda wa takribani saa sita umefanywa na wataalamu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila kwa kushirikiana na daktari bingwa mshauri wa upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu, Profesa Hun Seong, kutoka Yonsei, Korea Kusini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, daktari bingwa wa upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu katika Hospitali ya Muhimbili-Mloganzila, Dk. Raymond Makundi, alisema wamefanya upasuaji huo kwa mgonjwa mmoja ambaye kwa sasa anaendelea vizuri na ataruhusiwa kuondoka.

Alisema wagonjwa waliokuwa wanahitaji huduma hiyo walikuwa wanapelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kupatiwa matibabu ambayo iliwagharimu fedha nyingi.

Alisema kutokana na uchache wa wataalamu na ukosefu wa vifaa tiba hivyo, mgonjwa kama huyo angepelekwa nje ya nchi angelipia Sh. milioni 40.

Aidha, alisema tatizo la vivimbe katika mishipa ya damu kwenye ubongo hutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kurithi vinasaba ambayo mtu huzaliwa navyo, uvutaji wa sigara, na maambukizi ya vijidudu kama bakteria vinavyoathiri mishipa ya damu.

Dk. Makundi alisema ugonjwa huo huchelewa kugundulika kutokana na watu kutokufahamu dalili za hatari za ugonjwa huo na upungufu wa vifaa vya uchunguzi pamoja na wataalamu wa kulibaini tatizo hilo mapema.

"Baadhi ya dalili ni ku

INAENDELEA UK.8

# Kibali chakwamisha kesi ya Zitto

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya uchochezi inayomkabili Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, umedai mahakamani unasubiri kibali cha Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu cha kuita mashahidi kutoka nje ya Dar es Salaam.

Kesi hiyo ilipangwa jana kuendelea kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri, lakini ilishindwa kuendelea kutokana na upande wa Jamhuri kuwa bado hawajapokea kibali cha kuita mashahidi kutoka mkoani Kigoma.

Madai hayo yalitolewa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Nassoro Katuga, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi.

Katuga alidai kuwa mashahidi hao ni muhimu na kwamba Jamhuri inasubiri kibali hicho.

"Mheshimiwa tunaomba muda wa mwezi mmoja wakati tunasubiri kibali cha kuita mashahidi kutoka Kigoma. Mashahidi hao ni muhimu sana katika kesi hii," alidai Katuga.

Upande wa utetezi ulidai kuwa hauna pingamizi na ombi la Jamhuri.

Hakimu alisema kesi hiyo itasikilizwa siku mbili mfululizo Julai 16 na 17, mwaka huu na dhamana ya mshtakiwa inaendelea.

Awali aliposomewa maelezo ya awali, Zitto alikana kwamba Oktoba 28, mwaka jana katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika katika ofisi za makao makuu ya chama cha ACT -

INAENDELEA UK.5

# CUF yaanza maandalizi ya uchaguzi

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimeanza kujiandaa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka kesho wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu kwa kuitisha kongamano jijini Dar es Salaam Jumamosi.

Chama hicho kimeanza maandalizi hayo kwa kufanya kongamano la uzinduzi wa sera na kaulimbiu mpya ya chama hicho Jumamosi jijini Dar es Salaam.

Katika taarifa yake kuhusiana na kongamano hilo, Mkurugenzi wa Habari na Uenezi wa chama hicho, Abdul Kambaya, alisema uzinduzi wa sera hiyo mpya utafanywa na Mwenyekiti wa Chama hicho, Prof. Ibrahim Lipumba.

Kambaya alisema katika uzinduzi huo, wamekaribisha watu mbalimbali bila kujali itikadi za vyama vyao.

"Kongamano hili limepewa jina la 'Sauti ya haki na furaha kwa Watanzania wote'. Kongamano hilo litahudhuriwa na wanachama wa CUF wakiongozwa na viongozi wao wakuu, uzinduzi wa sera hizo ni katika kujiandaa na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na wa Serikali za Mitaa ambao utahusisha mitaa, vijiji na vitongoji ambao unatarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu," alisema Kambaya.

Aliongeza: "Na uzinduzi huu unafanyika mara tu baada ya kumalizika kwa kesi zilizodumu kwa takriban miaka mitatu na kusababisha baadhi ya wanachama wa CUF kufukuzwa."

Kambaya alisema kuwa kongamano hilo sio tu litatoa mwelekeo mpya wa chama, lakini pia litatumika kuonyesha nguvu za CUF katika Jiji la Dar es Salaam na viunga vyake, na kwamba sera hiyo mpya inatarajiwa kujikita katika kutumia rasilimali na maliasili za Tanzania katika kuleta haki hizo na furaha kwa Watanzania wote.



Mwendesha guta akisafirisha mzigo na abiria akiwa juu katika Barabara ya Morogoro, eneo la Manzese Tip Top, jijini Dar es Salaam juzi, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Bosi NMB atoboa siri viwango juu vya mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, Albert Jonkergouw, amesema sababu za benki kutoshusha viwango vya riba za mikopo ni kutokana na gharama za uendeshaji pamoja na hatari za majanga ya kuporomoka kwa taasisi hizo.

Jonkergouw alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuelezea mambo yaliyotokana na mkutano wa wanahisa wa benki hiyo uliofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Alisema hayo alipoulizwa ni kwa nini benki nchini zimekuwa hazipunguzi viwango vya riba vya mikopo pamoja na wito kutoka kwa watu mbalimbali, wakiwamo viongozi wa juu serikalini.

"Zipo sababu mbalimbali za kuwapo kwa viwango vikubwa vya riba na ni kweli kumekuwa na wito wa kupunguza riba za mikopo. Lakini jambo hili ni gumu kulifanyika kutokana na hali halisi ndani ya taasisi za fedha hususan benki," alisema.

"Ndani ya benki kuna ghara

INAENDELEA UK.5


Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-

- Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=
- Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=
- Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima
- Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku

215227501



## HABARI KITAIFA

# Wasimamisha msafara wa waziri awafukuzie tembo

**Na Gurian Adolf**, KALAMBO

WAKAZI wa Kijiji cha Mkowe, Kalambo mkoani Rukwa, juzi walisimamisha gari la Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Josephat Kandege, na kumwomba apeleke ombi Wizara ya Maliasili na Utalii iwarudishe kwenye hifadhi tembo wanaozagaa kijijini hapo na kusababisha kifo cha mtu mmoja.

Hivi karibuni, tembo hao ambao wamekuwa wakivamia kijiji hicho, walisababisha kifo cha Victor Tanganyika (69).

Wananchi hao walifanya hivyo juzi saa 1:45 usiku wakati Kandege ambaye pia ni Mbunge wa Kalambo, alipokuwa anapita kijijini hapo akiwa katika ziara ya kutembelea jimbo.

Kwa mujibu wa wananchi hao, walimwomba Kandege awasaidie kuwasiliana na Wizara ya Maliasili na Utalii ifanye utaratibu wa kuwarudisha tembo ndani ya hifadhi kwa kuwa wamekuwa kero na tishio kwa usalama wao.

Akizungumza kwa niaba ya wakazi wa kijiji hicho, Peter Sikavizya, alimwambia Waziri Kandege kuwa tembo hao wamekuwa wakitoka ndani ya hifadhi na kula mazao pamoja na kusababisha kifo cha mmoja wa wanakijiji hao.

Sikavizya alisema imekuwa kawaida kwa tembo kutoroka ndani ya hifadhi na kupita eneo hilo na baadhi yao wanakwenda mpaka Zambia ambako wamekuwa wakiharibu mazao waliyolima na kutishia usalama wao.

Alisema inafikia wakati wanalazimika kushinda ndani wamejifungia kwa hofu ya kuwaogopa tembo hao, hali ambayo imesababisha washindwe kufanya kazi zao za kila siku.

Baada ya kusikiliza ombi hilo, Naibu Waziri huyo aliahidi kulifikisha suala hilo kwenye wizara husika na watalitatua kwa kuwafukuza tembo hao warudi ndani ya hifadhi.

Hata hivyo, aliwashauri kutowatishia kwa sababu wakikasirika ni hatari kwao kwa kuwa wanaweza kuwadhuru na kuwasababishia maafa makubwa.



Mfanyakazi wa Benki ya NMB, Kanda ya Dodoma, Gulila Mapuli (wa pili kulia), akitoa maelezo kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (kushoto), alipotembelea banda la benki hiyo, kwenye maonyesho ya ng'ombe bora wa maziwa yaliyofanyika kitaifa viwanja vya Nanenane, Nzuguni, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU . PICHA: IKULU.**

# Majambazi yapora, yawapoza walioporwa kwa juisi, biskuti

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WATU wanne wanaosadikiwa kuwa majambazi wakiwa na bunduki mbili, wamevamia Kijiji cha Nonwe, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga na kupora fedha taslimu Sh. milioni nane, vipuri vya pikipiki, vocha za simu na betri za sola.

Akizungumzia tukio hilo, Di-

INAENDELEA UK. 8

# Kibali kesi ya Zitto

INATOKA UK 4

Wazalendo kwa nia ya kuleta chuki miongoni mwa wananchi wa Tanzania dhidi ya Jeshi la Polisi, alitoa maneno ya uchochezi.

Zitto alikana maneno ambayo anadaiwa kuyasema kuwa "Watu ambao walikuwa majeruhi katika tukio la mapambano baina ya wananchi na polisi, wakiwa wamekwenda hospitalini kupata matibabu katika Kituo cha Afya cha Nguruka, polisi wakapata taarifa kuwa kuna watu wanne wamekwenda hospitali kituo cha afya Nguruka kupata matibabu wakawafuata kule wakawaua."

Jamhuri inadai maneno hayo yalikuwa ya uchochezi yenye kuleta hisia ya hofu na chuki.

Mshtakiwa anadaiwa kutoa maneno kwamba: "Lakini tumefuatilia kwa kina jambo hili, taarifa ambazo tumezipata kutoka kijijini Mpeta Nguruka, Uvinza ni mbaya ni taarifa ambazo zinaonyesha wananchi wengi sana wameuawa na Jeshi la Polisi, pamoja na kwamba Afande Sirro amekwenda kule, halijatoa taarifa yoyote kuhusu wananchi....kama hawa Wanyantuzu walivamia eneo la ranchi, kuna taratibu za kisheria za kuchukua nasiyo kuwaua, wananchi wengi sana wamekufa."

# Bosi NMB atoboa siri viwango juu vya mikopo

INATOKA UK 4

ma kubwa za uendeshaji na pia kuna athari nyingi za majanga, hivyo benki ni lazima ifanye jambo kama hilo kwa uangalifu ili isiyumbe na haya kusimamisha shughuli zake," aliongeza.

Pia alionya juu ya suala la kupandisha viwango vya riba katika uwekaji fedha benki kwa kuwa jambo kama hilo linaweza kusababisha benki kulipa fedha nyingi kwa ajili ya riba na hatimaye kushindwa kuhimili uendeshaji na maendeleo yake kwa ujumla.

Akizungumza kuhusu yaliyojiri katika mkutano wa wanahisa wa benki hiyo, wanachama wameridhia kulipa gawio la Sh. bilioni 33, sawa na Sh. 66 kwa kila hisa. Alisema malipo hayo ni ongezeko la asilimia 3 ya Sh. 64 kwa kila hisa zilizolipwa mwaka jana.

"Benki iliripoti faida ya Sh. bilioni 142 kabla ya makato ya kodi kwa mwaka ulioishia Desemba, 2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia tatu kutoka faida ya Sh. bilioni 138 iliyopatikana mwaka uliotangulia," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya NMB, Prof. Joseph Semboja, benki hiyo imezidi kujiimarisha kwa uwiano wa mtaji kwa asilimia 16.5 hali ambayo inaonyesha kuwa iko salama kibiashara. Pia alielezea kuwa mkakati mkubwa kwa benki hiyo ni kuimarisha biashara ya fedha ili kukua zaidi kiuchumi.

"Kwa miaka kadhaa sasa, NMB imeendelea kuwa imara yenye afya kifedha, lengo ni kuendelea kuimarisha zaidi na kubaki hivyo. Ili kufikia mafanikio haya, tunapaswa kuhakikisha tunafanya uamuzi sahihi hasa katika udhibiti wa mabadiliko kwenye mahitaji makuu kimtaji," alisema Prof. Semboja.

# Watumishi Nida wanaswa tuhuma wizi mali mil. 15/-

INATOKA UK 3

watuhumiwa hao ambao majina yao yamehifadhiwa kwa uchunguzi, huiba vifaa hivyo na kuuza ili kujipatia fedha.

Alisema watuhumiwa hao waliiba vifaa wakati ofisi ikihamishwa kutoka ofisi ya awali iliyokuwa kwenye kiwanda cha kubangua korosho cha Tanita kilichoko Tumbi kwenda jengo jipya la Nida mjini Kibaha.

"Watumishi hawa waliteuliwa na Nida kuhamisha rasilimali vifaa kutoka ofisi hiyo ya zamani kwenda ofisi mpya za Nida, wakiwa njiani ndipo walipovichepusha na kuviuza kujipatia fedha kwa manufaa binafsi," alisema. Kamanda Nyigesa alisema taarifa za tukio hilo zilipokelewa Nida Juni 14, mwaka huu na katika ufuatiliaji wa Jeshi la Polisi ndipo walipowakamata watumishi hao saba.

"Jumla ya thamani ya mali yote iliyoibwa ni Sh. milioni 15," alisema.




## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Hatua hii itarejesha uhakika usafiri majini*

**USAFIRI** wa abiria na mizigo kupitia majini umekuwa changamoto kwa wananchi wa maeneo kadhaa nchini, kutokana na kukosa vyombo vya uhakika hususani meli.

Maeneo yanayozungukwa na maziwa wananchi wake wamejikuta wakikosa usafiri wa uhakika kutokana na uchache pamoja na uchakavu wa meli hizo.

Kwa mfano, katika Kanda ya Ziwa Victoria kumekuwapo na changamoto zaidi baada ya kupinduka na kuzama kwa meli ya MV Bukoba mwaka 1996 na kusababisha vifo vya watu zaidi ya 800. Meli hiyo haikuopolewa, hivyo kusababisha kukosekana kwa meli nyingine mbadala hadi leo.

Hatuwezi kuelezea athari zote katika mikoa yote inayozungukwa na maziwa nchini, lakini itoshe kusema kuwa wakazi wa maeneo hayo wameathirika sana kiuchumi na kijamii.

Wanasiasa kadhaa kwa kipindi kirefu wamekuwa wakitoa ahadi za kuboresha usafiri wa majini hasa ununuzi wa meli mpya katika maziwa ya Victoria, Nyasa na Tanganyika, bila ahadi hiyo kutekelezwa.

Ahadi iliyotolewa na Rais John Magufuli ya kuboresha miundombinu ukiwamo ununuzi wa meli mpya katika maziwa yote mwaka 2015, inaonekana kutimia, baada ya kuanza utekelezaji wake.

Kwa wananchi wa mikoa ya Ruvuma na Mbeya wanaoishi kando ya Ziwa Nyasa, wanatarajia kuanza kunufaika na usafiri wa meli ya MV Mbeya II ambayo ujenzi wake unatarajia kukamilika Agosti, mwaka huu.

Kwa miaka miwili sasa wananchi wa maeneo hayo, hawana usafiri wa uhakika baada ya meli ya MV Songea iliyokuwa ikitoa huduma katika ziwa hilo, kusitisha safari zake tangu mwaka 2017 kutokana na kuwa na hitilafu.

Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Abeid Gallus, alisema mapema wiki hii kuwa ujenzi wa meli hiyo umefika asilimia 82.

Ujenzi wa meli hiyo unagharamiwa na Mamlaka ya Bandari (TPA) kwa Sh. bilioni 9.1 na ina uwezo wa kupakia mizigo tani 200 na abiria 200 kwa wakati mmoja, hivyo kukamilika kwake itasaidia kupunguza tatizo la usafiri kwa wakazi wa mikoa hiyo.

Alisema hatua hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la usafiri kwa wananchi wa mikoa ya Ruvuma na Mbeya kwa sababu kwa muda mrefu walikuwa wakitumia usafiri wa boti au mashua, lakini hakuna chombo madhubuti kinachofanya kazi ziwani.

Meli hiyo pia itafungua wigo wa biashara kwa nchi za Malawi na Msumbiji, hivyo kuongeza wigo na kibiashara na kuboresha uchumi wa kwa jamii zinazozungukwa na ziwa hilo.

Katika hatua nyingine, wananchi wa Mkoa wa Kagera na mikoa ya jirani inayozungukwa na Ziwa Victoria, wanatarajia kunufaika meli mpya inayojengwa itakayokuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo.

Mbali na meli hiyo mpya, meli nyingine ya MV Victoria inafanyiwa marekebisho na itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200 hadi 4,000 na tani za mizigo 200 hivyo kurahisisha usafiri kwa wakazi hao.

Kaimu Meneja wa Bandari ya Ziwa Victoria, Geofrey Lwesya, aliyaeleza hayo wiki iliyopita kwa waandishi walipotembelea bandari hiyo ili kuona miradi ya maendeleo inayotekelezwa na TPA.

Alisema ujenzi wa meli hiyo unatarajiwa kukamilika Septemba mwakani na itasaidia kuongeza mapato zaidi katika bandari ya Bukoba ambayo licha ya kutokuwapo kwa meli za abiria, yamefika Sh. milioni 60 kwa mwezi kutoka Sh. milioni 29 miaka ya nyuma.

Tunazipongeza jitihada hizo za utekelezaji wa ahadi ya Rais Magufuli ya ununuzi wa meli mpya pamoja na vivuko katika maeneo mbalimbali nchini, ambao tunaamini kuwa umetokana na umakini katika suala zima la ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Jenifer Julius

# *Tanzania ichukue hatua zaidi kufikia makubaliano ya Paris*

**KATIKA** makubaliano ya Paris, mataifa yamewekewa malengo ya kuzuia hali ya ongezeko la joto la kimataifa kufikia nyuzi joto 1.5.

Kwa hatua hiyo mataifa hasa yanayoendelea yapo katika mapambano kuhakikisha kuwa lengo hilo linatimia na hasa wakati huu ambapo hali inazidi kuwa mbaya kadri muda unavyokwenda.

Mojawapo ya mataifa ambayo yanahitaji kukaza buti ipasavyo ni Tanzania, kutokana na kwamba athari za mabadiliko ya tabianchi zinaiathiri kwa kasi nchi hii iliyo Afrika Mashariki.

Na miongoni mwa athari zilizopo wazi ni kutotabirika kwa majira, hali inayoyumbisha uchumi.

Mfano kwa mwaka huu, baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, wakulima wamepata hasara ya kurudia kupanda mbegu kwa sababu zile za awali ziliozea ardhini, kutokana na mvua kutonyesha kwa wakati uliotegemewa.

Kwa mantiki hiyo wapo baadhi ya wakulima hawakurudia kupanda mbegu kwa kukata tamaa au kukosa pesa.

Katika Mkutano wa Mabadiliko ya tabianchi unaoendelea jijini Bonn, nchini Ujerumani, mjadala wa jinsi gani mataifa yanaweza kuzuia ongezeko hilo la joto ili kufikia makubaliano ya Paris ni miongoni mwa mingi.

Muungwana ana maoni kwamba kuna mambo yaliyojadiliwa ambayo ni muhimu Tanzania ikajifunza ili kuendana na kasi ya makubaliano ya Paris.

Na mojawapo ya mambo hayo ni yale yanayochangia ukataji wa miti na jinsi ya kupambana nayo.

Kutokuwa na sheria kali inayosimamia biashara ya miti ni baadhi ya mambo yanayotajwa kuchangia ukataji wa misitu holela.

Kwamba sheria ipo lakini haitekelezwi ipasavyo na watu wanajikatia miti bila woga.

Ujasiri wao unatoa taswira kwamba yupo mtu nyuma ya pazia anayewalinda.

Katika mahojiano na Nipashe Dk. Dil Raj Khanal kutoka Shirikisho la Jamii ya Watumiaji Misitu (Federation of Community Forest Users, (FECOFUN) nchini Nepal, anasema ni wakati sasa mataifa kusimamia utekelezaji wa sheria za biashara ya miti ili kuhifadhi hewa ukaa ya kutosha.

Sababu nyingine inayotajwa kuchangia uharibifu wa mazingira ni mwingiliano wa shughuli za kilimo, hasa kilimo kisichokuwa na mpangilio.

Hii ina maana kwamba shughuli za kilimo wakati mwingine zinasababisha ukataji wa miti kwa kiasi kikubwa.

Katika maandalizi ya shamba, mkulima analazimika kukata miti au kuchoma moto shamba ili aweze kupanda mbegu.

Kitendo cha kuteketeza hekari za maeneo yenye miti kwa ajili ya kilimo kwa nchi kama Tanzania kwa hali iliyonayo kwa sasa ni hatari.

Aidha, moto unaoteketeza hekari za mashamba hutoa moshi kwa wingi ambao wote huishia kuziba tabaka la ozoni.

Dk. Khanal anashauri ni wakati sasa wa mataifa kuzuia uchomaji wa moto mashamba na kutoa elimu kwa wakulima ya njia nzuri za kuandaa mashamba.

Vilevile anashauri mataifa kuzuia ukataji wa miti kwa ajili ya kilimo.

Uhamaji wa watu kutoka sehemu moja kwenda nyingine pia imetajwa kama chanzo cha uharibifu wa mazingira.

Kwamba jamii inapohamia eneo lingine hasa katika maeneo ya vijijini, inalazimika kukata miti ipate eneo la kujenga nyumba, lakini pia miti ya kujengea nyumba.

Jamii haina budi kuheshimu na kutangaza sheria za taifa za misitu.

Lakini pia elimu ya umuhimu wa misitu kwa jamii itolewe ikiambatana na uhamasishaji juu ya upandaji wa misitu ili kama taifa tufikie malengo tuliojiwekea kupitia Mkataba wa Makubaliano ya Paris ya kuzuia ongezeko la joto la dunia kwa kiwango cha nyuzi 1.5, na hivyo kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo zinaonekana wazi.

## BARUA/MJADALA

### *Tujengeeni daraja hili tulilolichangia*

**Mhariri**

MIMI ni mmoja kati ya wananchi wanaozikubali sana jitihada za Rais John Pombe Magufuli ya kuchapa kazi ili kujiletea maendeleo kama mtu mmoja mmoja, lakini na kwa ustawi wa taifa la Tanzania kwa ujumla wake.

Aidha, ni mmoja miongoni mwa Watanzania walio wengi ambao wanaikubali sana dhana ya wananchi kuchangia maendeleo ya eneo lao pale walipo, kwa kushiriki kwenye miradi mbalimbali ya kujitolea nguvu kazi ama kuchangia fedha.

Ninafanya hivyo kwa sababu michango kama hiyo huwa ina faida za moja kwa moja kwetu sisi wananchi au hata kama si ya moja kwa moja, ina faida zake kwa mgongo wa nyuma kwa maana ya ama watoto na wajukuu wetu, kama siyo kwa jirani zetu.

Kunapokuwa na changamoto kwa mfano ya barabara ambayo wananchi wana uwezo wa kuilima au ya daraja ambalo wananchi wanaweza kubeba mawe au kuchangia kidogo fedha ili daraja la kuwasaidia liweze kujengwa, basi mimi huwa niko mstari wa mbele kushiriki.

Na ndiyo maana nimeshiriki kwa mapana sana katika kutoa michango mbalimbali iliyohusu kuchangia ujenzi wa zahanati katika kijiji chetu au ujenzi wa madarasa, nikielewa fika kuwa huo ni wajibu wa msingi kufanya.

Hata hivyo, Mhariri ninapokuja kupinga au kutokubaliana na aina hii ya uchangiaji wa nguvu kazi ama fedha kutoka kwa mwananchi ni pale ambapo michango hiyo inapoishia hewani, bila kutekeleza kilichokusudiwa.

Na ndicho kilichonifanya leo hii niandike barua hii kwako Mhariri, nikiwa mkazi wa Kinondoni Mashariki, Kata ya Mabwepande, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Mimi pamoja na wakazi wenzangu wa wa Kinondoni Mashariki, tulichangia shilingi 70,000 kila kaya kwa ajili ya ujenzi wa daraja litakalorahisisha usafiri katika eneo la Mji Mpya.

Sasa hadi miaka imepita, na daraja hatuoni likijengwa huku viongozi wetu, kwa maana ya Mwenyekiti wetu wa mtaa pamoja na diwani wetu wa Kata ya Mabwepande, wakiwa wa kimya kama vile hakuna kitu kilichofanyika.

Mhariri, hapa ndipo ninapokuja kupingana na aina hii ya uchangiaji kwa sababu tunapochanga kwa ajili ya maendeleo yetu, inapaswa tulichochangia kionekane na si vinginevyo.

Ninaomba basi kupitia kwako wahusika watueleze fedha zetu zilipo kwa kuwa hatuoni daraja likijengwa na tatizo bado lipo.

**Mkazi Kinondoni Mashariki, Dar**

# Kama si wazazi wao nani atawafunza watoto?

**Na Gaudensia Mngumi**

WAKATI tunapoadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, ni muda kwa wazazi kutafakari mambo ambayo kutokana na mazingira na miiko ya Afrika hatuwezi kuyazungumza kwa watoto wetu.

Mojawapo ambalo hatulisemi ni suala la kushiriki ngono na utoaji mimba unaowaumiza mabinti wa taifa hili.

Ukweli tulio nao ni kuwa kizazi cha wazee wa leo wenye miaka 70 na kuendelea ni zao la jamii iliyokuwa na usiri mkubwa kwenye kuzungumzia mambo ya ngono.

Hawa ndio baba na mama wa wazazi wa leo ambao watoto wanatatizo na kufanya maamuzi kuhusu ngono.

Wakiwa pia hawakuzungumziwa na wazazi wao kuhusu masuala ya kujamiana utotoni, ni kundi la wazazi wa leo ambalo wanapaswa kubadili usiri huo na kuanza kuwafundisha watoto kuhusu kushiriki ngono na matokeo yake.

Eneo mojawapo linalotakiwa kujadiliwa ni athari kama za kupata mimba na kuzitoa kwa njia zisizo salama, jambo linaweza kusababisha kifo, heshima kushuka na wakati mwingine ugumba.

Wiki hii ni ya Mtoto wa Afrika na kwa Tanzania binti wa taifa hili anakabiliwa na kupata mimba utotoni kunakotokana na kubakwa.

Zaidi ya watu wengine hutokea kubakwa na ndugu zake wa karibu, kuwekwa kinyumba na baba yake mzazi au wa kumlea.

Mabinti hawa wanakuwa sehemu wa waathirika wa vifo vya wanawake vinavyohusiana na uzazi. Hii ni changamoto kubwa kitaifa kwani kinamama takribani 560 nchini, hufa kati ya kila vizazi hai 100,000.

Taarifa hizi ni kwa mujibu wa takwimu za Utafiti wa Afya ya Jamii (DHS) uliofanyika mwaka 2018. Hali hii unapoitizama pamoja na kasi ya unyanyasaji mabinti ambao hupata mimba udogoni, inaelekeza kuwa kuna haja ya wazazi kuzungumza na watoto kuhusu ngono na mimba utotoni.



Binti akihangaika kutafuta maisha mjini pengine ni kutokana na changamoto alizozipata utotoni. **PICHA MTANDAO.**

Zaidi ya hayo, Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (Tacaids), Machi mwaka jana , ilieleza kwenye ripoti ya utafiti wa VVU na Ukimwi kuwa vijana wa kati ya miaka 14 hadi 24 huambukizwa zaidi VVU nchini.

Asilimia kubwa ya maambukizi mapya ni kwa watoto wenye miaka 15 hadi vijana wa miaka 24 na kati yao wengi ni wanawake.

Ni dhahiri kuwa wazazi wanalazimika kubadilika, kwani wameshindwa kuzungumza kuhusu ngono na watoto wao na hata kutaja suala la upataji na utoaji mimba.

Inavyoelekea 'mmewatelekeza' watoto wenu waendelee kuogelea kwenye ngono za utotoni bila kuwasaidia.

Ni dhahiri kuwa huenda mabinti na vijana wa kiume (teenagers) hawahitaji kujamiiana bali wanachotaka ni upendo wa wazazi na ukaribu kutoka kwa baba na mama au walezi pamoja na familia na jamii inayowazunguka.

Watoto hawa wa Tanzania hasa mabinti, wana matatizo mengi mojawapo ni umaskini ndani ya familia zinazoshindwa kuwapa mahitaji muhimu kama chakula, elimu bora na makazi salama.

Si hivyo tu, wanaoishi mijini wanakabiliwa na tamaa za matumizi ya mihadarati na pombe, hamu ya kwenda na wakati kwa kumiliki vitu 'vikali' kama simu, mavazi na hadaa kutoka kwa mafataki za kuwapa magari.

Watoto hawa wa kike wanakabiliwa na hatari ya kunyanyaswa kingono ndani ya familia zao, shuleni na kwenye jamii hata kutoka kwa madereva wa bodaboda walio otapakaa nchi nzima.

Ni ukweli kuwa watoto hawa hufanya ngono na wanaamini kwamba zinawapa faraja na furaha wanayoikosa, japo si kweli wakati wote.

Wazazi wanalazimika kufunguka na kuzungumza masuala ya kujamiiana katika umri mdogo kwa sababu watoto hawa wenye umri wa chini ya miaka 18 hawafahamu athari za ngono za utotoni.

Katika mazungumzo haya, wazazi na walezi wawafahamishe mabinti kuwa watapata ujauzito na wanaweza kujaribu kutoa mimba kwa njia zisizo salama na kupoteza maisha.

Aidha, wanapoteza heshima (ubikira) kiholela, kujiingiza kwenye ngono kienyeji utotoni huwapotezea heshima wazazi na watoto hao ndani ya jamii.

Pia, kupata ujauzito na kutoa mimba kunasababisha athari kiafya ikiwa ni pamoja na kifo, ugumba, lakini pia kuwa na uhusiano na watu wazima (mafataki) wanaowaahidi kuwapa vitu kama magari, simu na mavazi kunaweza kuharibu ndoa za wenza na kuvuruga familia hivyo kuongeza tatizo la talaka, kutengana na kutelekeza familia.

Tatizo jingine ni kupata maradhi kwa wasichana na wavulana kama homa ya ini, VVU na UKimwi, kaswende, kisonono na maambukizi ya njia ya uzazi ambayo yote hufifisha hatima ya mtoto mwenye ndoto za kulitumikia taifa.

Watoto waambiwe kuwa kujiingiza kwenye ngono kutasababisha kijana kuua au binti kujiua kutokana na chuki za kimapenzi, kwa mwanaume anaweza kuhukumiwa kifungo cha maisha jela.

Wazazi hawahitaji orodha ndefu ya athari za kukaa kimya kuhusu suala la watoto kujamiiana. Ni wakati wa kuanza kuzungumza nao na kuokoa kizazi cha Mtoto wa Afrika ambaye ni Mtanzania.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**




**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Mbunge ataja sababu zinazoimaliza Kariakoo

INATOKA UK.2

tujiulize kuna nini hapo? Kwa nini tumelipoteza soko la Kariakoo, bidhaa zile zilikuwa zinapatikana pale zina grade zake (viwango), ukinunua mzigo kule Dubai, China kuna light weight, kuna heavy weight, sasa zile biashara zilizokuwa zinafanyika, TRA hawajui light, hawajui heavy, hawajui nini, wao ni kodi kodi tu, matokeo yake tumeua mtandao wa biashara."

Sadiq alisema huko ni kuwakatisha tamaa wafanyabiashara, wakati ambao Tanzania ilitakiwa kufungua milango ya Kariakoo.

"Dk. Mpango tusaidiane, tukae pamoja, tuzungumze hili, tuna ushahidi, tuna nia ya kusaidia eneo hii lirudi katika mtandao wa biashara katika nchi zote za maziwa makuu ambazo zimetuzunguka," alieleza Sadiq.

Sadiq alisema unapokwenda kununua mzigo Dubai au China, ukinunua mzigo wa dola 100,000 wafanyabiashara wa huko wanataka fedha taslimu.

"Je, utaratibu wa kupeleka dola 100,000 ukoje?" Alihoji na kuongeza kuwa ni lazima BoT wasaidie namna bora ya kuhakikisha biashara zinarudi.

"TRA kuna utaratibu ambao unasababisha wafanyabiashara na Watanzania wapate shida, shida namba moja ni zile fomu za usajili, fomu zile zimeandikwa kwa Kiingereza," alisema na kuongeza:

"Wafanyabiashara wanapata shida kuzijaza, fomu zile zina urasimu, matokeo yake kuna vishoka wamekaa nje kwenye ofisi za TRA wanachukua zile fomu wanawajazia watu, na vishoka wale wanawatoza Watanzania Sh. 10,000 hadi 20,000."

BASHE AMPA NENO MPANGO

Mbunge wa Nzega Mjini (CCM), Hussein Bashe, alimuomba Waziri Mpango akae na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Basgungwa, wafanye mabadiliko makubwa ili kunusuru biashara.

Bashe amemshauri Waziri Mpango kuichukua sheria iliyoanzisha Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela) na kuziunganisha taasisi zote hizi ndani yake na kisha serikali ianzishe Mamlaka ya Udhibiti Usajili wa Leseni za Biashara ili mtu anapoingia kusajili biashara na kuchukua leseni anapokutana na kila kitu mule ndani, akitoka aende kufanya biashara yake.

**NAPE ALIA NA TOZO**

Mbunge wa Mtama (CCM), Nape Nnauye, alisema uamuzi wa kufuta tozo 54 utasaidia kurahisisha mazingira ya ufanyaji biashara nchini, lakini bado kuna tozo nyingine zinapaswa kuangaliwa.

"Pamoja na kufuta tozo ya visima sasa fikirieni kufuta kodi kwenye mitambo ya kuchimba visima vya maji. Mitambo hii itasaidia kuchimba visima pamoja na malango kwa ajili ya umwagiliaji.

"Pia naunga mkono pendekezo la kamati ya bunge kuhusu sekta inayogusa watu wengi ambayo ni kilimo. Ikiguswa inagusa maisha ya watu wengi na ingeweza kupambana dhidi ya umaskini kwa wananchi," alisema.

Vilevile, aliishauri serikali kuongeza wigo wa walipakodi ambao watasaidia serikali kukusanya mapato yakutosha.

**SILINDE ATAKA PPP**

Mbunge wa Momba (Chadema), David Silinde, aliitaka serikali kutambua kuwa maendeleo ya nchi hayategemei kukusanya kodi.

Alisema maendeleo hutegemea kuboresha uwekezaji wa moja kwa moja na ushirikiano wa sekta binafsi na umma (PPP).

"Duniani kote maendeleo ya nchi hayategemei kodi pekee, nasema hivi kwa sababu wimbo humu ndani (bungeni) ni kodi tu. Nchi nyingi hutumia kodi kwa matumizi mengineyo na kulipa mishahara," ameeleza.

Alisema katika Bajeti ya Wizara ya Fedha imeainishwa miradi isiyotekelezeka na kutoa mfano wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ambao hivi karibuni Rais John Magufuli alisema mwekezaji alikuwa na masharti magumu.

Mbunge wa Gairo (CCM), Ahmed Shabiby, alisema wafanyabiashara husuan wadogo wanakabiliwa na tatizo kwenye mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EFD).

"Mashine za EFD zimekuwa kero, sijajua tatizo ni kampuni zilizopewa tenda au la. Kila siku ni mbovu sasa zimekuwa mtaji kwa watu utaambiwa mashine mbovu nunua nyingine,"

Naye Mbunge wa Ukerewe (CCM), Joseph Mukundi, alisema uchumi unaonyesha kupanda kwa asilimia saba ambazo zilizotokana na sekta mbalimbali za kiuchumi zilizofanya vizuri ikiwamo ya kilimo ambayo imekuwa kwa asilimia 5.3.

Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Ruth Mollel, alisema watumishi wamesahaulika katika maslahi yao husuan nyongeza ya mshahara.

"Nazidi kusisitiza watumishi wa umma ndio walipakodi wazuri anapopokea mshahara, analipa kodi bila kukwepa. Nimeangalia bajeti imetengwa kama Sh. trilioni saba kwa ajili ya mishahara ikionyesha hakuna nyongeza."

# Majambazi yapora, yawapoza walioporwa kwa juisi, biskuti

INATOKA UK. 5

wani wa Viti Maalumu wa kata hiyo, Gabriela Kimaro, alisema watu hao walivamia kijiji hicho na kuanza kuvunja nyumba za wafanyabiashara.

Alisema wananchi waliposikia vishindo hivyo walianza kupiga yowe kuomba msaada, lakini watu hao walipiga risasi hewani iliyowanyamazisha wananchi hao.

Mwathirika wa tukio hilo, Sumbu Nemelwa, alisema watu hao walivamia nyumbani kwake usiku na kumlazimisha atoe Sh. milioni 20 alizouza tumbaku.

Alisema alipowaambia hana fedha hizo walimpiga sehemu mbalimbali za mwili na kuamua kuwapa Sh. 200,000 na baadaye walimchukua na kwenda kumfunga kwenye mti, huku wakimwacha na mwenzao aliyekuwa na bunduki kumlinda na wao kwenda kufanya uhalifu sehemu nyingine.

Katika tukio hilo, mwathirika mwingine aliyevamiwa na watu hao, John Kimaro, alisema walifika kwenye nyumba yake na kupiga risasi moja hewani na aliposikia mlio wa bunduki alimwamsha mkewe na kubeba watoto na kukimbilia kwenye nyumba ya nyuma na kujificha.

Alisema watu hao walifanikiwa kuvunja mlango wa duka na kuvunja na wa chumbani kwao na kufanikiwa kuchukua Sh. milioni sita, alizokuwa ameziweka.

"Waliponikosa chumbani, jambazi mwingine aliamuriwa kuzunguka mlango wa nyuma baada ya muda niliwasikia majambazi hao wakiambiana wahi zunguka mlango wa nyuma ametukimbia," alisema Kimaro.

Alisema dukani walifanikiwa kuiba vocha, vipuri vya pikipiki, pamoja na betri za sola.

Diwani Gabriela, alisema eneo jingine lililovamiwa ni kwenye nyumba ya mchungaji waliyopanga wafanyabiashara wa mazao na kufanikiwa kuwapora Sh. milioni 1.8.

Alisema baada ya kufanya uhalifu huo, watu hao wakiwa wamebeba bunduki na mabegi, walimpitia mwenzao aliyekuwa anamlinda mwathirika aliyefungwa kwenye mti na kumfungua na kisha wakampa juisi na biskuti na kumwamuru anywe ili apoze maumivu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Richard Abwao, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alisema taarifa hiyo haijamfikia.

## Nchi 8 Afrika kujifunza Tanzania kuhusu afya

**Na Mwandishi Wetu**

MAOFISA wa nchi nane kutoka nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, wanatarajiwa kuwasili nchini Juni 23, kuhudhuria mafunzo ya programu ya wakufunzi kuhusu kuboresha utatuaji wa matatizo kwa njia nyepesi na inayotumia busara kubwa katika huduma ya afya na hospitalini (KAIZEN).

Maofisa hao ambao wanatarajiwa kuja kujifunza uzoefu kutoka Tanzania ni wa nchi za Benin, Ghana, Liberia, Malawi, Sierra Leone, Sudan, Uganda na Zimbabwe.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), ilisema kuwa katika mafunzo hayo jumla ya washiriki 47 pamoja na wawakilishi kutoka nchi mbalimbali watajifunza elimu ya msingi na kazi za vitendo zinazohusu Kaizen ili kuboresha huduma za hospitali na afya zinazotelewa na Tanzania kwa zaidi ya miaka 10 sasa.

Kwa Tanzania hospitali za rufani (RRH) na hospitali za taifa na kanda zimefanya juhudi kubwa kutokana na msaada wa mradi wa kuziongezea uwezo hospitali za rufani (RRHMP), ambao unatekelezwa na JICA, kwa ushirikiano na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia kazi mbalimbali za mpango wa Kaizen.

Taarifa hiyo ilisema baadhi ya mifano ambayo imetekelezwa na Kaizen ni pamoja kupunguza idadi ya maabara za damu zilizotelekezwa kutoka 65 hadi 10 (Hospitali ya Mbeya), kupunguza idadi ya wagonjwa wa vidonda wodini kutoka 11 hadi wawili (Hospitali ya Singida), kupunguza gharama za ununuzi wa mifuko ya kuwekea taka za hospitali kutoka Sh. milioni 16 hadi Sh. milioni tatu (Hospitali ya Mbeya) na kupunguza gharama za ununuzi wa chupa za kuchemshia vifaa vya hospitali kutoka Sh. milioni 17.6 hadi Sh. milioni 15.3 (Hospitali ya Rufani Mbeya).

Aidha, mpango huo pia umepunguza muda wa wagonjwa wa nje wa kusubiri huduma kutoka dakika 45 hadi dakika 15 (Hospitali ya Rufani Mbeya) na kupunguza gharama za dawa za matibabu ya macho kutoka Sh. milioni 12.5 hadi Sh. milioni 5.2 (Hospitali ya Taifa Muhimbili).

Kutokana na mafunzo hayo, uzoefu wa Tanzania utakwenda kufanyiwa kazi katika nchi za Afrika kwenye sekta ya afya.

# Muhimbili yafanya upasuaji uvimbe kwenye ubongo

INATOKA UK.3

pata maumivu makali ya kichwa, kuona vitu viwili viwili na kupoteza fahamu," alisema.

Dk. Makundi alisema vishipa vinapopasuka wagonjwa wanafika hospitali wakiwa na ugonjwa wa kiharusi, hivyo wanatibiwa kama wana viharusi kutokana na kukosa uelewa.

Makunda alisema ugonjwa huo huwaathiri wenye umri kuanzia miaka 30 hadi 60 na hospitali hupokea wagonjwa kati ya wanne hadi sita kwa mwezi.

Naye daktari wa upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu, Dk. Alvin Miranda, akielezea upasuji huo, alisema lengo la upasuaji ni kufunga vivimbe hivyo kwa kutumia vifaa tiba maalum (aneurysm clips) ili kuzuia damu isiendelee kuvuja katika ubongo.

"Mgonjwa anapopata tatizo la kuvuja damu kwenye ubongo kwa mara ya kwanza anakuwa katika hatari ya kupoteza maisha kwa asilimia 30, wakati akivuja damu kwa mara ya pili inaweza kusababisha kifo kwa asilimia 70 hadi 80," alisema Dk. Miranda.

Alisema kitakwimu wastani wa asilimia tatu ya watu duniani hupata tatizo hilo kila mwaka na nusu yao ambao huwahi kufika hospitalini mishipa inapopasuka huku wengine wakipoteza maisha kabla ya kufikia huduma.

Dk. Miranda alisema asilimia 50 ya wagonjwa hufika hospitali na asilimia 50 hutibiwa kwa tiba ya kiharusi.

Naibu Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Julieth Magandi, alisema wamefurahi kwa kuanza upasuaji huo na utasaidia kupunguza gharama za rufani za nje ya nchi.

# Watu 168 wanusurika ajali ya treni

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WATU 168 wamenusurika kifo baada ya treni ya abiria kugongwa na gari katika maunganiko ya barabara na njia ya reli enoe la Hazina jijini Dodoma.

Ajali hiyo ilitokea jana na ilihusisha gari lenye namba za usajili T 860 APW aina ya Isuzu likiendeshwa na dereva, Hamis Salamu (49), mkazi wa Nkuhungu jijini hapa ambapo gari hilo liligonga treni ya abiria No, Y 12, iliyokuwa ikiendeshwa na Michael Mdachi (44), mkazi wa Kisasa jijini hapa na Guard Abdala Ngola (59), mkazi wa Area C.

Akizungumza kwenye eneo la tukio, Kamanda wa Polisi mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema treni hiyo ilikuwa ikitokea Kigoma, Mwanza na Mpanda kuelekea Dar es Salaam ikiwa na mabehewa 9 za daraja tatu, mbili na daraja la kwanza.

Mengine ni behewa la mgahawa moja, behewa la vifurushi na la breki moja na kusababisha majeruhi 32 kati ya 168 waliokuwa kwenye mabehewa namba 3648 na 3607 ambayo yalianguka ambapo watatu hali zao siyo nzuri na wamelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Alisema safari ya kutoka Tabora kuelekea Dar es Salaam ilianza juzi saa 11:25 ikiwa na mabehewa 14, na kwamba ilipofika maeneo ya ya Hazina katika halmashauri ya jiji la Dodoma iligongwa na gari.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Patrobasi Katambi, alilitaka Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kujua chanzo cha ajali hiyo.

Naye Kaimu Mganga Mkuu Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, Dk. Abdulli Pumzi, alithibitisha kupokea majeruhi 25 na kati ya hao waliolazwa ni wanne.

Dk. Pumzi aliwataja waliolazwa ni Pili Majaliwa (40), mkazi wa Shinyanga; Launcia Kilini (38), Nachingwea na Deus Enock (4) kutoka Ilemela mkoani Mwanza, na kwamba wataendelea kutibiwa kutokana na kupata majeraha makubwa ikiwamo kuvunjika mguu na sehemu za kifua.

# Wanaopotosha kuhusu dengue wapewa angalizo

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imewaonya wanaotumia mitandao ya kijamii kupotosha kuwa ugonjwa wa dengue unaweza kutibiwa na mafuta ya nazi na majani ya mpapai.

Imesema kuwa taarifa hizo zinaendelea kufuatiliwa kuhakikisha wahusika wanachukuliwa hatua.

Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akitoa hali ilivyo kwa magonjwa ya dengue, kipindupindu na tahadhari inayopaswa kuchukuliwa na wananchi kuhusu ebola.

Akizungumzia kuhusu dengue, Dk. Ndugulile alisema ugonjwa huo hadi sasa hauna tiba na kuwataka wananchi kuacha kupotosha ukweli kupitia mitandao ya kijamii.

Alisema kwenye mitandao ya kijamii watu wanaongelea mambo mengi kuwa mtu anaweza kutibu dengue kwa kutumia mafuta ya nazi, majini ya mpapai au mbegu zake.

"Niwaombe sana wananchi kutosambaza hizo taarifa kwa sababu hazijathibitishwa kitaalamu kwamba vitu hivyo vinaweza kutoa majibu ama kutibu, niendelee kuwasisitiza wananchi waendelee kufuatilia taarifa kutoka vyombo vyetu kwa ajili ya matibabu," alisema.

Dk. Ngugulile aliongeza: "Serikali imeona taarifa mbalimbali mitandaoni ambazo tunaendelea kuzifuatilia kuhakikisha kwamba kwa wale wanaopotosha wanachukuliwa hatua stahiki."

Dk. Ndugulile alisema pamoja na kwamba ugonjwa huo umepungua, lakini zipo hatua zinazochukuliwa na serikali ikiwa ni pamoja na kudhibiti na kuondoa mazalia ya mbu ambazo zinaendelea maeneo tofauti.

Changamoto iliyopo mashine ya kupulizia dawa ya kuua mbu wakubwa hazipo nchini, lakini serikali inafanya jitihada za kuzinunua nje ya nchi," alisema.

Alisema huo ni mkakati wa ziara kwa sababu ili mbu awe mkubwa ataanzia kwenye viluilui ambavyo serikali inaendelea kuondoa mazalia yake.

Akizungumzia kuhusu ugonjwa wa ebola, Dk. Ndugulile alisema mpaka sasa Tanzania hakuna mgonjwa aliyegundulika na kuwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari hasa kwa wale wanaosafiri nje ya nchi.

Alisema serikali imeimarisha mifumo yake ya maabara, ili kuweza kuwabaini wagonjwa kwa haraka na kwa wale wanaoingia nchini wakitokea nchi zenye maambukizi hayo, wameweka utaratibu wa kuwafuatilia kwa ukaribu.

"Tunaomba wananchi wachukue tahadhari wanapomuona mtu ana dalili kama homa kali, anatokwa damu au kifo cha ghafla, kabla ya kumzika mtu wa namna hii tunaomba wawasiliane na mamlaka husika ili zikafanye uchunguzi wa mwili kabla ya mazishi," alisema.

Kuhusu ugonjwa wa kipindupindu mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Ndugulile alisema takwimu zinaonyesha unapungua ambapo hadi mwezi huu wagonjwa ni 361 na waliofariki ni watu sita.



Fundi wa kampuni ya Estim, akiendelea na kazi ya awamu ya kwanza ya upanuzi wa Barabara ya Morogoro, katika eneo la Kimara Stop over, jijini Dar es Salaam jana, itakayojengwa kwa njia sita kuanzia Kimara hadi Kibaha mkoani Pwani yenye urefu wa kilomita 19. **PICHA: JOHN BADI**.

# Wazee waomba sheria ya kulipwa pensheni

**Na Mwandishi Wetu,** MAGU

WAZEE wilayani Magu, mkoani Mwanza, wameiomba serikali kuharakisha utungaji wa sheria ya wazee ya kuwapatia pensheni kama inavyofanya kwa wenzao visiwani Zanzibar wanaolipwa pensheni jamii.

Wametoa kauli hizo wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wazee Ulimwenguni yaliyofanyika katika kijiji cha Lugeye, na kuratibiwa na Shirika la Kutetea Haki za Wazee la Maperece.

Kwa upande wa Tanzania visiwani, wazee hulipwa pensheni jamii ya Sh. 20,000 kila mwezi kwa kila mzee.

"Serikali itukumbuke, sisi ndiyo tumepigana kuiletea nchi hii uhuru, kwa nini tusisaidiwe? Tunaomba sheria ya wazee itungwe haraka, tupewe pensheni na bima ya afya," alisema mzee Luhende Mwebeya (74).

Ester Bulima, Medard Katafula na Mariam Tito, mbali na sheria ya wazee, walihimiza pia kupewa msaada wa lishe kwa kulinda afya zao.

Mratibu wa Shirika la Maperece, Julius Mwengele, alisema Sera ya Wazee iliyotangazwa miaka 16 iliyopita, hadi sasa haijatungiwa sheria jambo linalodaiwa kutoa mianya ya ukatili dhidi yao.

Aliziomba jumuiya za kibenki nchini, kuwasaidia mikopo wazee kwa ajili ya uzalishaji mali.


Mbunge wa Magu, Boniventura Kiswaga, alisema:

"Muswada wa sheria mpya ya bima ya afya uwe rafiki kwa wazee, niseme tu kwamba, wazee ni hazina, shule tulizosoma mmezijenga ninyi, sheria ya wazee ikija bungeni, mimi na wenzangu tutaipitisha."

Kiswaga aliwapatia wazee Sh. 500,000 taslimu, ili kuinuia mfuko wao wa kimaendeleo.

Mkuu wa Wilaya ya Magu, Dk. Philemon Sengati na Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya, Coletha Sanga, walihimiza usalama kwa wazee wote.

# Spika Ndugai awapa mbinu wabunge wanawake kukomesha ukandamizaji




Na Augusta Njoji

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewataka wabunge wanawake katika kipindi kilichobaki cha kumaliza Bunge la 11 waangalie namna ya kuwasilisha muswada binafsi wa kuondoa sheria kandamizi kwa wanawake.

Ndugai alitoa kauli hiyo jana bungeni baada ya kujibiwa swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Silafu Maufi, ambaye alihoji serikali ina mpango gani kutoa elimu na kuhakikisha wajane hawanyanyasiki kutokana na kuwepo na mfumo dume.

Mbunge huyo alisema wajane ni wengi, lakini wagane ni wachache kwa sababu mwanaume ni rahisi kuweka haraka mke mwingine, hivyo kuhoji serikali ina mpango gani wa kuwawekea mpango wa kuwawekezea kiuchumi ili wapate mikopo waweze kuhudumia familia zao.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, alikiri kumekuwapo na ubaguzi kwenye mirathi kwa wajane kutokana na mfumo dume.

Baada ya majibu hayo, Ndugai aliutaka Umoja wa Wabunge Wanawake (TWPG) kuhakikisha katika mikutano mitatu iliyobaki wawezeshe muswada wa wanawake wasisubiri serikali pekee.

"Hebu fanyeni jambo moja la wanawake kwa mfano iwe ni marufuku kwa nchi yetu mama na familia yake kutolewa katika nyumba ya familia au mambo haya ya mirathi, Viti Maalum tufanye kitu," alisisitiza Ndugai.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alisema mgane anapobaki na watoto hundi zinazolipwa kama kuna malipo huandikwa kwa jina lake, lakini kwa wajane huwa tofauti anapewa masharti ya kulipiwa mahakamani na awe na muhtasari wa kikao cha upande wa mwanaume na ndipo malipo yafanyike kwa mgao maalum.

Dk. Mahiga alisema hakuna sheria yoyote inayompa mgane haki zaidi ya mjane au kwa namna yoyote kuonyesha ubaguzi.

Hata hivyo, alisema utaratibu unaofanyika unamtaka msimamizi wa mirathi kuwasilisha mchanganuo wa malipo na hundi huandikwa kwa wanufaika wote pasipo kujali jinsia zao.

"Pamoja na kuwa na sheria nzuri, kumekuwa na uelewa mdogo miongoni mwa baadhi ya wananchi kuhusu sheria, kanuni na taratibu zinazohusu masuala ya mirathi, kupitia RITA na wadau mbalimbali imekuwa ikitoa elimu kwa makundi mbalimbali kuhusu mirathi," alisema.

Alifafanua kuwa masuala ya mirathi yanasimamiwa na Sheria ya Mirathi Sura ya 352 ambapo inatoa utaratibu mzima unaohusu masuala yote ya mirathi, wosia, kufungua mashauri ya mirathi, usimamizi, pingamizi la msimamizi au msimamizi anapofariki au asipotenda haki.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Watu Wenye Ulemavu, Stella Ikupa (kushoto), akibadilishana mawazo na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, bungeni jijini Dodoma, juzi. **PICHA: OWM**

# Watalii 5,400 watembelea kisiwa Mafia

JUMLA ya watalii 5,412 wametembelea kisiwa cha Mafia hususan Hifadhi ya Bahari ya Hindi kwa mwaka 2017/18.

Hayo yalibainishwa jana na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mafia (CCM), Mbaraka Dau.

Dau alihoji ni watalii wangapi walitembelea kisiwa cha Mafia kwa kipindi hicho.

Akijibu, Kanyasu alisema kutokana na uzuri na sifa ya kisiwa hicho idadi ya watalii wanaotembelea imeendelea kuongezeka ambapo katika kipindi hicho watalii 5,412 walitembelea.

"Kati ya watalii hao, Watanzania walikuwa 252 na wageni 5,160. Idadi hii ya watalii waliotembelea Mafia ni sawa na ongezeko la asilimia 12 ukilinganisha na watalii 4,817 waliotembelea kisiwa hicho katika msimu wa mwaka 2016/17," alisema.

Alieleza kuwa katika kuhakikisha kuwa kisiwa cha Mafia kinafikika kwa urahisi, serikali inaendelea na mikakati ya kuboresha miundombinu ya kisiwa hicho ikiwamo kujenga meli na kuboresha maegesho ya meli katika Bandari ya Nyamisati na Mafia.

Awali alieleza kuwa kisiwa hicho ni moja ya eneo la kimkakati katika uendelezaji wa utalii wa fukwe nchini.

"Katika miaka ya karibuni kisiwa hicho kimekuwa kikitembelewa kwa wingi na wageni kutoka ndani na nje ya nchi," alisema.

Alisema wageni hao wamekuwa wakivutiwa na vivutio mbalimbali vinavyopatikana katika kisiwa hicho ikiwamo papa potwe, magofu ya kale, utamaduni na fukwe nzuri.

Aidha, alisema watalii wamekuwa wakivutiwa na michezo kwenye maji kama vile scuba diving, sport fishing and snorkeling na kuogelea na samaki aina ya papa.

# Mambo 4 fursa za ajira kwa vijana

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, ametaja mambo manne ambayo yatatekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, ili kukuza fursa za ajira kwa vijana kupitia makundi mbalimbali ngazi za elimu na waendesha bodaboda.

Mavunde alisema hayo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Esther Mmasi, ambaye alisema serikali imeonyesha nia madhubuti kupitia mikakati yake ya kuinua ajira kwa Watanzania.

"Je, ni kwa namna gani serikali imejipanga kuinua ajira kwa vijana kupitia makundi maalum kama vile vijana wa kidato cha nne, darasa la saba na waendesha bodaboda?" Alihoji. Mavunde alisema mambo hayo ni kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika sekta zenye uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira hususani kilimo biashara.

"Pia serikali itajikita zaidi kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji kwenye viwanda vidogo, vya kati na vikubwa ili kufikia lengo la asilimia 40 ya nguvu kazi nchini kuwa katika sekta ya viwanda ifikapo mwaka 2020 kupitia mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano(2016/17-2020/21)," alisema.

Jambo la pili ni kuendelea kuimarisha utekeleaji wa mfuko wa maendeleo ya vijana ambao unalenga kuwasaidia vijana kuweza kujiajiri kwa kuwapa mikopo ya masharti na mafunzo ya ujasiriamali.

"Kadhalika kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kukuza ujuzi nchini ambao umelenga kutoa mafunzo ya vitendo yatakayofanyika maeneo ya kazi, ili kuwapa vijana wengi fursa za mafunzo," alisema.

Alieleza serikali imeanzisha programu maalum ya kutambua ujuzi uliopatikana kupitia mfumo usio rasmi na kuurasimisha kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wale watakaobainika kuhitaji na kuwapa vyeti.

Mavunde alisema utaratibu huo unawapa fursa vijana ya kuendelea na mfumo rasmi wa mafunzo na pia kutambulika na waajiri au watoa kazi.

"Mpango wa nne ni mwaka 2017, serikali ilirekebisha kanuni za sheria ya usafirishaji za mwaka 2010 kwa lengo la kuruhusu bodaboda na bajaji kubeba abiria na kurasimisha ajira ya waendesha bodaboda na bajaji," alisema.

Alisema serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa azimio la wakuu wa mikoa la Novemba mwaka 2014 kuhusu kuongeza fursa za ajira kwa vijana kwa kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji na biashara, kutoa kipaumbele kwa kununua bidhaa na huduma zinazotolewa na vijana na kutoa mikopo ya masharti nafuu.

HABARI ARUSHA

# Tanzania kinara kudhibiti ujangili

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TANZANIA imekuwa kinara wa kudhibiti ujangili wa mazao yatokanayo na misitu kwa zaidi ya asilimia 70 katika nchi za Afrika, tofauti na miaka ya nyuma iliposhika nafasi ya nane kwa nchi zinazoongoza kwa vitendo vya ujangili.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangala, alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa tatu wa kimataifa wa Pan Afrika wa wataalamu wabobezi wa kupiga vita uhalifu wa wanyamapori na mazao yatokanayo na misitu.

Aliwataka wafanyabiashara haramu wa nyara za serikali ambao wamezificha kutokana na kushindwa kuzisafirisha nje ya nchi kuzisalimisha kwenye ofisi yake mara moja.

"Tumedhibiti ujangili kwa zaidi ya asilimia 90 ila ujangili wa mazao

ya misitu ndiyo umebaki kidogo na kuna baadhi ya majangili wana mazao ya zamani ya nyara za serikali na wanatafuta njia za kupeleka nchi za

jirani wakauze, niwatake wasalimishe bidhaa hizo ofisini kwangu mara moja," alisema.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na ushirikiano wa nchi za jirani kupitia askari wa Interpol na wiki iliyopita wamemkamata jangili maarufu nchini Uganda, anayefahamika kwa jina la Mawazo ambaye ni wakala mkubwa wa kukusanya nyara zilizovunwa zamani katika ukanda wa

Afrika Mashariki na Kati na hivi sasa anapelekwa Marekani kushtakiwa kwa kesi zinazomkabili.

Alisema biashara ya nyara za serikali inapungua kwa kasi, lakini ni lazima jitihada za pamoja za nchi hizo zifanyike ili kudhibiti kabisa suala hilo.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori nchini, Dk. Marhus Msuha, alisema mkutano huo ni muhimu kwa nchi na Afrika ikiwa ni pamoja na kuangalia migongano kati ya wananchi na wanyamapori kwa sababu wanyamapori wengi wamekuwa wakiathiri mifugo, mazao, kujeruhi

binadamu na wakati mwingine kuwasababishia vifo.

Alisema hivi sasa wanaangalia namna ya kutatua kero hizo na matumizi ya teknolojia kwa kufunga kamera maalum kwa wanyama ili kuwatambua wanapotoka ndani ya hifadhi na kwenda kwenye makazi ya binadamu ili askari wa wanyamapori waweze kuwarudisha.

Mkurugenzi wa Msaidizi wa Kuzuia Ujangili nchini na Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Taifa cha Kuzuia Ujangili nchini (TAWA), Robert Mande, alisema watapata fursa ya kubadilishana taarifa mbalimbali za kiintelijensia ambapo kila nchi itatoa uzoefu wake na kujifunza intelijensia za nchi nyingine.



Wajasiriamali wakiendelea na kazi ya kukarabati na kushona viatu kama walivyokutwa na mpigapicha wetu mtaa wa Nyakato Sokoni, jijini Mwanza. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Wasiochangia mlo shuleni kushtakiwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Karatu mkoani Arusha, Theresia Mahongo, ametangaza kuanza kuwachukulia hatua za kisheria, wazazi na walezi wanaokataa kuchangia chakula shuleni.

Aidha, amewaonya wahusika hao kuwa hatakaa kimya kwani wanatafsiri vibaya waraka wa serikali wa sera ya elimu bure na kukwepa kuchangia chakula shuleni.

Aliyasema hayo jana wilayani humo, katika Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika iliyoadhimishwa kiwilaya katika Kata ya Endabash.

Alisema kwa kutafsiri vibaya sera ya serikali na kutumia mwanya huo kukwepa kutimiza majukumu yao kama wazazi au walezi ni kosa kisheria.

Aliongeza kuwa ni kwa sababu wanapokataa kuchangia huumiza watoto waliopo shuleni na kusababisha kutofanya vizuri kwenye masomo.

"Sasa nasema, kuanzia sasa serikali hatutawaacha tutafuatilia kwa karibu na tutawachukulia hatua kali za kisheria dhidi ya wale wote wanaokwepa kuchangia chakula shuleni kwa kisingizio cha serikali inafanya kila kitu," alisema Mkuu wa Wilaya.

Mahongo alisema Rais John Magufuli alikuja na mpango endelevu wa elimu bure, ili kuwafikia watoto wengi nchini kupata elimu, lakini suala la chakula shuleni bado ni jukumu la mzazi au mlezi.

Alisema suala hilo limeonekana kuwa na changamoto zinazosababishwa na wazazi na walezi kutowajibika ipasavyo, licha ya waraka huo kuwekwa bayana kwa wazazi au walezi juu ya umuhimu wa kushirikiana na

walimu katika kuunda kamati zitakazohudumia wanafunzi.

Aidha, Mahongo alieleza kutoridhishwa na hali ya upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Endabash katika wilaya hiyo, kwani imechangia kwa kiwango kikubwa kuathiri taaluma na ufaulu.

Alisema hivyo kupita Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 Namba 21 imeainisha adhabu mbalimbali dhidi ya wazazi, wanaoshindwa ama kukaidi maelekezo ya serikali hivyo atatumia kuwachukulia hatua wahusika wote wanaokwepa majukumu yao.

"Sipo tayari kuona wilaya yangu inashuka kiwango katika ufaulu kwa sababu ya suala la chakula, kwa kutumia Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, tutahakikisha tunawashughulikia wazazi, walezi ambao wanakwepa majukumu yao," alisema Mahongo.

Mratibu wa Mradi wa Shirika lisilo la kiserikali la World Vision na waandaaji wa siku hiyo, Daniel Kirhima, wakati akitoa taarifa, alisema wanaunga mkono Siku hiyo ya Mtoto Afrika katika

kuhakikisha haki za watoto na wajibu zinatekelezwa ndani ya jamii.

Alisema World Vision imewafikia zaidi ya watoto 1,000 kutoka kata mbalimbali wilayani humo katika kutekeleza miradi ya kilimo, maji, afya na elimu ili kuhakikisha ustawi wa wanafunzi unakuwapo shuleni.

"Watoto hawa ni taifa la kesho wanapokuwa na ustawi bora ni hatua kubwa kwa taifa kwani tunaamini nyanja mbalimbali zitapata wataalamu bora, waliojengewa misingi imara toka ngazi za chini," alisema Kirhima.

Mwaka 1991 wakati huo uliokuwa Umoja wa Nchi Huru ya Afrika ambao sasa ni Umoja wa Afrika (AU), ulizindua Siku ya Mtoto wa Afrika, ambayo imekuwa ikifanyika kila mwaka Juni 16.

Lengo ni kuwaenzi na kuwakumbuka watoto waliouawa katika Kitongoji cha Soweto huko Afrika ya Kusini wakati wa utawala wa ubaguzi wa rangi.

## Wafanyabiashara wafundwa kujisajili

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA wamekumbushwa kusajili biashara zao kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela), ili waweze kuingia katika soko la ushindani nje na ndani ya nchi.

Akizungumza jana jijini Arusha katika mafunzo ya siku mbili kwa wataalamu wa halmashauri za mkoa wa Arusha na mashirika binafsi, Mkurugenzi wa Utawala na Fedha wa Brela, Bakari Mketo, alisema usajili ni muhimu ili kulipa kodi.

Alieleza kuwa wametembelea Kanda ya Kaskazini kutoa elimu ya usajili kupitia mfumo mpya wa kielektroniki (OBS) ili kuwawezesha wafanyabiashara kuutumia na kufahamu taratibu za Brela.

Alisema wakala huyo amerahisisha usajili badala ya kutumia makabrasha, wanatumia mfumo mpya wa kielektroniki.

Aliwaambia kuwa husajili kwa haraka na kumpunguzia mhusika gharama za kufuata huduma hiyo mbali.

"Shida kubwa watu wengi wanaosajili kampuni au biashara zao hawafahamu kama wanatakiwa kulipa Sh.5000 kila mwaka kwa ajili ya majina ya biashara zao na Sh. 22,000 ya huduma nyingine zote hufanywa kila mwaka," alisema Mketo.

Anaeleza kuwa yote hayo hulipwa Brela na kufafanua kuwa wengine wanalipa wanaposajili na miaka inayofuata hawatoi malipo hayo na kujilimbikizia madeni makubwa.

Alisema kibaya zaidi wafanyabiashara wengi wanaposhindwa kuendesha biashara zao wanatoa taarifa Mamlaka ya Mapato (TRA).

Wakati hayo yakitokea Brela inaendelea kutoza kodi zao kila mwaka kwa sababu hawana taarifa za ufungaji wa biashara husika.

"Nawaomba toeni taarifa zenu kwenye taasisi zote kama TRA, Brela na halmashauri ili wafahamu na wasitoze kodi," alisisitiza.

Privanusi Katilila, mdau wa Brela alisema serikali inafanya mabadiliko ya utoaji huduma ili kuwafikia watu wote kwa kuboresha mfumo wa usajili biashara kwa njia ya kielektroniki.

"Kikubwa tunachoona wafanyabiashara wengi vijana wametengeneza madeni kwa kutofahamu unaposajili biashara kuna kodi za kila mwaka

zinazolipwa Brela. Hivyo unapofunga biashara lazima kutoa taarifa Brela , TRA, Halmashauri ili wasiendelee kukutoza kodi," aliongeza.

Suzan Senso kutoka Kitengo cha Miliki Bunifu cha Brela alisema, wapo mkoani Arusha kwa siku tano, lengo kuelimisha taratibu na mfumo wa Brela unavyofanya kazi, ili kusaidia wadau wa mkoa huo kutumia kusajili biashara zao.

# Wafanyakazi MoCU kuibua changamoto

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WATUMISHI wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), wamehimizwa kuibua na kutaja changamoto zinazowakabili ili zipatiwe ufumbuzi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo, Profesa Alfred Sife, aliyesema hayo jana, alipofungua wiki ya utumishi katika chuo hicho inayoadhimishwa kila mwaka Juni, ili kutathmini utendaji kazi na namna ya kuboresha huduma chuoni hapo.

Profesa Sife alisema katika kuadhimisha wiki hiyo watumishi watapewa nafasi kuwasilisha kero zao kwa wakuu wa vitengo vyao, idara na vitivo mbalimbali, ili kuja na mipingo ya kutatua changamoto hizo lengo likiwa kuimarisha huduma chuoni hapo.

"Wiki ya utumishi wa umma kwa mwaka huu tunaadhimisha kwa namna tofauti kama tulivyopewa maagizo na Ofsi ya Rais, Utawala Bora. Kila taasisi tunayoisimamia tunasikiliza changamoto zinazowakabili watumishi pamoja na wadau tunaowahudumia ili kuboresha huduma zetu," alisema Profesa Sife.

Zipo changamoto zilizoonekana zinahitaji kutizamwa ili kuboresha huduma, hivyo ilituagiza tusikilize kero hizo na kuandika ripoti itakayowasilishwa serikalini kwa ajili ya utekelezaji zaidi.

Jane Mnyombi ni Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu, MoCU, alisema uwepo wa mfumo huu utasaidia kupata changamoto nyingi na kuomba uongozi wa chuo hicho kuzitatua bila kuangalia itikadi za kisiasa na kidini kwa ukarimu na mhusika atakayelalamikiwa.

Kwa upande mwingine Mhadhiri wa Chuo Kelvin Lucas, alisema kuwa utaratibu huu ni huru na unaweza kumsaidia mtoaji maoni kuwa salama kutokana na kutoandikwa kwa jina la mhusika.

"Tunaipongeza serikali kwa utaratibu huu ulioanzisha kwani ni huru na unaweza kuwasaidia kutatua changamoto zinazoikabili taasisi husika bila kuwapo kwa migogoro baina ya watumishi na uongozi," alisema Lucas.



Mmoja wa wanachama wa vikundi vya vicoba vilivyo chini ya mradi wa kuwakomboa wanawake na watu wenye ulemavu kiuchumi katika Tarafa za Tarakea na Userri, wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro, chini ya Shirika lisilo la kiserikali la AJISO, akishiriki uchangiaji damu kutatua tatizo la upungufu wa damu katika hospitali za wilaya hiyo. Vikundi hivyo vimewezeshwa na AJISO kwa ufadhili wa Shirika la Bread for the World la Ujerumani. **PICHA: JAMES LANKA**

# Waliokimbia Chadema wasimikwa CCM

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MADIWANI wawili wa Chadema waliohamia CCM Deogratius Mushi wa Kata ya Kibosho Magharibi na Bertin Mkami wa kata ya Uru Shimbe, wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro wameapishwa baada ya kupita bila kupingwa.

Madiwani hao wameapishwa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, Judith Mahole, baada ya kukabidhiwa vyeti vyao na Msimamizi wa Tume ya Uchaguzi, Kastory Msigala ambaye pia ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Moshi.

Madiwani hao, walijiuzulu mwezi Aprili 2019, wakitokea Chadema na kujiunga na CCM, kwa kile walichoeleza kuwa ni kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa baada ya kuapishwa, Mushi alisema kwa sasa anakwenda kufanya kazi ya kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM, na kuwaletea wananchi maendeleo ya kweli.

"Kwa sasa niko kwenye chama taasisi, nakwenda kutekeleza ilani ya chama kilichoko madarakani na kuwaletea wananchi maendeleo ambayo waliyakosa kwa kipindi chote cha miaka minne, ambayo nilikuwa kwenye chama ambacho hakina ilani," alisema Mushi.

Aidha, alisema moja ya mambo ambayo anakwenda kuyatekeleza kwa sasa katika kipindi kilichobaki, ni usambazaji umeme, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami na moramu, usambazaji wa maji, pamoja na ununuzi wa gari la kubebea wagonjwa.

"Nakwenda kushughulika na kero zote za wananchi ikiwa ni pamoja na kukomesha dhuluma, uonevu, kusaidia yatima na wajane na kwa muda uliobaki, nitatekeleza miradi ya maendeleo, ambayo nilishindwa kuikamilisha," alisema Mushi bila kueleza atafanyaje na atapata mbinu gani.

Akizungumzia hatima yake Mkami alisema amechoka na upinzani na kwamba sasa wamerudi katika chama tawala ili kushirikiana na Rais John Magufuli, kutekeleza ilani na ahadi zilizotolewa wakati wa uchaguzi.

Alisema ameamua kurudi CCM, baada ya kuona hata kule kuna udhaifu viongozi hawashirikiana na wananchi, wakiwamo watendaji wa chama hicho, madiwani na wapigakura kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Alisema kwa sasa anakwenda kuhakikisha vikundi vya wanawake, vijana na walemavu wanapata fursa ya kupata mikopo isiyokuwa na riba inayotengwa na Halmashauri ya Moshi.

Aidha, ametangaza kukamilisha mradi wa umeme na ukarabati wa shule za msingi na sekondaria na kuhakikisha wanaokula mali na fedha za ushirika wanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

# CCM waazimia kushinda Serikali za Mitaa

**Na Paul William,** MOSHI

MWENYEKITI wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa (UVCCM), Kheri James, amewataka Makatibu na Wenyeviti wa Jumuiya hiyo kufanyakazi kwa bidii kukipa chama chao ushindi kwenye uchaguzi ujao.

Aliwaagiza viongozi hao kuhakikisha kuwa CCM inashinda katika uchaguzi za serikali za mitaa katika wilaya zao.

Kauli hiyo ya UVCCM imekuja baada ya bajeti ya serikali kuwasilishwa bungeni wiki iliyopita na Waziri wa Fedha, Dk. Phillip Mpango, iliyoainisha vipaumbele vya serikali kwa mwaka 2019/2020 na kueleza kuwa eneo mojawapo lililotengewa fedha ni Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Vijiji unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

James ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM alitoa maagizo hayo juzi mkoani Kilimanjaro alipokuwa akizungumza na vijana wa mkoa wa Kilimanjaro kuhusiana na uzinduzi wa mkakati wa Kilimanjaro ya kijana wenye lengo la kuleta ushindi zaidi kwa CCM.

Alisema kuwa, vijana ndiyo injini ya chama na kuwataka kuhakikisha kuwa wanashinda kwa kishindo na kuwataka viongozi wa UVCCM wanajitoa kwa nguvu kubwa kukipigania chama ili kishinde na kunyakua mitaa mingi katika uchaguzi huo wa serikali za mitaa na vijiji.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa, hayupo tayari kufanyakazi na viongozi wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa CCM ambao hawajitoi kikamilifi kukikitetea chama chao.


Aliahidi kuwa uchaguzi za serikali za mitaa uitakuwa ni kipimo cha viongozi hao kuhakikisha chama kinashika hatamu.

"Chama kinawategemea sana vijana katika kuhakikisha kinashinda katika uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji pamoja na uchaguzi mkuu mwakani na hili litafanikiwa endapo mtajitoa kwa nguvu bila woga pamoja na kuachana na usaliti ambao vijana wengi mmekuwa ni watuhumiwa," alionya James.

Alisema kuwa, jukumu la vijana katika chama si kukipangia mgombea wanayemtaka wao bali ni kuhakikisha mgombea atakayepitishwa na chama anashinda kwa kishindo bila kujali ni nani na kuwataka kushirikiana na jumuiya nyingine za chama kuleta ushindi.

Mjumbe huyo wa kamati kuu alisema kila mara uchaguzi nchini unaendeshwa kwa uhuru, uwazi na haki na CCM imekuwa ikishinda kwa haki.

Ukurasa 18



**Mshauri Rais Marekani awasha moto eneo la Mashariki ya Kati**

## UCHAMBUZI:

Waandishi Zanzibar waazimia kukemea wenye kauli chochezi



Ukurasa 19

**Kimataifa**



**AfcFTA kutimiza ndoto za soko huru Afrika**

Ukurasa 14


# siasa

JUMATANO JUNI 19, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




**Rais wa zamani wa Misri azikwa baada kufariki dunia mahakamani**

Ukurasa 17

## BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano

MZEE Pius Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salama na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia mshauri muhimu wa serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.

Pia, Mzee Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mzizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.

Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu na kuundwa Muungano huo,

Endelea 16




Spika wa Bunge mstaafu, Pius Msekwa. **PICHA: MTANDAO**

**Vita yanukia eneo la Ghuba baada ya kushambuliwa meli kubwa za mafuta** Ukurasa 20

# AfcFTA kutimiza ndoto za soko huru Afrika

- Ni 'ndoto' iliyobuniwa na wapigania uhuru



Viongozi wa mataifa ya Afrika wakiwa Makao Makuu ya Umoja wa Afrika (AU), nchini Ethiopia. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mashaka Mgeta**

SUALA la upatikanaji masoko kwa bidhaa zinazozalishwa Afrika ni miongoni mwa changamoto zinazozikabili nchi zilizopo barani humo na hivyo kuzifanya zitegemee zaidi masoko ya nje.

Hata hivyo, masoko ya nje kwa bidhaa na huduma zinazotoka Afrika zimekabiliwa na vikwazo vikiwamo viwango vikubwa vya ubora visivyolingana na teknolojia za uzalishaji kwenye nchi hizo.

Mazingira ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na upatikanaji duni na usiokuwa wa uhakika wa nishati, ubovu wa miundombinu kama barabara, teknolojia duni na mengineyo kama hayo, yamesababisha bidhaa na huduma zinazozalishwa barani Afrika kushindwa kuhimili ushindani kwenye soko la kimataifa.

Badala yake, sehemu kubwa ya bidhaa na huduma zinazotumika Afrika zimekuwa zinatoka nje ya bara hilo, hivyo kuzifanya nchi za kiafrika kuwa tegemezi zaidi na zinazoingiza bidhaa nyingi, kulipa fedha nyingi za kigeni zaidi kuliko zinazotoka nje ya mipaka yake.

Hali hiyo inatokea wakati ambapo suala la kuwapo kwa ushirikiano na mwingiliano wa watu, usafirishaji wa bidhaa na huduma ndani ya mipaka ya bara hilo, limezungumzwa na kujadiliwa kwenye vikao vingi vya wakuu wa nchi za Kiafrika, lakini pasipo na ufanisi wowote katika utekelezaji wake.

Badala yake, nchi za Kiafrika 'zilijimega' na kuunda ushirikiano wa kikanda kama ilivyo kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Nchi za Magharibi mwa Afrika (ECOWAS) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Si kwamba kuwapo kwa jumuiya hizo na nyingine zinazofanana na hizo, hakutoi tafsiri ama maana ya kutokuwa na umuhimu kwa maendeleo ya Afrika na ustawi wa watu wake, la hasha, lakini kumepewa kipaumbele zaidi na kuimarishwa kuliko ilivyo kwa upande wa ukanda wote wa bara la Afrika.

**ENEO HURU**

Hata hivyo, matumaini mapya ya kuondokana na utegemezi huo yameanza kuonekana baada ya mchakato wa muda mrefu wa kutaka kuwapo eneo huru la biashara kwa nchi hizo kukamilika.

Kufikiwa kwa mchakato huo kunatarajiwa kuongeza chachu ya ushindani na ukuzaji wa biashara na huduma ndani ya bara la Afrika, hatua itakayochangia pia kulifanya eneo hilo lenye idadi kubwa ya watu, kuwa soko lisilotegemea zaidi bidhaa kutoka nje.

Aprili 29, mwaka huu, nchi kadhaa zilizo wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) ziliridhia kuwapo Mkataba wa Eneo la Biashara Huru Afrika (AfcfTA) na ukaanza kutekelezwa Mei 30, mwaka huu.

Umuhimu wa mkataba huo haustahili kubezwa kwa vile unakisiwa kuwa eneo kubwa zaidi la biashara duniani, tangu kuanzishwa kwa Shirika la Biashara Duniani (WTO) mwaka 1994.

Nchi 44 kati ya 55 zilizo wanachama wa AU zilianza kusaini AfcFTA na hivyo kuwa kigezo kinachoashiria viongozi wa mataifa hayo wanavyokusudia kufikia dira ya muda mrefu ya mwingiliano rasmi wa shughuli za biashara na uchumi barani humo.

Tangu kuzinduliwa kwake, AfcfTA imezidi kupata uungwaji mkono na kwamba idadi ya nchi zilizosaini zimeongezeka kufikia 52.

Nchi zilizosaini AfcFTA tangu awali hadi sasa zimefikia 52 wakati 22 zimeridhia mkataba huo, 15 zimeshawasilisha nyaraka za kuridhia mkataba huo kwa AU na 7 zimeridhia lakini bado hazijawasilisha nyaraka zao.

Wakati Eritrea, Nigeria na Benin hazijasaini, utaanza kutumika rasmi siku 30 baada ya idadi ya nchi inayohitajika kwa nchi zilizoridhia kuwasilisha nyaraka zao AU.

Kwa ukanda wa Afrika Mashariki, nchi za Tanzania, Burundi na Sudani Kusini hazijaridhia mkataba wa AfcFTA, ingawa ni miongoni mwa nchi zilizousaini.

Ucheleweshwaji wa baadhi ya nchi kuridhia na kuwasilisha nyaraka zao AU ni miongoni mwa changamoto dhidi ya utekelezaji wa AfcFTA.

Kwa mfano kuna haja ya kurahisisha miundombinu ya kiuchumi, kurahisisha uhuru wa kusafirisha bidhaa na watu kutoka nchi moja kwenda nyingine.

Hali hiyo itajumuisha kuunganisha mitandao ya barabara, reli na kupunguza gharama kubwa katika sekta ya usafiri na usafirishaji.

"Tumeonya kuhusu uanzishwaji wa taasisi nyingi za AU, hivyo tunasisitiza AU inapaswa kuwa makini katika matumizi ya rasilimali fedha, lakini vinginevyo tunaunga mkono jitihada za kuanzishwa AfcFTA," anasema Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi, Geoffrey Jideofor Kwusike Onyeama, wakati wa mkutano wa 32 wa wakuu wa AU uliofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia.

Mtaalamu wa masuala ya uchumi wa dunia, Profesa Landry Signé anakadiria kuwa kupitia mafanikio ya AFcfTA, Afrika itawaunganisha wateja katika biashara inayokadiriwa kufikia thamani ya Dola za Marekani trilioni 6.7 ifikapo mwaka 2030. Dola moja kwa mujibu wa taasisi zinazobadilisha fedha za kigeni ni sawa na Sh. 2,300.

Pia anasema AfcfTA itakuwa na manufaa makubwa katika utengenezaji bidhaa na maendeleo ya viwanda, utalii, ushirikiano wa kikanda na mageuzi ya kiuchumi.

Kamisheni ya Uchumi wa Umoja wa Mataifa kwa Afrika (UNECA) yamekisia kwamba utekelezaji wa AFcfTA utaongeza biashara inayofanyika ndani ya bara la Afrika kwa kati ya asilimia 15 na 25 zikiwa na thamani ya kati ya dola za Marekani bilioni 50 na bilioni 70 ifikapo mwaka 2040.

Kiwango hicho ni kikubwa kufikiwa ikilinganishwa na hali ilivyo kabla ya kuanzishwa kwa AFcfTA.

> Si kwamba kuwapo kwa jumuiya hizo na nyingine zinazofanana na hizo, hakutoi tafsiri ama maana ya kutokuwa na umuhimu kwa maendeleo ya Afrika na ustawi wa watu wake, la hasha, lakini kumepewa kipaumbele zaidi na kuimarishwa kuliko ilivyo kwa upande wa ukanda wote wa bara la Afrika.

Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) nalo linaakisi kwamba, kupitia AFcfTA, kukua kwa bara hilo, ubora wa bidhaa na soko la ajira kutaliwezesha kupanda katika viwango vya ushindani duniani.

Ongezeko la kulifikia soko la bidhaa na huduma linatarajiwa kuchagiza ushindani kwenye viwanda na ujasiriamali na mipango mizuri ya matumizi ya rasilimali.

**VIPENGELE**

Wakati hatua ya kuiridhia AfCFTA ikipaswa kuibua shangwe, kazi imebaki kubwa kutokana na vipengele muhimu vya mkataba huo kutokamilika, ikiwamo uthibitisho wa nchi wanachama kuhusu tozo za kibiashara na huduma, kanuni za asili, uwekezaji, ushindani na uwezekano wa kufanyika kwa biashara mtandao.

Kiwango ambacho AfCFTA itapunguza vikwazo kwa biashara za ndani ya bara la Afrika kwa kiasi kikubwa inahusishwa na makubaliano yanayoendelea.

Hali hiyo inatoa mwelekeo wa makubaliano yanayolenga zaidi bidhaa na huduma kulifikia soko na masuala ya kanuni.

Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kupitia namba 0754691540 ama barua pepe: mgeta2000@yahoo.com.

UCHAMBUZI

# Wateuliwa wajue cheo ni dhamana, wanapoondolewa ndivyo siasa ilivyo

**Na Sabato Kasika**

CHEO ni dhamana na uongozi ni utumishi, ni dhana zilizozoeleka miongoni mwa Watanzania, ingawa baadhi yao ni kama wamezi-weka pembani na kudhani kwamba nafasi wanazoteuliwa au kuchaguliwa basi ni haki yao.

Wapo wanaoamini kuwa cheo ni matokeo ya jitihada za mtu binafsi na si dhamana ambayo anapewa na kwamba kupata cheo kunatokana na elimu yake au uzoefu ama uwezo wa kukuza uhusiano mzuri kati yake na watu wengine.

Wapo wanaofikia kusema kuna haja ya kuondokana na fikra za kijamaa kwamba cheo ni dhamana na uongozi ni utumishi.

Hawa wanasisitiza kuwa cheo ni matokeo ya jitihada za mtu binafsi na si dhamana ambayo mtu anapewa.

Hata hivyo, ukweli unabaki pale-pale kwamba cheo ni dhamana kama ambavyo inasisitizwa kwenye Ahadi ya 5 ya Mwanachama wa TANU ambayo imerithiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Ahadi hiyo inasema: "Cheo ni dhamana, sitakitumia cheo changu au cha mtu mwingine kwa faida yangu."

Hilo ndilo jambo la msingi la kutambua maana ya dhana hii ya cheo ni dhamana.

Kwa mujibu wa wataalamu wa lugha ya Kiswahili, neno dhamana ni kama kitu au ahadi inayotolewa kumdhamini mtu anayetaka kukopa mali au anayekabiliwa na mashtaka mahakamani.

Aidha, ni kitu apewacho mtu ili atimize jambo fulani, kama kuwa katika ofisi ya umma au kutimiza wajibu mwingine wowote, vinginevyo anaondolewa.

Ni muhimu kwa maana hiyo kueleweka kwamba hata kama mtu amesoma kiwango gani cha elimu na akapata cheo kutokana na elimu na uzoefu wake, kumbe sehemu anayofanyia kazi inaweza kuendelea kuwapo bila yeye.

Hivyo ni vyema wanaopewa vyeo wakatambua kuwa wameshikilia dhamana.

MSINGI WA UTANGULIZI

Msingi wa utangulizi nilioanza nao hapo juu ni mkutano wa saba wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aprili mwaka 2012, uliibuka mjadala mkali uliosababisha mawaziri sita na naibu wawili kupoteza nafasi zao.

Mawaziri hao walitoswa baada ya kutajwa au kuhusishwa na madudu ya usimamizi usiofaa wa fedha za serikali kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Pia mawaziri hao waliguswa na Ripoti za Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali (PAC), Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC) na Ardhi, Maliasili na Mazingira za mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Cha ajabu baada ya kutemwa tu zikaibuka kauli mbalimbali za kushangaza zilizotolewa na baadhi yao pamoja na wapambe wao kwamba wameonewa.

Kuna waziri alimwandama aliyekuwa naibu wake, akidai kwamba alimgeuka kwenye baadhi ya maamuzi, hali ilionyesha wazi kuwa hakukubaliana kuondolewa katika nafasi hiyo.

Mbali na huyo, kuna waziri mwingine ambaye aliibuka na kudai kwamba alionewa, akisema bila kumumunya maneno kwamba aliondolewa kwa sababu ya fitna na chuki.



Rais John Magufuli akiwa katika shughuli ya kuapisha wateule wake. **PICHA: MTANDAO**

Ilifikia hatua ya baadhi yao kuibuka na mbinu mbalimbali kwenye majimbo yao kuhamasisha wananchi kufanya mikutano ya kuwasafisha au maandamano.

Na kwa nyakati tofauti, baadhi ya wafuasi wao waliandika mabango ya kuwasafisha kwamba hawana makosa yoyote, na wengine wakitishia kutopigia kura Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Walisahau dhana ya kuwa cheo ni dhamana wakiamini kuwa haitatokea wakaondolewa kwenye nafasi walizokuwa wakishikilia na kujikuta wakilalamikia mamlaka za uteuzi.

Jambo la msingi hapa ambalo walalamikaji walipaswa kulifanya ni kuendelea na majukumu mengine kama kawaida, badala ya kulalamika.

Nimeanza kwa mifano hiyo michache ili kuonyesha ni jinsi gani baadhi ya viongozi wanaamini wakishateuliwa au kuchaguliwa, basi huwa ni kwa maisha yao yote kitu ambacho ni kupotoka.

Ieleweke kwamba unapoteuliwa au kuchaguliwa katika nafasi fulani ya uongozi, unaapishwa na kupewa kanuni unazopaswa kuzizingatia wakati ukitekeleza majukumu yako, lakini ukienda kinyume kuna uwezekano wa kuondolewa.

Hata hivyo, somo la cheo ni dhamana linaelekea kueleweka kwa sasa tangu kuingia madarakani serikali ya awamu ya tano mwishoni mwa mwaka 2015, kitu ambacho ni cha msingi.

Hadi sasa kuna zaidi ya mawaziri 10 ambao wameondolewa kwenye nafasi zao, na wanaendelea kutumikia wananchi wao kama kawaida bila kulalamika.

MAWAZIRI HAO

Mei mwaka 2016, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Charles Kitwanga alitumbuliwa na nafasi yake kuchukuliwa na Dk. Mwigulu Nchemba.

Pia Mei 2017 aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, Profesa Sospeter Muhongo alitumbuliwa.

Aidha, Septemba mwaka 2017, George Simbachawene (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) alijiuzulu katika nafasi hiyo baada ya jina lake kuonekana katika ripoti zilizotolewa na Kamati ya Bunge kwenye uchunguzi kuhusu madini ya Tanzanite.

Katika mwendelezo huo wa mawaziri kutumbuliwa, ulimgusa pia aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii Profesa Jumanne Maghembe na naibu wake Mhandisi Ramo Makani (Wizara ya Maliasili na Utalii).

Wengine ni Dk. Nchemba aliyerithiwa na Kangi Lugola, Charles Mwijage Wizara ya Viwanda na Uwekezaji, Charles Tizeba (Waziri wa Kilimo) na Nape Nnauye (Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo).

Mwingine ni aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Susan Kolimba aliyeachwa Septemba 2018, na nafasi yake ikachukuliwa na Dk. Damas Ndumbaro.

Hivi karibuni, mrithi wa Mwijage katika Wizara ya Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda naye aliondolewa kwenye nafasi hiyo.

La msingi hapa wote hawa wanaendelea kuwatumikia wananchi katika nafasi nyingine bila malalamiko.

Hiyo inaonyesha ni jinsi gani wanatambua maana nzima ya dhana ya cheo ni dhamana, ambayo kimsingi ni vyema kila kiongozi aizingatie.

Kwamba hawa hawajaenda majimboni kulalamika kwa wapigakura kudai wameonewa kama ambavyo iliwahi kutokea kwa baadhi ya mawaziri walioondolewa madarakani mwaka 2012, wakatafuta kila njia ili kuonekana wameonewa.

Kama nilivyosema, wenye mawazo ya aina hiyo ni wale ambao wanakalia ofisi za umma na kusahau kwamba cheo ni dhamana, lakini kwa yule anayejua hilo anaachia ngazi na maisha yanaendelea kama kawaida.

Mawaziri wa sasa waliotumbuliwa wanaweza kuwa mfano wa kuigwa kwa ukimya wao ambao wameuonyesha, hasa kwa kutambua nafasi ya uongozi ni kama koti la kuazima ambalo mwisho wa siku litarudishwa kwa mwenye nalo.

Kimsingi hakuna aliyezaliwa akiwa na cheo au alizaliwa ili awe waziri bali anakuta nafasi hiyo baadaye, kwa kuchaguliwa ama kwa kuteuliwa, hivyo akiondolewa katika cheo ajue dhamana aliyokabidhiwa imeisha.

UCHAMBUZI

BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano

**Inatoka Uk. 13**

ameamua kuandika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho **Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar**, kinachoweka undani wa historia kwa hatua. Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa. Fuatilia...

'Kifungu cha 4 cha sheria iliyoridhia mkataba wa Makubaliano ya Muungano, ambayo ni namba 22 ya mwaka 1964, kinasomeka kama ifuatavyo:

"The Republic of Tanganyika and the Peoples' Republic of Zanzibar shall, upon Union Day and over after, be united into one Sovereign Republic by Tanganyika & Zanzibar."

Maneno "and and after' yaliyomo katika kifungu hicho ni muhimu sana, kwani yanamaanisha kuwa, Muungano huu utakuwapo milele na milele.

Bila shaka huo ndio ulikuwa utashi wa kisasa wa waasisi hao. Bila shaka hayo ndio yaliyokuwa makusudio na matarajio ya waasisi wa Muungano waliopitisha sheria hiyo.

Jambo lingine linalohusu usemi unaosikika kwamba, Muungano wa Tanganyika ni mfano pekee wa Muungano uliodumu kwa muda mrefu katika Bara la Afrika.

Ni kweli kabisa kwamba, Watanzania wengi wanajivunia siyo tu kuwapo kwa Muungano huu wa nchi zetu mbili za Tanganyika na Zanzibar, ambazo tayari zimekwisha kila moja kupata uhuru wake baada ya kufanikiwa kwa harakati zao za kujikomboa kutoka katika fedheha ya kutawaliwa na wakoloni, bali pia, wanajivunia ukweli uliopo kwamba, Muungano huu umeweza kudumu kwa kipindi kirefu hadi sasa, zaidi ya miaka hamsini. Wengine wanaendelea kusema kwamba, huu ni mfano pekee katika Afrika wa Muungano ambao umeweza kudumu kwa miaka yote hiyo bila kuvunjika, kama ilivyotokea katika baadhi ya nchi nyingine za Afrika.

Hapana shaka kwamba, ipo mifano ya nchi za Afrika zilizowahi kuungana, lakini, Muungano wao ukavunjika baada ya miaka michache tu. Baadhi ya mifano hiyo imeelezwa katika kitabu hiki, ambayo ni pamoja na nchi za Misri na Syria, ambazo ziliungana mwezi Februari 1958 na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Kiarabu, iliyopewa jina la United Arab Republic (UAR), lakini Muungano huo ulidumu kwa miaka minne tu hadi Septemba mwaka 1961, ulipovunjika.

Mfano mwingine ni nchi za Senegal na Gambia. Nchi hizo mbili ziliungana kuanzia tarehe 1 Februari, 1982 na kujulikana kwa jina la Senegambia. Muungano huo pia ulivunjika tarehe 30 Septemba, 1989, baada ya kuwapo kwa miaka saba tu.

Lakini, yafaa vilevile ijulikane kuwa, siyo Muungano wa Tanganyika na Zanzibar peke yake ambao unaweza kudumu hadi sasa, kwani Afrika inayo mfano mwingine wa Muungano wa nchi mbili, ambao umedumu kwa kipindi kirefu zaidi hata kuliko Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Muungano husika ni ule Muungano wa Jamhuri ya Cameroon, kwa kweli, Muungano huo wa Jamhuri ya Cameroon ni mfano wa kipekee kabisa, kutokana na changamoto ya kuwa na historia, mila na desturi zinazotofautiana sana baina ya nchi hizo mbili, kabla hazijaungana. Nchi za Tanganyika na Zanzibar hazikuwa na changamoto ngumu kama hizo, kwa ushahidi unaopatikana katika hotuba ya Rais wa Tanganyika, Mwalimu Julius Nyerere, katika bunge la Tanganyika, alipokuwa akiiliomba bunge hilo likubali kuridhia Mkataba wa Makubalino ya Muungano na Zanzibar, ambako Rais alitaja hoja ya udugu uliokuwapo baina ya nchi za Tanganyika na Zanzibar, kama mojawapo ya sababu kubwa za kuunganisha nchi hizi. Mwalimu Nyerere alisema hivi:

"Tanganyika na Zanzibar ni nchi ndugu. Tunashirikiana kwa historia, lugha, mila, tabia na siasa. Udugu wa Afro – Shirazi na TANU wote mnaufahamu. Udugu wa viongozi wa vyama hivi viwili haukuanza jana. Basi, tunazo sababu zote hizo za kutufanya tuungane na kuwa kitu kimoja".


Hali haikuwa hivyo hata kidogo kwa upande wa Cameroon, kwani mazingira ya nchi hizo yalikuwa ni tofauti kabisa. Wao hawakuwa na udugu wa aina hiyo uliokuwapo baina ya Tanganyika na Zanzibar, na wala hakukuwa na ushirikiano wa mila, lugha, tabia, wala udugu wa kisiasa.

Hali ya huko ilikuwa ni kwamba nchi ya Cameroon ilikuwa ikitawaliwa na Ujerumani kabla ya VitaVikuu vya Pili, (kama ilivyokuwa nchi ya Tanganyika).

Historia inatuambia kwamba, Wajerumani waliposhindwa katika vita hivyo, walinyang'anywa makoloni yao yote, na kuyagawa kwa mataifa yale yaliyoshinda, hususani, Uingereza na Ufaransa. Lakini, kabla ya makabidhiano hayo, nchi ya Cameroon kwanza iligawanywa katika nchi mbili tofauti, yaani, Cameroon ya Mashariki na Cameroon ya Magharibi. Cameroon ya Mashariki iligawiwa kwa Ufaransa kupewa jina la 'French Cameroon'; wakati Cameroon ya Magharibi iligawiwa kwa Uingereza na kupewa jina la 'British Cameroon'.

French Cameroon ilipata Uhuru wake tarehe 1 Januari, 1960. Lakini, kabla Waingereza hawajatoa uhuru kwa sehemu yao ya British Cameroon, walifanya zoezi la kura ya maoni ya kuwauliza wananchi kama wanapenda kujiunga na wenzao wa Cameroon ya Mashariki wanaozungumza Kifaransa (kutokana na kwamba awali walikuwa chini ya utawala wa Wafaransa); au kama wanapenda kujiunga na Nigeria inayosema Kiingereza kama kwao.

Zoezi hilo lilifanyika mwezi Februari, 1961. Kura hiyo ya maoni ilileta mgawanyiko mkubwa, ambako sehemu ya kaskazini ya British Cameroon iliamua kujiunga na Nigeria, na sehemu ya kusini ikachagua kujiunga



Rais John Magufuli ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCM (kushoto) akiwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein. **PICHA: MTANDAO**

na Cameroon ya Mashariki. Kutokana na uamuzi huo, nchi hizi mbili (kati ya Cameroon ya Mashariki iliyokuwa awali inatawaliwa na Ufaransa); na sehemu ya kusini ya Cameroon ya Magharibi (iliyokuwa awali inatawaliwa na Uingereza ); ziliungana rasmi tarehe 1 Octoba, 1961. Muungano huo ulipewa jina la "Federal Republic of Cameroon", na umeendelea kuwapo hadi leo hii. Hiyo ni miaka mingi zaidi kuliko Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaliwa mwaka 1964, zaidi ya miaka miwili baadaye.

Lakini, mazingira yao yalikuwa na changamoto kubwa sana, kwani, tofauti na udugu ulikuwepo baina ya Tanganyika na Zanzibar ulioelezwa katika hotuba ya Rais Nyerere, vitabu vya historia ya nchi hiyo vinaeleza kuwa :

"The federal structure was designed to meet the challenges posed by Cameroon' s racial, tribal, religious and political diversity."

Yaani: Muundo wa Muungano ulikusudiwa kutoa majibu kwa changamoto nyingi walizokuwa nazo na tofauti za rangi, ukabila, udini, na tofauti za kisiasa.

Ndiyo kusema kwamba, walikuwa na changamoto ngumu kama hizo zilizotajwa, ikiwa ni pamoja na tofauti ya lugha. Lakini, pamoja na changamoto hizo kubwa zilizoibana nchi hiyo, bado waliweza kukubaliana kuungana; pamoja na kukubaliana kuwa na muundo huo wa serikali moja ulisaidiwa na kuunganishwa kwa vyama tawala vya siasa vya pande zote mbili mnamo mwaka 1965, muungano ambao ulizaa chama cha Cameroon National Union. (Pengine ndiyo sababu Mwalimu Nyerere alikuwa na matumaini kwamba ujio wa Chama Cha Mapinduzi kungesaidia kuhamasisha kukubalika kwa muundo wa serikali moja katika Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kutokana na mfano huo wa Cameroon). Historia yao inaonesha kwamba, baada ya kuunganisha vyama vyao vya siasa, juhudi ziliendelea kwa hatua mbalimbali zilizokuwa zikichukuliwa na kuelekea kwenye muuundo wa serikali moja, ikiwa ni pamoja na hatua muhimu ya wananchi wote kupewa nafasi ya kupiga kura ya maoni kwa ajili ya kuamua jambo hilo. Kura hiyo ya maoni ilipata mwafaka wa wananchi, ambao uliiwezesha nchi hiyo kutunga katiba ya Muungano wa serikali moja ambayo ilianza kutumika mwaka 1972. Hata hivyo, mfumo huo wa serikali moja baadaye uliwaletea matatizo makubwa sana, kama tutakavyoona hapo baadaye katika sura ya sita ya kitabu hiki.

Kuna jambo moja jingine ambalo limekuwa likiwatatiza baadhi ya wananchi (hasa wa upande wa Tanzania Bara); nalo ni suala la itifaki inayotumika siku ya maadhimisho ya mapinduzi ya Zanzibar yaliyotekelezwa usiku wa kuamkia tarehe 12 Januari, 1964. Itifaki hiyo ni pamoja na kumpigia Rais wa Zanzibar mizinga 21 wakati wa sherehe hizo. Lakini, jambo hili lina maelekezo yake mazuri tu, kama ifuatavyo:

Neno "itifaki" ni tafsiri ya neno la Kiingereza "protocol" Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiingereza ya "Oxford Advanced Learner's Dictionary," neno hilo limepewa maana ifuatavyo, "A system of rules governing formal accession". Yaani, itifaki ni utaratibu au kanuni zilizowekwa kwa ajili ya kutumika kwenye matukio maalum.

Tukio la kumbukumbu siku yalipofanyika Mapinduzi ya Januari 1964 Zanzibar, ni tukio maalum kabisa katika historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kwani ni dhahiri kwamba, bila mapinduzi hayo, Muungano huu usingekuwapo.

Kwa ajili hiyo, ulitengenezwa utaratibu wa kutoa heshima kubwa kwa mapinduzi hayo, kwa njia hii ya kuyapigia saluti ya mizinga 21 kila maadhimisho yake yanapofanyika, yaani tarehe12 Januari ya kila mwaka. Siyo kwamba mizinga hiyo 21 anapigiwa Rais wa Zanzibar kwa wadhifa wake huo. Ndiyo sababu Rais wa Zanzibar hapigiwi mizinga anapowasili Tanzania Bara, kwa sababu anakuwa yuko ndani ya nchi yake, ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Maelezo haya pia yanahusu itifaki nyingine anazopewa Rais wa Zanzibar katika maadhimisho yasiyo na Siku ya Mapinduzi, kama vile, kuwasili kiwanjani baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano kuwa ameshakwisha kuwasili; na kuwasili kwa msafara unaosindikizwa na pikipiki za polisi, kama anavyofanyiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano katika maadhimisho ya siku za kitaifa. Kwa hiyo, basi, yafaa izingatiwe kwamba, itifaki zote hizi zinatolewa kwa Rais Zanzibar katika siku hiyo maalum tu, kama kielelezo cha heshima kwa mapinduzi matukufu yaliyofanyika siku kama hiyo mwaka 1964 . Kwa maneno mengine, heshima hiyo inatolewa kwake katika wadhifa wake kama mwakilishi wa Mapinduzi hayo matukufu yaliyoikomboa Zanzibar na kuwezesha kupatikana kwa Muungano wa Zanzibar na Tanganyika.

Pius Msekwa
Dar es Salaam

**KUUNDWA KWA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR**

- **Mchakato wa Kuunda Muungano**

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulizaliwa tarehe 26 Aprili, 1964. Viongozi wakuu wa nchi hizi mbili ndio waliokubaliana kwa niaba ya wananchi wa nchi husika, waliposaini " Mkataba wa Makubaliano" ya kuunganisha nchi hizi mbili, mjini Zanzibar tarehe 22 ya mwezi huohuo. Kwa kuwa ulikuwa ni mkataba baina ya mataifa mawili tofauti; ili kuwa na uhalali wa kisheria ilikuwa ni lazima mkataba huo uridhiwe na mabaraza ya kutunga sheria ya nchi zote mbili. Kazi hiyo ilifanyika tarehe 25, Aprili 1964; ambapo Baraza la Mapinduzi la Zanzibar lilifanya hivyo katika kikao chake asubuhi ya siku hiyo; na Bunge la Jamhuri la Tanganyika nalo likafanya hivyo katika kikao chake mchana wa siku hiyo hiyo. Muungano huo ndio uliozaa nchi yetu hii, inayoitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwani, kabla ya Muungano huu, tulikuwa na nchi mbili tofauti, ambazo zilikuwa ni Jamhuri ya Tanganyika kwa upande mwingine. Viongozi wetu wakuu, yaani, marais wananchi hizi mbili, ndio waliokubaliana kuziunganisha ili kuunda Dola moja na taifa moja la wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maelezo ya kina zaidi kuhusu tukio hili kubwa la kihistoria, yametolewa katika sura za kitabu hiki.

**1.2. Madhumuni ya kitabu hiki**

Kwa hakika, wakuu wetu hao walikuwa na maono ya masafa marefu. Kwani wakati kitabu hiki kinaandikwa mwaka huu wa 2018, tayari mwaka wa hamsini na nne tangu Muungano huu ulipoasisiwa. Kwa hiyo tayari kuna vijana, na hata watu wazima wengi, waliozaliwa baada ya kuwapo kwa Muungano huu, ambao, wanastahili kufahamu vizuri historia yake. Na hayo ndiyo hasa madhumuni ya kitabu hiki. Tunaanza na ushuhuda wangu mimi mwenyewe, kuhusu mambo yaliyokuwa katika ile wiki moja ya 'matukio makubwa', ambayo kwa pamoja yalizaa muungano huu.

**1.3. Ushuhuda Wangu wa hayo Matukio Makubwa**

Wiki hii ya ' matukio makubwa' ambayo yalinihusu mimi mwenyewe moja kwa moja ilianza tarehe 20 Aprili, 1964, na kumalizika tarehe 27 Aprili, 1964, matukio muhimu ni haya yafuatayo:

**1.3.1 Kuitwa na Rais Nyerere, Ikulu**

Nikiwa Katibu wa Bunge, nilikuwa ofsini kwangu kama kawaida, mnamo saa saba za mchana, nilipokea simu kutoka Ikulu, kuniambia kwamba Rais Nyerere alikuwa anataka kuniona haraka. Ilinichukua chini ya dakika kumi kufika ofisini kwa Rais Nyerere, akaniambia kwamba, alikuwa na nia ya kuitisha Bunge la dharura, kwahiyo, akaniuliza, je, nahitaji muda gani kuwaita wabunge wote wafike Dar es Salaam kwa madhumuni hayo? Nilimjibu kwamba, "nitawajulisha mara moja juu ya wito huo, na nina hakika kwamba ndani ya siku mbili, wote watakuwa wameshawasili Dar es Salaam. Niliendelea kusema kwamba, kwa kuwa leo ni Jumanne, endapo utaona kuwa inafaa, Bunge linaweza kukutana siku ya Ijumaa ya wiki hii," Rais akafurahi, akaniagiza niendelee na mpango huo, lakini, kwa msaada mkubwa sana wa Shirika la Posta na simu, kwani nyakati hizo, ukitaka kupiga simu ni lazima umuombe opereta wa posta iliyoko katika eneo lako, yeye ndiye akuunganishe na namba unayohitaji. Kwa utaratibu huo, ilikuwa ni lazima kusubiri muda mrefu sana kabla haujaunganishwa. Lakini, kwa dharura hiyo, niliomba msaada wa Mkuu wa Posta mwenyewe wa Makao Makuu ya Posta, ambaye alikubali kuniunganisha kwa mfululizo, moja baada ya nyingine na simu za wakuu wa mikoa yote. Wakati huo wakuu wa mikoa walikuwa vilevile ni wabunge, kwa nyadhifa zao hizo. Kwahiyo, kwa pamoja, tuliweza kufanikisha zoezi hilo, na ilipofika siku ya Alhamisi jioni, nikarudi kwa Rais kutoa taarifa hiyo, na kuomba kujua ni mambo gani yatakayozungumziwa katika kikao hicho, ili niweze kuandaa Order Paper (Orodha ya Agenda). Ndipo nilipoambiwa kwamba agenda itakuwa moja tu, ambayo ni "Hotuba ya Rais", na pia, kwamba, kikao cha Bunge sasa kitafanyika siku ya Jumamosi na siyo Ijumaa.

**1.3.2 Kikao cha Bunge, Jumamosi tarehe 25 Aprili 1964**

Hotuba ya Bunge ilikuwa na jambo moja tu, nalo ni kuliomba Bunge kuridhia Mkataba wa Makubaliano ya kuunganisha nchi za Tanganyika na Zanzibar. Tutarejea kwenye maudhui ya hotuba hiyo baadaye kidogo. Katika taratibu za ki-Bunge, kazi ya kuridhia mikataba ya kimataifa kama huu, hufanywa kwa njia ya kupitisha muswada wa sheria wenye madhumuni hayo. Kwa hiyo, serikali ilikuwa imeandaa muswada, ambao jina lake lilikuwa ni :

" A Bill for Act to ratify the Articles of Union between the Republic of Tanganyika and the Peoples' Republic of Zanzibar, to provide for the Government of the United Republic and of Zanzibar, to make provision for the laws of Tanganyika for the purpose of giving effect to the Union and the said Articles, and for matter connected therewith and incidental thereto."

Muswada huo uliwasilishwa bungeni kwa 'Hati ya Dharura' iliyotolewa na kusainiwa na Rais mwenyewe. Kutokana na furaha iliyotawala bungeni kuhusu tukio hili la kuunganisha nchi mbili, muswada huo ulijadiliwa na kupitishwa bungeni ndani ya muda mfupi tu. Wabunge wote waliafiki hoja hiyo. Nilikuwa nimepewa maelekezo kwamba, muswada ukishapitishwa na Bunge, niupeleke kwa Rais mara moja bila kuchelewa, ili Rais aweze kuweka saini yake, na kwahiyo, kuufanya uwe na sheria ya nchi. Nami nilitekeleza maalezo hayo, majira ya saa mbili usiku huo huo.

Mkataba wa makubaliano uliagiza kwamba, Jamhuri ya Muungano itazaliwa "siku inayofuata baada ya kuridhiwa kwa makubaliano hayo." Ndiyo sababu siku rasmi ya kwanza ya uhai wa Muungano huu.

**1.3.3 Kikao cha Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano, tarehe 27 Aprili, 1964**

Rais Nyerere alikuwa ameitisha kikao cha kwanza cha Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano, kifanyike siku ya Jumatatu, tarehe 27 Aprili, 1964. Sheria ya kuridhia makubaliano ya Muungano, ilikuwa imeweka vifungu mbalimbali mahsusi, kwa ajili ya utekelezaji wa makubaliano hayo. Kwa mfano kifungu cha 5 (c) kilielekeza kwamba, wateuliwe Makamu wawili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Uteuzi huo ulifanyika siku hiyo ya tarehe 27 Aprili, 1964, ambapo, Rais Abeid Amani Karume wa Zanzibar, aliteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, na Rashid Mfaume Kawawa aliteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais, aidha kifungu cha 5(d) cha sheria hiyo kilieleza kwamba, wawepo wawakilishi wa Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. Njia pekee ya kuwapata wawakilishi hao wakati huo, ilikuwa ni njia ya uteuzi unaofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano. Rais Nyerere aliteua kundi la kwanza la wawakilishi kutoka Zanzibar siku hiyo ya tarehe 27 Aprili 1964, ambao niliwapangia nafasi ya kuapishwa bungeni siku hiyo hiyo. Baada ya hapo, agenda iliyofuata ilikuwa ni "kubadilishana hati za Muungano," ambapo, aliyekuwa Rais wa Tanganyika Mwalimu Julius Nyerere, alikabidhi nakala ya hati hiyo kwa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Sheikh Abeid Aman Karume. Shughuli hiyo ndiyo ilikamilisha shughuli za Bunge la Kwanza la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Na hili ndilo lilikuwa la dharura Bunge hitimisho la 'wiki ya matukio makubwa,' iliyoanzia tarehe 20 Aprili 1964.

**INAENDELEA JUMATANO IJAYO**

## Rais wa zamani wa Misri azikwa baada kufariki dunia mahakamani

RAIS wa zamani wa Misri, Mohammed Morsi, alizikwa jana, baada ya kuanguka mahakamani juzi na kuaga dunia.

Mashirika ya kutetea haki za binadamu yametaka kufanyika uchunguzi huru, kufahamu sababu halisi ya kifo chake.

Wakili wa rais huyo wa zamani anasema Morsi alizikwa jana asubuhi katika makaburi ya Medinat Nasr Mashariki mwa mji mkuu, familia yake ikiwepo.

Televisheni ya taifa hilo imesema kifo chake kilisababishwa na mshtuko wa moyo.

Morsi, Rais wa kwanza wa kiraia wa Misri, ambaye ni wa kwanza pia kuchaguliwa kwa njia ya kidemokrasia, alianguka katika kizimba chake mahakamani baada ya kujieleza, na aliwahishwa hospitalini ambako ilitangazwa kuwa alikuwa tayari amekata roho.

Tangu alipoangushwa katika mapinduzi ya kijeshi Julai 2013, aliyekuwa waziri wake wa ulinzi Abdel Fattah al-Sisi amechukua hatamu za uongozi wa nchi hiyo, akipambana vikali na maelfu ya wanachama na wafuasi wa kundi la Udugu wa Kiislamu (Muslim brotherhood), huku miongoni mwao wakikabiliwa na hukumu ya kifo.

**SERIKALI YANYOOSHEWA KIDOLE**

Watetezi wa haki za binadamu wanakosoa mazingira ya wafungwa magerezani nchini Misri.

Wanaharakati wa kutetea haki za binadamu nchini Misri wanasema yumkini mazingira mabaya gerezani yamesababisha kifo cha Morsi, hali ambayo wanasema ni ukiukaji wa haki za binadamu.

Mmoja wao, Amr Magdi wa Shirika la Human Rights Watch anasema:

"Tunaamini kwamba mazingira mabovu na ya kutengwa aliyowekwa Morsi yanakidhi vigezo vya utesaji kwa mujibu wa maazimio ya Umoja wa Mataifa (UN) na kanuni za msingi za hali ya wafungwa, ambazo serikali ya Misri ilizipuuza kabisa."

Mwanaharakati huyo anaongeza kuwa anadhani serikali ya al-Sissi imeonyesha dharau ya kupindukia dhidi ya haki za msingi za binadamu.

Mwanaharakati huyo wa haki za binadamu, anasema pia kwa muda mrefu Morsi amekuwa akilalamikia ukosefu wa matibabu yanayofaa kwa ugonjwa wa kisukari aliokuwa nao na kunyimwa ruhusa ya kumuona daktari wake.

Awali, mtoto wa Morsi, Abdullah Mohammed Morsi, aliiambia DW kwamba mara ya mwisho familia iliruhusiwa kumtembelea baba yake Septemba mwaka jana.

**MORSI SHAHIDI**

Rais wa Uturuki Recep Tayyip Erdogan ambaye ni mshirika wa kundi la Udugu wa Kiislamu amemshambulia Rais al-Sisi kwa kifo cha Morsi aliyemuita shahidi, na kuzikosoa nchi za Magharibi kufumbia macho rekodi yake mbaya kuhusu haki za binadamu.

Naye Katibu Mkuu wa Tawi la Kijeshi la Udugu wa Kiislamu, Murad Adeileh, akizungumza kutoka nchini Jordan anasema kifo cha Morsi kimetokana na uhalifu, na akataka ufanyike uchunguzi wa kimataifa.

Iran na kundi la Kipalestina la Hamas pia wametoa salamu zao za rambirambi.

Morsi amekuwa jela kwa miaka mitano iliyopita, na mwaka 2015 alihukumiwa kifo, kwa hatia za ujasusi na kushirikiana na magaidi.

**DW**



Rais wa zamani wa Misri, Mohamed Morsi aliyezikwa jana baada ya kufariki dunia juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Mshauri Rais Marekani awasha moto eneo la Mashariki ya Kati

## • Ni Kushner mkwewe Rais Trump



Rais wa Marekani, Donald Trump (kulia), akiwa na mshauri wake Jared Kushner ambaye pia ni mkwewe. **PICHA: MTANDAO**

**Na Anil Kija**

MSHAURI wa karibu wa Rais Donald Trump wa Marekani na mkwewe, Jared Kushner, ameingia katika anga za kidiplomasia kwa kuzua taharuki kote Mashariki ya Kati na kwingineko duniani.

Ni wakati akianza kutoa viainisho vya mpango wake wa amani Mashariki ya Kati ambao kimsingi hauwalengi Wapalestina ila nchi za jirani, ziisaidia Marekani kuondoa tatizo la Wapalestina na hivyo eneo hilo liwe na amani, sambamba na kupambana na Iran kwa hali zote, ambaye ndiyo mfadhili mkuu wa Hamas, adui tangulizi wa Israel. Ni sera kamilifu, ila si amani.

Kiini cha mpango wa amani aliouandaa kwa zaidi ya miezi sita sasa, na kimsingi amekuwa akiufanyia kazi tangu Rais Trump aingie madarakani Januari 2017 ni udhaifu wa utawala wa chama cha ukombozi wa Palestina (PLO) chini ya Rais Mahmoud Abbas, mwenyekiti wa mamlaka ya Palestina.

Endapo Palestina inapewa hadhi ya nchi kamili yenye madaraka yake ya ndani bila kuingiliwa na vyombo vya ulinzi na usalama vya Israel, Palestina itatekwa na kundi la Hamas linaloshikilia Ukanda wa Gaza; lina mwelekeo tofauti na PLO, ni hasimu jadidi wa Israel.

Fununu za mpango huo zilizoanza kuvuja mwishoni mwa mwezi Mei zilionyesha kuwa kimsingi mshauri huyo wa Rais Trump anafikiria kuwapo kwa eneo la kutoa misaada kwa ujenzi wa miundombinu na xxx makazi ya watu inayounganisha nchi za Ghuba, Saudia, Jordan na Misri, na kwa maana hiyo kutoa nafasi kwa mwendelezo wa mpango huo kugusa Wapalestina.

Wakati mpango huo ukianza kutajwa, ziko dalili kuwa serikali ya Marekani inafikiria kutoa azimio la kufutwa kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Palestina (UNRWA) ambalo limekuwapo tangu 1948, wakati Israeli inajitangazia uhuru.

Fedha zinazochangwa hapo zinamilikiwa na serikali ya Rais Abbas, ambaye anazilipa familia za majihadi wakijitoa mhanga.

Marekani tayari imepunguza kwa asimilia 50 kiasi cba fedha inazotoa kwa UNRWA tangu Rais Abbas asitishe mawasiliano ya kidiplomasia na utawala wa Marekani kutokana na hatua ya Rais Trump kuitambua Yerusalemu kuwa mji mkuu wa Palestina.

PLO na Hamas wanataka kuundwa kwa dola ya Palestina yenye makao makuu Yerusalemu Mashariki, na hawataki kusikia Israel inatambuliwa kuwa mji mkuu wake ni Yerusalemu badala ya Tel Aviv.

Ni mojawapo kati ya maeneo yenye utata kwa hisia za Marekani kuhusu uwezo wa kujitawala wa Palestina, kuwa Rais Abbas na chama chake hawawezi kuihakikishia dunia kuwa ikiundwa dola ya Palestina kwa mipaka ya kabla ya vita vya mwaka 1967 inaweza kuishi kwa amani na Israel.

Marekani bado inaamini itakuwa ni kusogeza tu wapiganaji wa Hamas na silaha zao kutoka Iran kuilipua Israel.

Suala linalobaki ni kama Kushner ana mpango wa amani Mashariki ya Kati au amebuni kitu kama mpango wa maendeleo ya eneo hilo, akitazamia kuwa asasi za kiraia na hata za kisiasa za Wapalestina zinaweza kushiriki katika mpango huo.

Ila ushiriki huo ni kati ya washikadau kadhaa wakubwa wenye sera zinazoshabihiana na Marekani, na siyo mpango ambako Marekani inalenga kuzungumza na Mamlaka ya Palestina ili kuafikiana kuhusu chochote kile.

Marekani inaongea na washirika wake, hasa Saudia na nchi za Ghuba, na Kushner anatazamiwa atoe maelezo marefu zaidi katika mkutano wa kimataifa nchini Bahrain kwa suala hilo mwezi huu.

Baadhi ya wachambuzi wa habari Mashariki ya Kati na kwingineko wakaanza kutoa hoja kuwa Kushner ni mbaguzi, kwani hawezi kutoa hoja kuwa "Wayahudi hawawezi kujitawala' lakini anadiriki kusema 'Wapalestina hawawezi kujitawala.'

Licha ya kuwa wako wasomi lukuki watakaounga mkono hoja hiyo, bado kuna mashiko kitaaluma katika kile alichokisema Kushner kwani uwezo wa kujitawala katika sheria za kimataifa ni pamoja na uwezo wa kuingia mikataba na kuitekeleza.

Utawala wa Abbas hauwezi kuingia mkataba wowote kuhusu kuwepo kwa dola tofauti katika eneo la Palestina, yaani Israel na dola huru ya Palestina, na Hamas au Iran wautii.

Kimsingi hali hiyo inamaanisha kuwa mradi itikadi ya Iran na Hamas inaongozwa na hisia za kijihadi na matazamio kuwa hatimaye watashinda na kuiondoa Israel, ili Wapalestina watumie haki ya kurudi walikotoka kabla ya kufanywa wakimbizi, uundwaji wa dola huru ya Palestina kwa mikataba hasa kupitia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ni ndoto.

Wakati huo huo raia wa Israel wanaendelea kuchota maeneo katika ukingo wa magharibi na sasa serikali ya Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu inatayarisha mpango wa kumega baadhi ya maeneo yenye wakazi wa Israel kuwa yaingizwe katika mfumo wa sheria wa nchi hiyo.

Katika majadiliano ambayo sasa yamechukua hatua kubwa zaidi baada ya kuhojiwa na vituo vya televisheni na magazeti makubwa nchini Marekani kuhusu anachofikiria kwa suala la Palestina, Kushner alisema yako mambo kadhaa ambayo serikali ya Palestina imefanya vizuri, na yako ambayo yanakosekana.

Alisema ili eneo hilo liwe (salama) kwa wawekezaji kuja na kuingiza fedha zao katika viwanda, miundombinu na kuzalisha ajira, "lazima kuwe na mfumo bora wa mahakama, uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kujieleza, uhuru wa kuabudu bila bughudha kwa dini yoyote ile."

Hivyo ni vigumu kuona jinsi utawala wa Palestina unaweza kufikia hayo.

Hata hivyo, mshauri huyo wa Rais Trump alijitahidi kutosema moja kwa moja kuhusu uwezekano wa kuwepo suluhisho la nchi/dola mbili ambalo ni msingi wa madai ya makundi yote ya Wapalestina.

> Baadhi ya wachambuzi wa habari Mashariki ya Kati na kwingineko wakaanza kutoa hoja kuwa Kushner ni mbaguzi, kwani hawezi kutoa hoja kuwa "Wayahudi hawawezi kujitawala' lakini anadiriki kusema 'Wapalestina hawawezi kujitawala.'

Wachambuzi wa habari wanasema amekuwa akikwepa kujibu swali hilo kinagaubaga tangu aanze kupigia debe mpango wake wa amani, ambao anautangaza kuwa ni 'dili la karne,' kama dola huru ya Palestina itapatikana.

Akiulizwa aseme kama kutakuwa na nchi huru ya Palestina yenye makao yake makuu Yerusalemu Mashariki, alisema anaamini kuwa "Wapalestina wanashughulikia zaidi kulipia mikopo ya benki yenye dhamana ya nyumba..."

Mpangilio huu wa fikra ya Ikulu ya Marekani kuhusu suala la Palestina unabadilisha kila kitu kuhusu Mashariki ya Kati kama kinavyojulikana hadi sasa, ambako Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa la Juni 1967 limekuwa ndiyo msingi wa majadiliano.

Sasa inaelekea suala la Wapalestina linaanza kufanana na lile la Wakurdi katika nchi za Syria, Iraq, Iran na Uturuki ambako wana viwango tofauti vya kujisimamia wenyewe ambako nchini Iraq wana uhuru mpana.

Kwingineko ni majimbo yanayokaliwa kijeshi na viongozi wake kuswekwa ndani au kuwa na uhuru mfinyu katika masuala ya uchaguzi.

Wapalestina ni sehemu kubwa ya nchi ya Jordan ambayo ilikuwa inamiliki eneo la Ukingo wa Magharibi kabla ya Juni 1967 wakati nchi za Kiarabu kuzunguka Israel zilipoishambulia ili kuiteketeza na kushindwa.


Kuanzia hapo wamekuwa wakitegemea kubatilisha matokeo ya vita hivyo kupitia azimio la 242 la kuondoa majeshi ya Israel na kuundwa kwa taifa la Palestina katika mipaka ya 1967.

Tatizo ni kuwa dai hilo haliwezi kutekelezwa bila Marekani kuishurutisha Israel kukubali azimio hilo, na hilo ni ndoto ambayo sasa Marekani inailipua kweupe, kulenga uwekezaji chini ya Israel, na si dola huru.

UCHAMBUZI

# Waandishi Zanzibar waazimia kukemea wenye kauli chochezi

- Ni kuelekea Uchaguzi Mkuu 2020
- Ilikuwa kwenye maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KIMSINGI, vyombo vya habari vimekuwa ndiyo macho na masikio ya wananchi kufikisha ujumbe unaohusu mambo mbalimbali yanayotokea ndani na nje ya nchi.

Ni dhahiri vyombo vya habari nchini vimekuwa kiungo muhimu cha kuisaidia serikali kutoa taarifa zake mbalimbali, lakini pia kusaidia suala la ajira kwa raia wake katika dhima nzima ya kupunguza tatizo hilo nchini.

Hivi karibuni dunia iliadhimisha Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari mnamo Mei 3 na Tanzania nayo ikiwa sehemu ya dunia, ilishiriki vilevile.

Zanzibar kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haikuwa nyuma katika kuadhimisha siku hiyo, ikiwa na kauli mbiu "Wajibu wa vyombo vya habari katika uchaguzi na demokrasia."

Pamoja na Zanzibar kuadhimisha siku hiyo, lakini waandishi wa habari wanakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwamo za baadhi ya waajiri kutofuata sheria katika suala la kuwalipa stahiki zao.

Faki Mjaka ni mwandishi wa habari na katibu wa Chama cha Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC), anazungumzia baadhi ya changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kipato kisichoendana na kasi ya maisha.

Anabainisha kwamba kuna haja kwa msingi huo kuwa na chama cha kutetea maslahi yao na ikiwezekana hata katika mhimili wa Mahakama.

"Sisi kama ZPC hatuwezi kufika mahakamani kwani wajibu wetu ni kuwaelimisha, kuwapatia mafunzo, kusimamia na kufuata misingi na maadili ya uandishi wa habari," anasema na kuongeza:

"Lakini kama kutakuwa na chama hicho kitakuwa kinatetea maslahi ya waandishi, kuhakikisha wanaishi vizuri na kuibua mambo ya kuisaidia jamii na maendeleo kwa ujumla," anasema.

**TAMWA**

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) upande wa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, anasema umefika wakati kwa umoja wa waandishi wa habari kukaa pamoja, kujadili na kujiwekea viwango na vigezo vya viwango vya malipo wanachostahili kulipwa.

Anasema licha ya kazi kubwa zinazofanywa na waandishi wa habari kwa manufaa ya jamii, lakini wapo baadhi yao wasiokuwa na mikataba ya kazi wala mshahara.

"Na ndiyo maana ipo haja ya kuwapo kwa jumuiya itakayotetea maslahi ya waandishi wa habari ili kipato watakacholipwa kiwawezeshe kuendesha maisha yao," anasema.

Aidha, Dk. Mzuri anaikubali kazi nzuri inayofanywa na kada hii kwa kuandika habari mbalimbali zenye manufaa makubwa kwa umma zikiwamo za udhalilishaji wa kijinsia na hivyo kuiwezesha serikali kutimiza wajibu wake.

"Kuandika habari zinazofichua maovu na ufisadi na vitendo vya ukatili wa kijinsia, ndiyo kazi yetu na kamwe tusichoke kutekeleza wajibu huo kwa ufanisi na uadilifu mkubwa," anasema.

MAELEZO

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) Zanzibar, Juma Mohamed, anasema wameshaanza kushughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili waandishi wa habari zikiwamo za mishahara na za kuingiliwa katika majukumu yao.

Anabainisha kwamba katika hatua za awali tayari wamewasiliana na wamiliki wa vyombo vya habari kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi tatizo la malipo.

**WIZARA YA HABARI**

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Saleh Yussuf Mnemo, anasema inahitajika sheria ya vyombo vya habari ambayo itakuwa mwongozo kwa ajili ya utendaji wa kazi za waandishi wa habari Zanzibar.

Mnemo anafafanua kwamba sheria inayotumika sasa ya usajili wa magazeti na vijarida Namba 5 ya mwaka 1988, imepitwa na wakati na haikidhi mahitaji na mabadiliko makubwa ya tasnia ya uandishi wa habari.

Anasema amekuwa akihamasisha na kuwataka viongozi wa wizara hiyo kwa nyakati tofauti kuhakikisha wanawahusisha watu wengi zaidi katika mchakato huo ili kupata maoni yatakayoboresha sheria mpya.

"Nimewaagiza viongozi wa wizara ya habari kuhakikisha mchakato wa matayarisho ya sheria ya vyombo vya habari unawashirikisha watu wengi kwa wakati mmoja... tunataka wadau wote wapate nafasi ya kutoa maoni yao," anasema.

Hata hivyo, anasisitiza kwamba uhuru wa vyombo vya habari umeimarika kwa kiwango kikubwa, licha ya kutokuwapo kwa sheria ya vyombo vya habari Zanzibar.

"Kwa hivi sasa Zanzibar, waandishi wa habari wamekuwa wakifanya kazi zao bila ya kusumbuliwa na tishio la kufungiwa vyombo vyao au wenyewe kuzuiwa kufanya kazi," anasema.

Anabainisha kwamba hatua hiyo imesaidia kwa kiwango kikubwa kujenga ushirikiano kati ya vyombo vya habari na serikali katika kufanya kazi.

**WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma Nhunga ambaye alikuwa mgeni rasmi katika Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, anasema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) haina matatizo na waandishi wa habari kwani wako huru kufanya kazi zao kwa kuzingatia maadili.

"SMZ inathamini kazi za vyombo vya habari na wapo huru kukosoa pamoja na kuelekeza nini kifanyike katika masuala mbalimbali, kwani huo ndio wajibu wao," anasema.

Nhunga anawataka waandishi wa habari kufichua rushwa na uhujumu uchumi, kwa sababu ni miongoni mwa mambo ambayo yamepewa kipaumbele na SMZ.

Naibu huo anasema bado waandishi hawajafanya kazi kubwa katika eneo la rushwa kwa kutoa taarifa na kuwafichua watu wanaokula rushwa.

"Serikali imetunga sheria ya kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi... sasa tunataka kutokomeza rushwa na watu ambao wanaweza kutusaidia ni waandishi wa habari," anasema.

Anafafanua kuwa Zanzibar ipo katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya ambazo ni tishio kwa maisha ya wananchi, hasa vijana.

"Tunawaomba waandishi wa habari wajikite katika eneo la mapambano dhidi ya dawa za kulevya ambazo athari zake kwa jamii ni kubwa," anasema.

Anabainisha kwamba watazifanyia kazi changamoto za waandishi zilizoelezwa katika kongamano hilo, ikiwamo ya kutolipwa mishahara na waajiri wao hasa vyombo binafsi.

**MAAZIMIO**

Akisoma maazimio waliyofikia mbele ya waandishi wa habari, Katibu wa Jumuiya ya Waandishi wa Habari za Maendeleo (WAHAMAZA), Salma Said, aliwaasa waandishi wa habari kutoa kipaumbele kwenye ujumbe wa siku hiyo katika kazi zao.

Anasema mwaka 2020 kutakuwa na harakati za uchaguzi mkuu kwa hiyo waandishi wanatakiwa kuibeba ajenda ya kauli mbiu 'Wajibu wa vyombo vya habari katika uchaguzi mkuu mwaka 2020 na demokrasia'.

Anabainisha kwamba wataibeba ajenda hiyo kwa kukemea vikali lugha za uchochezi zinazotolewa katika majukwaa na wanasiasa kwenye safari ya kuelekea uchaguzi mkuu.

"Tunapoelekea mwaka 2020, tuwakemee na kuwafichua viongozi wanaotoa kauli za uchochezi zenye lengo la kugombanisha wananchi kwa maslahi yao binafsi," anasema.

Pamoja na mengine katika maazimio yao walikubaliana kufanya kazi na serikali kufichua maovu ya rushwa na uhujumu uchumi pamoja na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia, vikiwamo vya kudhalilisha wanawake na watoto.

"Tuna mengi tuliyoyabaini, mojawapo ni eneo la rushwa bado hatujalifanyia kazi...lakini pia tunaomba ushirikiano na mamlaka za kupambana na rushwa, zitushirikishe katika matukio pamoja na kutupatia mafunzo na mbinu mbalimbali," anasema.

# Vita yanukia eneo la Ghuba baada ya kushambuliwa meli kubwa za mafuta



Moja ya meli ambayo Marekani inadai ililipuliwa na Iran. **PICHA: MTANDAO**

**Na Anil Kija**

UWEZEKANO wa kutokea kwa vita kati ya Marekani na Iran kulipanda kwa kiasi cha kutisha hivi karibuni baada ya meli kubwa mbili kushambuliwa na kile ambacho Jeshi la Marekani linasema ni mabomu ya kutegwa.

Ilitoa video kutoka ndege ya kijeshi angani iliyowahi eneo hilo baada ya mlipuko katika ubavu wa meli mojawapo, ikionyesha makomandoo wanaotajwa kama wa vikosi maalum (vya kimapinduzi) vya Iran wakiondoa bomu ambalo halikulipuka.

Nchi nyingine zilikuwa zinajitahidi kutokuinyooshea kidole haraka mno Iran, ikiwa ni pamoja na Japan, inayomiliki meli hizo (super tankers), ikidai ni kitu kilichorushwa, sio kutegwa.

Wakati mabomu hayo yanalipuka Waziri Mkuu wa Japan, Shinzo Abe, alikuwa ziarani nchini Iran, akijaribu kupeleka ujumbe maalum kutoka kwa Rais Donald Trump wa Marekani, kwa kiongozi mkuu wa Iran Ayatollah Ali Khamenei, ambaye alifanya mazungumzo na kiongozi huyo wa Japan, lakini hakupokea ujumbe wowote.

Ayatollah Khamenei alisema Rais Trump hana jema analowaza moyoni mwake kuhusu nchi hiyo, hata kupeleka ujumbe kwa wakuu wa Iran.

Katika lugha ya kidiplomasia ni kama kusema tuko vitani, na kabla ya hapo Rais Hassan Rouhani alikuwa ameuambia mkutano wa wakuu wa eneo la Asia ya Kati kuwa vikwazo vya Marekani kwa Iran havivumiliki.

Baadhi ya wachunguzi wa habari wakasema kuwa shambulio hilo ni kama lilikuwa linangojewa, na labda cha kushangaza ni kuwa limechukua miezi kadhaa kutokea.

Isitoshe, vikosi maalum vya Jeshi la Iran (Revolutionary Guards) vilitajwa miezi michache iliyopita na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani kuwa ni 'taasisi ya kigaidi.'

Vikosi hivyo vinafanya kazi nyingi za kiuchumi nchini Iran, kama ambavyo nchini Marekani kazi yote ya upelelezi, utafiti na kufanyika safari za anga za juu ipo chini ya Wizara ya Ulinzi, na mifano si haba.

Ina maana kulikuwa na msukumo au changamoto kutoka kwa wakuu wa vikosi hivyo kuonyesha kuwa taasisi hiyo ipo, hivyo kama Iran itarushiwa mabomu, biashara eneo hilo itakuwa hatarini.

Waziri Mkuu Abe alielekea kuelewa hoja hiyo, akapunguza makali ya video hiyo ya kijeshi ya Marekani na mchango wake tarajiwa kuandaa hatua za Japan kuhusu hilo.

Japan, kama ilivyo kwa nchi nyingine washirika wa Marekani katika umoja wa kujihami wa NATO inachelea kufuata tu 'kibubusa' hatua zote zinazochukuliwa na Marekani dhidi ya maadui zake, hivyo wanadiplomasia wa Marekani watapata wakati mgumu kuungwa mkono kuchukua hatua kuhusu ulipuaji huo.

Wanadiplomasia Ulaya na Mashariki ya Mbali wanataka suala la msingi litangulizwe, ambalo ni Marekani kujiondoa katika mkataba kudhibiti sekta ya nishati ya nyuklia nchini Iran ili isitengeneze mabomu kama Korea ya Kaskazini, na kila mahali wanakiri kuwa Iran imefuata matakwa ya mkataba huo.

> Waziri Mkuu Abe alielekea kuelewa hoja hiyo, akapunguza makali ya video hiyo ya kijeshi ya Marekani na mchango wake tarajiwa kuandaa hatua za Japan kuhusu hilo.

Marekani haisikii hoja hiyo 'kwa sikio hilo,' ikidai hata wakati wa Rais Obama kuwa na mkataba huo una udhaifu mwingi, hivyo iachane nao. Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu alitumia hotuba yake katika jukwaa la Umoja wa Mataifa na katika ziara zake za hapa na pale nchini Marekani kuonyesha vielelezo vya kipelelezi vya Israel kuhusu kinachotokea katika sekta ya nyuklia nchini Iran.

Inasisitiza, wao wanadai kuwa inadhihirisha kuwa kile Iran inachokionyesha kwa wakaguzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) ni kiini macho, kwani kuna miundombinu muhimu ambayo ni kama haiko katika ramani za shirika hilo na hivyo haikaguliwi.

Ni mjadala mgumu wa kitaaluma ila barani Ulaya na kote Mashariki ya Kati na ya Mbali watasema ni upuuzi wa kutunga, ulete vita.

Ndiyo maana ni vigumu kusema ni mkondo upi wa kidiplomasia ulifaidika na mashambulizi hayo na upi uling'ong'wa.

Iran imethubutu kuiangalia Marekani usoni bila kupepesa kope za macho, lakini kwa msingi kuwa iwe ni onyo tu la kidiplomasia kuhusu hatua za Marekani dhidi ya Iran, na siyo kama mwelekeo rasmi wa nchi hiyo kuhusu biashara ya mafuta katika eneo hilo, suala ambalo ni nyeti kwa watawala wa Iran, kwani Marekani imezuia nchi zote zinazotaka kufanya biashara na taifa hilo lenye nguvu kubwa kiuchumi duniani kutonunua mafuta kutoka Iran.

Kuna misamaha ya muda mfupi iliyotolewa mwaka jana wakati vikwazo vinarudishwa dhidi ya Iran, na muda wake wa miezi sita kimsingi inaelekea ulishamalizika, ila baadhi kama Japan wananunua bado.

Kuna kanuni ya fizikia (maumbile) kuwa kitu chochote chenye uhai au mwendo ni lazima kiendelee na mwendo wake kwa mustakabali au mapana yanayoeleweka, kwani mwendo huo ukisimama kitu hicho kinasambaratika.

Ukiangalia jinsi Marekani na Iran wanavyopimana nguvu katika eneo hilo, si vigumu kuona kuwa Iran imeshika makali na Marekani imeshika mpini, hivyo inaweza kupuuza tukio hilo ikaendelea kuibana Iran na washirika wake kwa nguvu zaidi, ingawa baadhi kule Tehran na kwingineko watasema hakuna nguvu iliyobaki ambayo Marekani wanaweza kutumia.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wawekezaji kutoka nje ambao kimsingi wanahitaji kuwa na uhakika kuwa hapatakuwa na vita kati ya Marekani na Iran, hata kusiwepo na mkataba wa nyuklia au kibali cha kufanya biashara, kama Russia na China ambazo tayari zina vikwazo tofauti dhidi yao, hata wao wataogopa kutia saini mikataba mipya au kutekeleza hiyo iliyopo mradi kuna wingu la vita bado limetanda.

Vikosi vikishambulia tena itakuwa 'jehanam.'

Mtafaruku huu mpya kati ya Marekani na Iran ulizuka wiki hiyo hiyo ambako Rais wa zamani wa Marekani, Bill Clinton alikaribishwa kwa heshima isiyo kawaida kule Pristine nchini Kosovo ambayo mwaka 1999 ilikuwa inaangamizwa na majeshi ya kifashisti ya Serbia yakijiita ni ya Kikristo.

Rais Clinton alimtuma mjumbe maalum, Rais mstaafu Jimmy Carter kwa uongozi wa Serbia na washirika wao wa Serbia Herzegovina, wakampuuza.

Kilichofuata ni 'cruise missiles' zisizohesabika kurushwa Belgrade, mji mkuu wa Serbia, kuharibu miundombinu, kupunguza morali ya kuiunga mkono serikali iliyoko madarakani.

Iran haina migawanyiko ya kina kama ilivyokuwa eneo la Balkans, ila bado kukwamishwa katika 'si vita, si amani' kutaidhuru vilevile.

Labda ndicho alichokuwa akimaanisha Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo.

Akiongea kabla ya ziara ya Abe ya Tehran, alisema Marekani haijaweka mbele lengo la kubadili utawala wa Iran. Inachotaka ni Iran kuacha kuwasha moto eneo la Ghuba na ukanda wa Gaza dhidi ya Israel. Inaelekea alimaanisha kuwa wasipofuata mstari, basi watajiangamiza wenyewe.

Si ajabu pia Shinzo Abe angekuwa na ujumbe kwa Ayatollah Khamenei wa kuainisha tofauti kati ya kuendelea kupimana nguvu na Marekani na kuzidi kuharibu uchumi wa Iran, au kuondoa sera hizo za kimapambano zinazotawaliwa na hisia kali dhidi ya Marekani, sera inayofuatwa Iran tangu mapinduzi ya Kiislam mapema mwaka 1979.

Ni sera ambayo Marekani inaieneza kote Mashariki ya Kati kuwa makundi ya kipambanaji au ya 'kijihadi' yaache sera hizo na kuingia katika matazamo wa kukuza uchumi, kuacha harakati za kubadili mifumo ya utawala iliyopo sasa.

Marekani ikishirikiana na nchi za Ghuba ijaze fedha kwa ajili ya miundombinu, walipwe wananchi wa maeneo hayo (hasa Palestina, Iraq, Yemen, Syria na kwingineko) waanze biashara nyingine, si vita. Endapo utawala wa Tehran hautaelewa, baadaye waandamanaji wataishuhudia.



HABARI MBEYA

# Ma-RC Nyanda za Juu Kusini waita wawekezaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MIKOA ya Nyanda za Juu Kusini inadaiwa kuwa na fursa nyingi na kubwa ambazo hazijatumika ipasavyo kutokana na kutowekezwa na Watanzania wala wawekezaji kutoka nje ya nchi.

Baadhi ya wakuu wa mikoa ya Nyanda zas Juu Kusini waliyasema hayo jana kwenye kongamano la kuhamasisha wawekezaji katika sekta ya kilimo cha mboga na matunda liliandaliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Jumaa Homela, alisema katika mkoa wake kuna fursa kubwa ya kilimo cha matunda, lakini hadi sasa hakuna mwekezaji mkubwa aliyewekeza katika eneo hilo. Alisema kuanzia sasa serikali itaanza kuhamasisha wananchi kuwekeza kwenye kilimo cha matunda na mboga kwa kuwa kuna mazingira mazuri ya wakulima kunufaika na fursa hiyo.

Alisema Mkoa wa Katavi unazo njia zote za usafiri ambazo zinaweza kutumika kusafirisha matunda na bidhaa nyingine za wakulima kama wataamua kuwekeza ipasavyo.

"Kwenye mkoa wangu tuna uwanja wa ndege ambao ni wa pili kwa ukubwa katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ukitanguliwa na uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe, tuna reli inayofika Mpanda ikipitia Kaliua, lakini pia barabara zinajengwa za kutosha na njia zote hizi zinafanya fursa hii ya kilimo cha matunda na mboga iwe yenye manufaa kwa watu watakaoamua kuwekeza," alisema Homela.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema mkoa wake una hali nzuri ya hewa inayoruhusu kilimo cha mboga na matunda ya aina mbalimbali kustawi vizuri.

Alisema mkoa wake umeanza kwa kiwango kidogo kuzalisha maparachichi, lakini uwekezaji huo haujakua kwa kiwango cha kuridhisha.

Chalamila aliwataka wananchi na wawekezaji kutoka maeneo mengine ya nchi na nje ya nchi kufika mkoani Mbeya kuwekeza kwenye eneo hilo kwa vile kuna mazingira mazuri.

"Tunao Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe ndani ya Mkoa wa Mbeya, tunayo reli ya Tazara na pia barabara zetu zinapitika mwaka mzima kuelekea katika maeneo yote ya nchi, hivyo kilimo cha matunda na mboga kinawezekana na mazao yake hayawezi kukosa soko hata kidogo," alisema Chalamila.

Aliongeza Mkoa wa Mbeya pia una bandari mbili za kisasa katika mwambao wa Ziwa Nyasa ambazo pia zinaweza kutumika kusafirisha bidhaa kuelekea maeneo mengine ya nchi na hata nchi jirani za Malawi na Msumbiji ambako soko la matunda na mboga linaweza kupatikana kwa kiwango kikubwa.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mdeme, aliiomba TIC kushirikiana na ofisi yake kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kilimo cha maparachichi.

Alisema mkoa wake umebainika kuwa miongoni mwa maeneo ambayo zao hilo linastawi vizuri, lakini hawajapata wawekezaji wa kueleweka kuwezesha uzalishaji mkubwa.

## Changamoto wanawake wajasiriamali zabainishwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAWAKE wengi wanakosa fursa mbalimbali ikiwamo ya mikopo na elimu ya ujasiriamali kutokana na kufanya shughuli zao bila kuwa na chama kinachowatambua.

Vilevile imeelezwa ni asilimia tano pekee ya wanawake nchini wanaofanya shughuli kwenye sekta isiyo rasmi ndio wanaoweka akiba ya fedha benki na asilimia 95 wanahifadhi fedha zao kwenye mifumo isiyo rasmi.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini, Samora Julius kutoka Shirika lisilokuwa la kiserikali la EFG, wakati wa ziara ya mafunzo ya kutekeleza mikakati na shughuli za programu ya Sauti ya Mwanamke Sokoni yenye lengo la kuwahamasisha wanawake wafanyabiashara kujiunga na umoja wa wanawake sokoni.

Julius alisema hali hiyo imekuwa ni kikwazo cha mwanamke kufikia malengo yake kiuchumi, na kwamba katika kufikia uchumi wa kati utokanao na viwanda ifikapo mwaka 2025, shirika hilo limedhamiria kumkomboa mwanamke kifkra ili aweze kunufaika na kile anachokifanya na awe chachu ya kufikia lengo hilo.

"Ukiwa peke yako hauwezi kufanya kitu chochote, lakini kupitia umoja mkaunganisha nguvu moja mnaweza mkafanya mambo makubwa...mfano halmashauri wanatoa mikopo kwenye vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, hivyo fursa hiyo mnaweza kuipata ikiwa mtakuwa na umoja," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya EFG, Penina Leveta, alisema kupitia mradi huo wamewahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi kwenye masoko na kuwa na ajenda inayohusu changamoto zao.



Meneja wa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Rodney Alananga (kushoto), akitoa maelezo ya kazi wanazozifanya kwa Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (kulia), wakati wa kongamano la kuhamasisha kilimo cha mboga na matunda liliandaliwa na Kituo cha Uwekezaji (TIC) na wadau wengine jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**.

# Kiingereza chadaiwa kukwaza taarifa za matokeo ya utafiti

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UANDAAJI na uwasilishaji wa taarifa za matokeo ya utafiti wa kilimo kwa lugha ya Kiingereza umedaiwa kuwa kikwazo cha teknolojia mpya na za kisasa zinazogundulika kutowafikia wakulima wengi nchini.

Hali hiyo inatokana na wakulima hao kushindwa kuelewa lugha hiyo. Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wafanyakazi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo Uyole cha jijini Mbeya.

Chalamila alisema kutokana na wakulima wengi hasa wadogo kushindwa kuelewa lugha ya Kiingereza wamekuwa wakishindwa kutumia taarifa za utafiti hizo badala yake wanaendelea kulima kwa mazoea.

"Imekuwapo tabia ya watafiti kufanya utafiti wao na wanapomaliza wanaandaa taarifa za matokeo kwa lugha ya Kiingereza, hali hii imekuwa ni kikwazo kikubwa kwa wakulima wadogo nchini kutumia utafiti huo kwenye kilimo, badala yake wanaendelea kulima kwa mazoea," alisema Chalamila.

Aliwataka watafiti hao kuanza kuandaa taarifa za matokeo ya utafiti huo kwa lugha ya Kiswahili ili wakulima wengi wamapate maarifa, teknolojia na mbinu za kilimo cha kisasa kwa lengo la kuongeza tija kwenye kilimo.

Alisema kuwa kinyume chake taarifa hizo zinawanufaisha watu wa mataifa mengine na sio Watanzania.

"Natambua kuwa wakati mwingine mnafadhiliwa na mataifa ya nje kufanya utafiti mbalimbali wa kilimo na mnaandaa taarifa zenu za matokeo kwa lugha ya Kiingereza ili kuwaridhisha wafadhili wenu, lakini pia mnatakiwa kujiuliza kama kwa kufanya hivyo mnalisaidiaje taifa lenu," alisema Chalamila.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema kuwa serikali imeanzisha taasisi hiyo na kuipatia majukumu ya kufanya utafiti na kusimamia ubora wa utafiti wa kilimo ili kuhakikisha unaleta mabadiliko makubwa kwenye sekta ya kilimo nchini.

Alisema taasisi hiyo imeanza kutimiza majukumu hayo kwa kufanya utafiti mbalimbali wa upatikanaji wa mbegu bora, kujua afya ya udongo na aina za mbolea zinazopaswa kutumika katika maeneo mbalimbali nchini.

Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Mbeya, anayeshughulikia Uchumi na Uzalishaji, Said Madito, alikitaka kituo hicho kutatua changamoto ya afya ya udongo ambayo inawakabili wakulima katika maeneo mengi ya Mkoa wa Mbeya.





# Wabunge wapewa mtihani usimamizi bajeti h/shauri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WASHIRIKI wa mjadala juu ya changamoto za ajira na upatikanaji wa kazi zenye staha nchini, wamewataka wabunge kuzisimamia halmashauri kutumia kwa ufanisi bajeti ili kuleta mabadiliko kwenye shughuli za ujasiriamali.

Mjadala huo wa siku mbili uliandaliwa na shirika linalojihusisha na masuala ya vijana (YPC)

Hayo yalielezwa na Meneja mradi wa Shirika la YPC, Jane Mulungi, alipokuwa akiwasilisha mapendekezo ya washiriki kwa wabunge wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mulungi alisema kupitia mjadala huo juu ya changamoto ya ajira na upatikanaji wa kazi zenye staha chini ya ufadhili wa Action Aid, walijadiliana kwa pamoja na kutoka na mapendekezo hayo ambayo waliyawasilisha kwa wabunge.

Alisema moja ya mapendekezo hayo ni wabunge kuzisimamia halmashauri, ili kutumia bajeti zao kwa ufanisi ili kuleta mabadiliko katika shughuli za ujasiriamali kama usindikaji, ufugaji, kilimo na usafirishaji.

Aidha, waliwataka wabunge kuimarisha uhusiano wao na wajasiriamali ili kuleta tija katika kazi zenye staha.

Pia waliwataka wabunge hao watunge sheria ambayo itakuwa ni lazima viwanda waajiri kushirikiana na taasisi za elimu, vyuo kuwawezesha vijana kupata uzoefu.

"Warekebishe sheria ya ajira na mahusinao kazini ili kutambua mchango wa sekta rasmi pamoja na kulinda maslahi ya watumishi wa sekta isiyo rasmi," alisema Mulungi.

Aidha, wadau hao waliwataka wabunge kutumia fedha za mfuko wa jimbo katika kuhakikisha wajasiriamali wadogo kama wasindikaji wa vyakula na bodaboda wanapata mahali pa kufanya kazi.

"Wabunge wahimize utoaji wa elimu kwa wadau husika juu ya upatikanaji wa kazi zenye staha na watengeneze mazingira salama yatakayo wasaidia wajasiriamali wadogo mfano katika shughuli za usindikaji wa vyakula na usafirishaji hususani bodaboda," alisema.

Waliitaka serikali itengeneze sera ambayo itawafanya vijana kuanzia elimu ya sekondari kupata elimu yenye nadharia na mazoezi kwa vitendo kwa uwiano sahihi.

"Wizara ya Viwanda na Biashara itengeneza programu za uanagenzi na mafunzo kwa wafanyakazi tarajiwa ili kuwajengea uwezo vijana kupata uzoefu kwa kuweza kuajirika na kupata kazi zenye staha ndani na nje ya nchi," alisema.

Wabunge walisema kuwa vijana wa kitanzania wanatakiwa kuchangamkia fursa zilizopo na kuacha kulalamika vijiweni.

Magreth Sitta, Mbunge wa Urambo, alisema kuwa vijana wa Kitanzania wamekuwa wazito katika kuchangamkia fursa ukilinganisha na wa nchi nyingine katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Aliishauri serikali kuboresha vyuo vya ufundi ili kuwawezesha vijana kujiajiri.



Wakazi wa Jiji la Dodoma wakiangalia mabehewa mawili yaliyodondoka baada ya kugongwa na lori lenye namba za usajili T 860 APW lililotokea makutano ya Barabara ya Hazina, jijini Dodoma juzi usiku majira ya saa tano usiku. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**.

# Ndugai atoa mwisho wa kilimo jembe

**Na Ibrahim Joseph**, KONGWA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema serikali imedhamiria kufuta kilimo cha jembe la mkono nchini kutokana na kuagiza matrekta kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC).

Kauli hiyo aliitoa alipokuwa akizungumza baada ya kukabidhiwa trekta na uongozi wa NDC neo la Mbande wilayani Kongwa.

Ndugai alisema serikali imekusudia kukifuta kilimo cha jembe la mkono kutokana na kuhuisha upya NDC ambalo limepewa jukumu la kuagiza zana hizo za kilimo.

"Azimio la serikali ni kufuta kilimo cha jembe la mkono, hivyo Watanzania waunge mkono shirika hili ili kunufaika katika kilimo," alisema.

Aidha, alisema mkulima akinunua trekta ananufaika kwa kutumia kwa kilimo pamoja na kulitumia kama kiwanda baada ya msimu wa kilimo.

Alizitaja faida za kulitumia trekta kama kiwanda kuwa ni kusaga nafaka, kupukuchua mazao, kubebea majani pamoja na mazao kutoka shambani na kusafirisha.

Aliwataka wananchi watakaokopeshwa matrekta na NDC kuwa waaminifu kwa kuhakikisha wanalipa kwa wakati ili na wengine waweze kunufaika na mikopo hiyo.

"Hili trekta ni langu mwenyewe, sio la jimbo ...nimekopa kwa masharti ya kulipa kwa muda, nitajitahidi kulitumia kwa faida ili niweze kulipa kwa wakati," alisema.

Mkurungenzi Mtendaji wa NDC, Prof. Damian Gabagambi, alisema wameshasambaza matrekta 442 nchi nzima.

Prof. Gabagambi alisema kati hayo, mkoa wa Dodoma wamesambaza matrekta 28, na kwa Wilaya ya Kongwa ni matrekta 11 hadi jana.

Alibainisha kuwa katika Mkoa wa Manyara unaongoza kwa kununua matrekta mengi kwani wamesambaza matrekta 136 na bado wateja wanayahitaji.

Aidha, alisema bei za matrekta hayo zinatofautiana kutokana na ukubwa wake, ambapo alizitaja baadhi ya bei hizo kwa trekta moja ni kuanzia Sh. milioni 46 hadi 56.

# Maonyesho kufundisha wananchi ufugaji kisasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imeandaa gwaride la maonyesho ya mifugo litakalofanyika jiji hapa, ili kuwasaidia wananchi kujifunza njia bora za ufugaji wa kisasa na wenye tija.

Maonyesho hayo yatakayofanyika kitaifa jijini Dodoma, yanalenga kuongeza hamasa katika ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa.

Akizungumzia maonyesho hayo Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema Tanzania ni kati ya nchi zenye ng'ombe wengi, hivyo kuna haja ya kuboresha mifugo.

Alisema Tanzania ni ya pili kwa kuwa na mifugo mingi barani Afrika, hivyo ipo haja ya kuhakikisha kuwa tasnia ya mifugo inaendelezwa.

"Hakuna sababu ya kuendelea kujisifu kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo wakati wanachi hawanufaiki nayo, lazima tufanye kitu ambacho kitawasaidia kuboresha maisha ya wafugaji wetu," alisema.

Pro. Ole Gabriel alisema gwaride la mifugo ni la kwanza kufanya nchini ambalo limelenga kuonyesha namna sayansi inavyotumika katika kutengeneza mbegu bora za mifugo.

"Katika kutumia sayansi kutengeneza mbegu bora za mifugo ndiko kutatusaidia katika kuwa na ng'ombe bora, maziwa bora na hata ngozi bora," alisema.

Aidha, aliwataka Watanzania kutambua kuwa afya ya mifugo ni jambo la muhimu ili kuwa na ufugaji wenye tija.

Alisema katika maonyesho hayo pia wananchi watapa fursa ya mafunzo mbalimbali ikiwamo matumizi ya dawa za mifugo na malisho.

"Suala la malisho ni jambo la msingi sana hata ilani ya chama chetu cha CCM, inasisitiza katika kuandaa maeneo ya malisho kwani inatusaidia katika kuondoa migogoro ya ardhi, lakini pia migongano na watumiaji wengine wa ardhi," alisema.

Hata hivyo katibu huyo alisema kuwa malengo ya maonyesho hayo ni kutia hamasa ya kuwafanya Watanzania kuacha kujivunia kuwa na wingi wa mifugo bali wawe na mifugo bora na yenye uzito mkubwa.



# Vyanzo vya maji hatarini kutoweka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba, Maji, Nishati, Salama Aboud Talib, amesema vyanzo vya majisafi na salama vilivyopo Zanzibar, viko katika hatari ya kutoweka kutokana na tabia ya wananchi kuvamia na kujenga nyumba za kudumu.

Alisema hayo juzi wakati akifanya majumuisho na kujibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka wa fedha wa 2019/20.

Talib alisema kitendo cha uvamizi na kujenga katika maeneo ya vyanzo vya maji ni hatari na kinatishia kukauka kwa vyanzo hivyo.

Alivitaja baadhi ya vyanzo vya maji ambavyo viko katika hatari ya kutoweka ni pamoja na Mwanyanya ambacho ni maarufu kwa uzalishaji mkubwa wa maji yanayotumika katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

"Hiki chanzo cha majisafi na salama kilichoko Mwanyanya kipo tangu enzi za ukoloni kinaongoza kwa uzalishaji mkubwa wa majisafi na salama, lakini kimeanza kupungua kutokana na kasi ya ujenzi wa nyumba," alisema.

Alivitaja baadhi ya vyanzo vya majisafi na salama ambavyo vimetoweka kutokana na tabia ya wananchi kujenga nyumba za kudumu karibu na vyanzo hivyo kuwa ni Bububu, Kiyanga na Masingini, Unguja.

Hata hivyo alisema juhudi zinazochukuliwa kwa sasa na Mamlaka ya Majisafi na Salama (ZAWA) kwa kujenga uzio katika vyanzo hivyo ili kuzuia uvamizi na matukio ya aina hiyo.

Alisema ujenzi wa uzio wa chemchemu ya Mwanyanya uko katika hatua nzuri na unasubiri mkandarasi kwa ajili ya kazi hiyo.

"Ujenzi wa ukuta wa chanzo cha maji cha Mwanyanya upo katika hatua nzuri tunasubiri mkandarasi kwa sasa, lakini baadhi ya visima kama vile Matuleni na Ngwachani tumefanikiwa kujenga uzio," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walipitisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara ambayo ni Sh. bilioni 156.582 kwa kazi za kawaida na maendeleo.

Waziri huyo alisema mafanikio ya wizara yako katika utekelezaji wa Sera ya Maji ya mwaka 2004, Sheria ya Maji ya mwaka 2006, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Awamu ya Tatu (MKUZA III), Dira ya Maendeleo ya 2020 na Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDG).



Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni (kushoto), Nassor Salim Ali, akizungumza na Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana ya CCM (UVCCM), Tabia Mwita, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mil. 400/- zatumika kwa kupima viwanja

**Na Rahma Suleiman, Z**ANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, amesema Sh. milioni 400 zimetumika kwa ajili ya kupima maeneo ya ujenzi wa miradi ya viwanda vidogo na vya kati Unguja na Pemba.

Alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Wawi, Hamad Abdalla Rashid, aliyetaka kujua maeneo mangapi yamepimwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya viwanda katika visiwa hivyo.

Balozi Amina aliyataja maeneo yaliyopimwa tayari kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa viwanda ni pamoja na Nungwi mkoa wa Kaskazini Unguja, Nyamanzi, Dunga Wilaya ya Kati na Chamanangwe kisiwani Pemba.

Alisema hivi sasa eneo la Chamanangwe liko katika mpango wa matumizi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kati.

"Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la Chamanangwe, Pemba, tumeanza kupima ramani ya eneo hilo, ili uwekezaji wa viwanda vya aina mbalimbali uanze kufanyika," alisema.

Balozi Amina alisema Zanzibar sasa inatekeleza sera ya kuelekea katika uchumi wa kati ambao umelenga katika kuinua kipato cha mwananchi wa kawaida.

Alisema mafanikio ya uwekezaji huo kwa kiasi kikubwa utasaidia kutoa ajira kwa vijana ikiwa ni moja ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020.

# SMZ yaipa 5 China kwa misaada

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeipongeza China kwa misaada ambayo imelenga kukuza uchumi na maendeleo katika sekta muhimu za jamii zikiwamo afya na mawasiliano.

Waziri wa Fedha na Mipango wa Zanzibar, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, alisema hayo jana wakati wa utiaji saini wa msaada wa Sh. bilioni 3.3 kutoka serikali ya China katika ofisi za wizara hiyo, Vuga mjini Unguja.

Balozi Ramia alisema Jamhuri ya Watu wa China ni miongoni mwa marafiki wakubwa wa Tanzania na nchi hiyo ilikuwa ya kwanza kuyatambua Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 1964.

Alisema baada ya kuyatambua Mapinduzi hayo, China ilianza kusaidia ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo na uchumi ikiwamo ujenzi wa viwanda vya uzalishaji wa bidhaa muhimu.

"Tunawapongeza kwa dhati marafiki zetu kutoka Jamhuri ya Watu wa China kwa misaada yao ambayo imetusaidia na kujenga uchumi imara na kupiga hatua kubwa ya maendeleo," alisema. Naye Balozi mdogo wa China aliyeko Zanzibar, Xie Xiao Wu alisema, serikali yake itaendelea kupanua wigo wa misaada yake kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo Zanzibar.

Alisema misaada inayotolewa na China imelenga katika kukuza uchumi, kuimarisha huduma za afya na kupunguza umaskini kwa ajili ya kufanikisha dira ya maendeleo 2020 malengo endelevu ya dunia.

Alisema China ilianza kutoa mikopo ya aina mbalimbali tangu mwaka 1964 ambayo baadaye ilibadilishwa na kuwa misaada.

"Tutaendelea kusaidia sekta binafsi katika ukuaji wa uchumi katika maeneo mbalimbali ikiwamo kilimo na ufugaji wa mazao ya baharini," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Khamis Mussa, alisema msaada huo umelenga katika kuimarisha sekta ya afya kwa kujenga nyumba za madaktari mkoani Pemba.

Alisema China ilijenga Hospitali ya Rufani ya Abdalla Mzee, lakini tatizo lililojitokeza ni ukosefu wa nyumba za kuishi madaktari na wafanyakazi.

# Waziri Kairuki awaotesha wanawake fursa biashara

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, amewataka wanawake kuipitia Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2019/2020 iliyosomwa wiki iliyopita bungeni ili kuangalia fursa zilizopo zitakazowawezesha kuingia kwenye uwekezaji.

Waziri Kairuki aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa wanachama wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) ulioandaliwa kwa ajili ya wanachama wake wanaojumuisha kongamano la wanawake ndani ya taasisi hiyo.

Waziri Kairuki alisema serikali kupitia bajeti hiyo imefungua fursa mbalimbali za biashara kwa kufuta ada na tozo 54 zinazotozwa na wizara, idara na taasisi zinazojitegemea.

Alhamisi iliyopita, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, akisoma bungeni bajeti hiyo alitangaza serikali ilifuta ada na tozo 54, ili kuondoa kero na urasimu kwa wafanyabiashara na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Dk. Mpango alibainisha kuwa hatua hizo ni sehemu ya kwanza za utekelezaji wa mapango wa kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (Blue Print), ambao umekuwa ni moja ya kilio cha mara kwa mara kwa wafanyabiashara.

Waziri Kairuki alisema kuondolewa kwa ada na tozo hizo kumewezesha kuweka mazingira rafiki ya biashara hususan kwa wanawake.

Pia alisema ofisi yake kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda Biashara ipo katika mchakato wa kufanya mapitio ya kwenye baadhi ya kodi na tozo ambazo siyo rafiki kwa wafanyabiashara kufanya biashara ili kuona namna ya kuziondoa.

Waziri Kairuki alisema ili kuwezesha utekelezaji wa Blue Print, serikali itawasilisha bungeni muswada wa kuwa na mfumo wa udhibiti kwa ajili ya mkakati huo.

"Tutapanga mkutano na Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Kituo cha Uwekezaji (TIC) na taasisi zinazohusika ili kuwapitisha kwenye fursa tofauti zilizopo za biashara pamoja na kubainisha njia nyepesi zaidi ya kufanya biashara," alisema.

Pia alisema ofisi yake imeanza mchakato wa kuzungumza na taasisi za fedha ikiwamo benki za NMB, CRDB, NBC, TPB na nyingine, ili kuona namna gani wataweza kurahisisha vigezo vya upatikanaji wa mitaji.

Kadhalika, Waziri Kairuki aliwataka wanawake wabadili mitazamo yao na wajielekeze kwenye umiliki wa mali kwa sababu hakuna sera wala sheria ambayo inakataza kufanya hivyo.

"Inakatisha tamaa kuona wanawake wengi hawamiliki ardhi wala nyumba ambazo hutumika kama dhamana za kuombea mikopo kwenye taasisi za fedha," alisema.

Alisema serikali inafanya kila linalowezekana kuhakikisha Tanzania kunakuwa na mazingira rafiki ya biashara ambayo pia yatamwezesha mwanamke kuwekeza.

Naye, mwakilishi wa wazalishaji wanawake kutoka TPSF, Fatma Kange, alisema msingi wa majadiliano ulikuwa ni kuwaleta wajasiriamali wanawake kote nchi waweze kubainisha vikwazo mbalimbali vinavyowakwamisha ili kuja na njia ya kuvishughulikia.

Kange alisema jukwaa hilo lengo lake ni kuzalisha wanawake mabilionea 20 kutoka mabilionea 100 ambao Rais John Magufuli, alitangaza hivi karibuni atawazalisha kabla ya kuondoka madarakani.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akikabidhi cheti kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara ya DCB, Godfrey Ndalahwa, kilichotolewa kwa kutambua udhamini wa benki hiyo katika kufanikisha kongamano la nne la kitaifa la uwezeshaji wananchi kiuchumi lililofanyika mjini Dodoma hivi karibuni. Wa (pili kulia) ni Waziri Ofisi ya Rais, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama na Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madaktari wa Marekani, Ulaya kutoa matibabu bure

**NA Idda Mushi,** MOROGORO

MAELFU ya wananchi wa mkoa wa Morogoro wanatarajia kupata huduma bure ya upimaji na matibabu kwa magonjwa ya macho, meno na elimu ya biashara kutoka kwa madaktari toka nchi za Marekani, Norway na Sweden waliowasili nchini wakiambatana na mhubiri wa kimataifa, Mchungaji Johannes Amritzer.

Watu 223 kutoka mataifa hayo wamewasili nchini wakiongozana na mhubiri huyo toka Sweden, ambaye amekuwa akifanya shughuli zake katika nchi mbalimbali za Afrika, wataendesha shughuli hizo katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro ukiwamo uwanja wa Shule ya Msingi Kiwanja cha Ndege kwa siku tano kuanzia Juni 19, hadi 23, mwaka huu.

Amritzer alisema shughuli hizo zitakwenda sambamba na mahubiri, michezo ya watoto na ushauri nasaha kwa kulenga marekebisho kwa vijana waliojiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya na waliokata tamaa, hivyo kujiingiza kwenye vitendo ambavyo ni kinyume cha maadili ikiwamo biashara ya ngono.

Akabainisha kuwa ugeni huo uliowasili nchini kupitia ya Umoja wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT), utawashirikisha wananchi wa Morogoro kumuombea Rais John Magufuli kumudu kufanya vyema kazi zake, kabla ya kukutana naye jijini Arusha mwezi ujao.

Pia watashiriki kuwaelimisha wananchi hususani vijana juu ya dhana nzima ya kujitegemea na kuiinua upya Tanzania na pia masuala yanayohusu uongozi

Mwenyeji kutoka Tanzania aliyeongozana na ujumbe huo, Miriam Lukindo Mauki, akabainisha kuwa semina kwa ajili ya masuala ya biashara itatolewa Jumamosi katika Kanisa la Bethel Revival, na kwamba nia ni kuwasaidia wote wanaotaka kuanzisha biashara, waliokwama au wanaotaka kukuza biashara zao.

# Musoma yakopesha mamilioni

**Na Sabato Kasika**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Musoma mkoani Mara imetoa mkopo wa fedha wa zaidi ya Sh. milioni 101 kwa vikundi 21 vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mkurugenzi wa Wilaya ya Musoma, John Kayombo, ndiye aliyebainisha hayo na kuongeza kuwa halmashauri hiyo bado ina zaidi ya Sh. milioni nane ambazo inatarajia kuzitoa kwa vikundi vingine kabla ya Juni 28 mwaka huu.

Aliliambia gazeti hili jana kwa njia ya simu kuwa katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, halmashauri ilitenga zaidi ya Sh. milioni 109 kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

"Mwaka huu wa fedha tumetoa mkopo wa Sh. 101,000,000 kwa vikundi 21, ambao ni sawa na asilimia 92.6, na kufikia Juni 28 tutakuwa tumemaliza kutoa fedha nyingine zilizosalia ili kutimiza lengo la asilimia 100 la utoaji wa mikopo kwa mwaka 2018/2019," alisema Kayombo.

Kayombo alivitaja vikundi vya vijana vilivyopata mkopo kuwa ni Amani Group kilichopo kijiji cha Tegeruka na cha Jenga na Sisi cha kijiji cha Mkirira, vyote vimekopeshwa Sh. milioni tano kila kimoja.

"Wengine ni vijana waendesha bodaboda wa kijiji cha Mkirira wamepata Sh. milioni 6.7, Kwikuba Carpenters wa kijiji cha Kwikubwa Sh. milioni sita na Jitahidi Ufaidike wa kijiji cha Kamguruki Sh. milioni nane," alisema.

Alifafanua kuwa vikundi hivyo vimepata mkopo wa Sh. milioni 30.7, kwa ajili ya kuendeshea biashara mbalimbali ikiwamo za useremala, ufugaji kuku, kusaga, uuzaji wa ng'ombe na kilimo cha mboga.

Kwa upande wa vikundi vya watu wenye ulemavu, Kayombo alisema Shivyawata Erusuri Group cha kijiji cha Bwai Kumsoma kimepata Sh. milioni mbili na Mifunda Walemavu wa kijiji cha Chumwi kimepata Sh. milioni 1.3 na kwamba jumla ya mkopo wao ni Sh. milioni 3.3.

"Vikundi vya wanawake vilivyopata mkopo ni vingi zaidi nikianzia Upendo Women Group cha kijiji cha Bwai Kwitururu na Imani Chumwi, vyote vimepata Sh. milioni tano kila kimoja," alisema.

Alivitaja vikundi vingine kuwa ni Mtakatifu Jema cha kijiji cha Maneke, Tumaini Group cha kijiji cha Kwikubwa, kila kimoja Sh. milioni tano na Imuca Group cha kijiji cha Chumwi, Sh. milioni nne.

Alivitaja vikundi vya kinamama Vicoba cha kijiji cha Busungu, Upendo Group cha kijiji cha Chumwi na Tujikombo Group cha kijiji cha Rukuba, ambavyo vyote kila kimoja kimepata mkopo wa Sh. milioni tano.

"Kuna Bomafa cha kijiji cha Kinyang'erere na Kuludala cha kijiji cha Buraga, kila kimoja kimekopeshwa Sh.milioni tatu na pia kuna Upendo Group cha kijiji cha Chitare, kimekopeshwa Sh. milioni saba," alisema.

Vingine kuwa ni Matumaini Group cha kijiji cha Tegeruka, Mkombozi Group cha kijiji cha Mkirira na Amani na Upendo cha kijiji cha Kigera Etuma na kwamba kila kimoja kimepata Sh. milioni tano.

Alifafanua vikundi hivyo vimepata jumla ya Sh. milioni 67 na kwamba vinajishughulisha na biashara mbalimbali zikiwamo za uuzaji wa nafaka, kilimo cha bustani za mboga na matunda, ufugaji wa kuku.

# Chumvi ya chakula yagunduliwa mwezini

**WASHINGTON, Marekani**

WANASAYANSI wamegundua chumvi inayoweza kutumika katika chakula iliyopatikana mwezini.

Hatua hiyo inakuja baada ya kubaini kuwa bahari kubwa inayopatikana katika mwezi wa sayari ya Jupiter ina chumvi- kama ile inayotumia katika chakula.

Kwa mujibu wa wanasayansi, wamekuwa wakitumia darubini ya Hubble kuchunguza mwezi, kwa muda mrefu sasa na imepata chumvi kama ile inayotumiwa katika chakula.

Chumvi inayotumika katika chakula ndiyo inayozifanya bahari kuwa na chumvi. Watafiti walisema inamaanisha kwamba bahari inakabiliwa na milipuko ya volcano mara kwa mara.

Walisema inafurahisha kwa sababu ripoti hiyo inaongeza fursa ya kuwepo kwa ishara za maisha ya ziada huko kwenye mwezi.

Duniani maisha yanasemekana kuanzia eneo la chini la bahari lenye maji yanayochemka.

Kwa mujibu wa Shirika la Anga za Juu, nchini Marekani Nasa, linakaribia kuanza uchunguzi mwezini, huku ujumbe wa kwanza ukitarajiwa kuondoka duniani mwaka 2023.

Hadi kufikia wakati huo, wakati pekee ambao wanasayansi wameuona mwezi kwa karibu ni mwisho wa miaka ya 90 na mapema mwaka 2000 kupitia ndege iitwayo Galile.

Kazi hiyo ilifanyika kwa kutumia mwanga uitwao Infrared, wanasayansi hao walitafuta vipengele mbalimbali kwa kutumia mionzi ya mwanga huo. Chumvi hiyo ilipatikana hususan karibu na barafu na safu ya milima inayopita katika sakafu yake.

Profesa Mike Brown kutoka Taasisi ya Teknolojia ya California, alisema: Tumekuwa na uwezo kufanya tathmini na darubini kwa takriban miaka 20. ''Ni kitu ambacho hakuna aliyefikiria kukifanya,'' alisema.

**Walisema inafurahisha kwa sababu ripoti hiyo inaongeza fursa ya kuwepo kwa ishara za maisha ya ziada huko kwenye mwezi.**

*BBC*

# Serikali yakataa Morsi kuzikwa nyumbani kwake

**CAIRO, Misri**

RAIS wa zamani wa Misri aliyefariki dunia juzi mahakamani, Mohammed Morsi (pichani), amezikwa saa chache baada ya kifo huku mazishi yake yakihudhuriwa na wanafamilia.

Aidha, mtoto wa kiongozi huyo ameeleza kuwa serikali imekataa familia kumzika kiongozi huyo kwenye makazi yake.

Wakili wa Morsi aliliambia shirika la habari la Ufaransa, AFP kuwa kiongozi huyo wa zamani alizikwa mashariki mwa jiji la Cairo jana asubuhi na familia yake ikiwapo.

Morsi, aliyekuwa na miaka 67, alikuwa rumande tangu alipoondolewa madarakani mwaka 2013.

Makundi ya watetezi wa haki za binadamu, ambayo yalikosoa mazingira ambayo Morsi aliwekwa huko rumande, yametoa wito wa kufanyika uchunguzi kuhusu kifo chake.



Familia yake na wanaharakati wamezungumzia kifo hicho na kujadili muda ambao aliwekwa katika seli ya peke yake, akizuiliwa kutembelewa na wanasheria wake pamoja na familia yake.

Mtoto wake, Abdullah Mohamed Morsi, aliliambia shirika la habari la Uingereza, Reuters juzi Jumatatu kuwa mamlaka za Misri ziliikatalia familia yake kufanya maziko katika mji yalipo makazi ya rais huyo wa zamani.

Kiongozi wa juu wa zamani wa kundi lililopigwa marufuku nchini humo la Muslim Brotherhood, alikuwa rais wa kwanza kuchaguliwa kidemokrasia mwaka 2012.

Aliondolewa na kushikiliwa baada ya mapinduzi ya kijeshi mwaka mmoja baadaye baada ya kufanyika maandamano makubwa kupinga utawala wake. Abdul Fattah al-Sisi, kiongozi wa zamani wa kijeshi, amekuwa madarakani tangu mwaka 2014.

Baada ya kuondolewa madarakani, mamlaka zilipambana na wafuasi wake na wapinzani wengine na kukamata maelfu ya watu.

Muslim Brotherhood na Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, mshirika wa karibu wa Morsi ni miongoni mwa walioshutumu utawala wa Misri kuhusu kifo cha Morsi.

Jumatatu wiki hii Morsi alikuwa mjini Cairo kwa mashtaka ya kufanya vitendo vya kijasusi ikihusisha kuwa na mawasiliano na kundi la wanamgambo wa Kiislamu la Kipalestina, Hamas.

Maofisa walisema aliomba kuzungumza mahakamani na kuongea kwa dakika tano kutoka kwenye kizimba kilichokuwa na kioo ambacho alikuwamo ndani yake na washtakiwa wengine.

Dakika chache baadaye alizimia wakati wa mapumziko mahakamani hapo. ''Alipelekwa hospitali na huko alithibitishwa kupoteza maisha,'' taarifa ya mwendesha mashtaka ilieleza.

Maofisa walisema katika ripoti yao kuwa hakuna majeraha yeyote ambayo yalionekana kwenye mwili wake. Awali Televisheni ya Taifa ilieleza kuwa chanzo cha kifo chake ni mshtuko wa moyo.

Hadi mauti ilipomkuta Mosri alikuwa anatumikia kifungo kutokana na mashtaka matatu yaliyokuwa yakimkabili. Awali alihukumiwa adhabu ya kifo, ambayo baadaye ilitenguliwa.

*BBC*



Bahari iliyoko mwezini, ambayo sasa imethibitika ina chumvi. **PICHA :BBC.**

# Marekani kupeleka vikosi zaidi Ghuba

**WASHINGTON, Marekani**

JESHI la Marekani litatuma kikosi zaidi cha wanajeshi 1,000 kwenda Mashariki ya Kati wakati kukiwa na hali ya mvutano na Iran.

Waziri wa Ulinzi, Patrick Shanahan, alisema hatua hiyo ni kutokana na kile alichodai kuwa 'tabia za uchokozi' zinazodaiwa kufanywa na vikosi vya Iran.

Vikosi vya maji vya Marekani vilionyesha picha mpya, wakiihusisha Iran na vitendo vya mashambulizi dhidi ya meli ya kubeba mafuta katika Ghuba ya Oman.

Iran ilitangaza juzi Jumatatu kuwa haitatekeleza sehemu ya makubaliano ya mwaka 2015 kuhusu nyuklia.

Ilisema itavunja makubaliano yaliyofikiwa na mataifa yenye nguvu kuhusu zana za nyuklia ifikapo Juni 27 mwaka huu. Iran ilitangaza kuwa itakiuka makubaliano ya nyuklia.

Kutumwa kwa vikosi vya Marekani kwenye eneo la Mashariki ya Kati kulitangazwa na Shanahan mapema Jumatatu.

Katika taarifa yake, alisema: "Marekani haitafuti mgogoro na Iran, lakini hatua imechukuliwa ili 'kuhakikisha kunakuwa na usalama na ustawi wa wanajeshi wanaofanya kazi katika ukanda huo kulinda maslahi ya taifa."

"Mashambulizi ya hivi karibuni ya Iran yanaonyesha wazi ni vitendo vya kichokozi vya vikosi vya Iran na mawakala wake ambayo yametishia wanajeshi wa Marekani na maslahi yake katika ukanda mzima."

Alisema jeshi litaendelea kufuatilia hali ilivyo eneo hilo na kufanya marekebisho ya vikosi ipasavyo.

*BBC*

# Mwalimu mkuu adaiwa kumpa ujauzito mwanafunzi la saba

**Na Joctan Ngelly, Kigoma**

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Nyantole, Jason Rwekaza (42), anashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kigoma kwa tuhuma za kumpatia ujauzito mwanafunzi wa darasa la saba (umri na jina vinahifadhiwa).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Martin Otieno, alisema mwalimu huyo alikuwa anafanya mapenzi na mwanafunzi huyo, hivyo kumpatia ujauzito uliosababisha kukatisha masomo yake.

Otieno alisema alipata taarifa kutoka kwa mama mzazi na hatimaye kumkamata mtuhumiwa huyo na yuko nje kwa dhamana wakati upelelezi unaendelea na utakapokamilika atafikishwa mahakamani ili sheria ichukuwe mkondo wake.

Aidha, kamanda huyo alisema matukio ya kuwapa wanafunzi ujauzito yamekithiri katika mkoa wa Kigoma, hivyo kuwataka wananchi wa mkoani hapa hasa kinamama kutoa ushirikiano kwa polisi, ili kuhakikisha watuhumiwa wanapata adhabu stahiki.

Alisema wananchi wengi wana tabia ya kumalizana pindi inapotokea mtoto wake amepewa ujauzito kwa kumalizana nyumbani, tabia ambayo si nzuri kwa kuwa inachochea kuenea kwa vitendo hivyo.

Wakati huo huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Wilaya ya Kigoma, Pendo Mangali, alisema wameanzisha utaratibu wa kuwapima ujauzito wanafunzi kila baada ya miezi mitatu katika shule za msingi na sekondari.

Mangali alisema Mei 15, mwaka huu, alimwagiza Mratibu Elimu Kata afuatilie upimaji wanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Nyantole iliyokuwa inatarajia kufanya mtihani kwa mara ya kwanza. Alisema baada ya maelekezo hayo, mwalimu mkuu hakutekeleza agizo hilo.

Alisema baada ya mwalimu mkuu kushindwa kutekeleza agizo hilo, Juni 3, mwaka huu, Mratibu Elimu Kata alibaini kati ya wanafunzi waliopimwa mmoja alikuwa mjamzito.

Mangali alisema baada ya mwanafunzi huyo kubainika kuwa ni mjamzito, walimpeleka katika kituo cha polisi Mwandiga ili amtaje mhusika na alipewa fomu ya matibabu ya polisi ( PF3) na kwenda Hospitali ya Mkoa Maweni kwa uchunguzi zaidi.

Alisema baada ya daktari kumpima, alibaini kuwa mwanafunzi huyo ni mjauzito na walirudi kituo cha polisi Mwandiga ndipo alipohojiwa na kumtaja mwalimu mkuu wa shule hiyo, Rwekaza, kuwa ndiye aliyempatia ujauzito huo.

Alisema baada ya kumtaja mtuhumiwa huyo alikamatwa na kumfungulia kesi ya kumpa mwanafunzi mimba.

"Kwa sasa suala hili liko chini ya vyombo vya sheria ili lifanyiwe kazi ipasavyo," alisema.



Meneja Masoko ya Nje wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tan-Trade), Stephen Kaborou (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Suji Soya, Yohana Sefue, katika maonyesho ya wajasiriamali yaliyoandaliwa na Kanisa la Waadventista Wasabato la Makongo Juu, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanafunzi wanusurika kifo nyumba ikichomwa moto

**Na Said Hamdani, LINDI**

WANAFUNZI wanne wamenusurika kuteketea kwa moto, baada ya watu wasiojulikana kuvamia na kuchoma nyumba yao kata ya Nyengedi, wilayani Lindi, mkoani Lindi.

Wanafunzi walionusurika ni Hadija Gamblo (15), anayesoma darasa la saba, Tumanno Gamblo (11) darasa la tatu, Leshda Membe (7) wa darasa la kwanza na Rajabu Shabani (13), darasa la tatu.

Habari kutoka kijijini humo na kuthibitishwa na Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Thomas Ngomo, zilisema kuwa wakati tukio hilo likifanyika mama wa watoto hao, Amina Ibrahimu (45), alikuwa amekwenda kijiji jirani kwenye msiba.

"Ni kweli hiyo taarifa ipo na hivi ninapoongea na wewe usiku huu mimi nipo eneo la tukio tukishirikiana na wenzangu kuzima moto," alisema Ngomo.

Alisema moto huo ulichomwa eneo la ua uliokuwa umezungushiwa miti na kuezekwa kwa makuti na uligunduliwa na mmoja wa watoto hao aliyekuwa akitaka kutoka nje ili kujisaidia.

Alisema alipoamka aliona moto huo ukiwa unaunguza nyumba yao na kuwaamsha wadogo zake, huku akipiga kelele za kuomba msaada kutoka kwa majirani zao, ambao walijitokeza na kusaidia kuuzima, baadhi yao wakijaribu kuokoa vifaa bila ya mafanikio.

Mmoja wa wanafunzi hao, Hadija, alimweleza mwandishi wa habari hizi kuwa aliona moto ukiwa unateketeza kwa kasi nyumba yao, jambo lililomfanya akatishe kwenda kujisaidia na kwenda kuwaamsha ndugu zake kuokoa maisha yao.

Alisema wakati akiwa amewashika wadogo zake kuelekea mlango wa kutokea waliukuta ukiwa umefungwa kwa nje na kulazimika kupiga yowe kuwaomba majirani wawafungulie.

"Tunamshukuru Mungu na majirani waliojitokeza kuwahi kutufungulia vinginevyo leo majina yetu yangebadilika na kuitwa marehemu," alisema Hadija.

Mashuhuda wa tukio hilo, Juma Yusufu, Mariamu John na Hemedi Selemani, walisema wakati wakiendelea na uzimaji wa moto, walipiga simu Kituo cha Polisi cha Mtama, ambao walifika kuchukua maelezo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP Podinsiana Protas, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alisema hajapata taarifa na kuahidi kufuatilia.

Hili ni tukio la pili kutokea ndani ya wiki moja kwa watu wasiojulikana kuchoma moto nyumba mkoani hapa, juzi ofisi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) ilichomwa moto na kusababisha hasara kubwa.

## NMB yatoa semina elekezi kwa wataalamu wa MSD

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB kupitia kitengo cha 'Trade Finance' na 'Corporate Banking' imetoa semina kwa baadhi ya maofisa wa Bohari ya Dawa (MSD) nchini ikiwa ni kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Maofisa 17 kutoka kitengo cha Uhasibu cha Bohari ya Dawa nchini wamejengewa uwezo huo na wataalamu wa masuala ya biashara kutoka Benki ya NMB ikiwa ni utaratibu wa kawaida kuwajengea uwezo wateja wao wakubwa wanapokuwa na uhitaji.

Akizungumza katika semina hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam, Meneja Uhusiano Mwandamizi Idara ya Fedha NMB, Louis Kavira, alisema benki hiyo imetoa semina hiyo kuwajengea uwezo MSD kwenye utendaji wa biashara kimataifa.

Alisema MSD hivi karibuni imefanikiwa kupata tenda ya kuwa mnunuzi mkuu wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara kwa ajili ya nchi 16 wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), hivyo wakiwa kama wateja wao wameamua kuwajengea uwezo kufanikiwa zaidi katika tenda hiyo.

Aidha, alisema huo ni utaratibu wa kawaida kuwajengea uwezo wateja wao wakubwa kupitia vitengo vya Trade Finance na Corporate Banking kutoka Benki ya NMB.

Naye mmoja wa washiriki wa semina hiyo, Ofisa Viatarishi wa MSD, Hassan Ally, alisema mafunzo hayo yamewasaidia kujenga uwezo kuhusu ufanyaji biashara hasa za kimataifa na kuishukuru NMB kwa hatua hiyo. Aliiomba kuendeleza ushirikiano huo na kutanua wigo na hata kutatua kwa haraka changamoto pale zinapotokea kwa wateja wao.

Oktoba mwaka jana (2018), MSD ilisaini mkataba wa makubaliano kuwa mnunuzi mkuu wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara kwa ajili ya nchi 16 wanachama wa SADC.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,

2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**


## NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA KAZI ,** Mtu wa IT diploma anahitajika na Mesenger form six. Mawasiliano: 0715 885533


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI**


## KUPOTEA KWA VYETI



**Wakati Tesha** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo: Kidato cha nne chenye index namba **S0620-0064** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2001 katika Shule ya Sekondari Tegeta, Cheti kilichotolewa na chuo cha University of Dar es Salaam chenye namba **00104** kilichotolewa mwaka 2007. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **UTE/RB/179/2019**

115281802

## CHETI KIMEPOTEA



**ESTHER JUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2804-0018** kilichotolewa na MUSOMA UTALII SEKONDARI mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DSM/RB/42956/2019.**

115282602


## PASSPORT IMEPOTEA



**HAPPINESS PHEDSON MWAMBETE** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **AB 457760** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam mwaka 2018. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **KMR/RB/11789/18.**

115281002

## CHETI KIMEPOTEA



**JOHN STEPHEN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.353/31** kilichotolewa na PARANE SEKONDARI mwaka 1985. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CD/RB/3699/2019.**

11282902

## TANGAZO LA KUPOTELEWA VYETI 30 VYA KIDATO CHA NNE.

**Agha Khan Mzizima** Secondary School- **S0335.** Inatangaza kupotelewa vyeti ***30 vya kidato cha nne*** vilivyotolewa na Baraza la ***Mitihani la Taifa mwaka 2012.*** Aidha shule imetoa taarifa ya kupotea kwa vyeti hivyo kituo kikuu cha polisi-Dar es Salaam, na kupewa RB Namba **DAR/SEL/RB/65326/2019** ya tarehe 12/05/2019.

115282102

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**SAMWEL LAURENT MBOYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya **SANLING** yenye namba za usajili **T 131 ASF.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KW/BI/I/VO/LXXW/59.**

115282702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA TARAKA NAMBA:47..2019.**

**Mdai: BAKARI MOHAMED NYUMBA**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: SALAMA MOHAMED BANGANYOKA**

**Kwa:**
**SALAMA MOHAMED BANGANYOKA**
**WA OMAN**

**Ombi la mdai; BAKARI MOHAMED NYUMBA**

**Madai ya: TARAKA**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 01 mwezi 07 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 18 mwezi 06 mwaka 2019

215282802


**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767 223 311**

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311***



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MADRID YATAJA BEI YA POGBA

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Real Madrid imeiambia Manchester United kwamba, watalipa pauni milioni 90 tu kwa ajili ya kumsajili Paul Pogba kipindi hiki cha majira ya joto, lakini 'Mashetani Wekundu' hao wanajiandaa kumpa mkataba mpya ili abakie hapo Old Trafford.


Pogba mwishoni mwa wiki alisema kwamba, anataka kuondoka Manchester United ili kwenda kutafuta changamoto nyingine na Real Madrid ndiko anakoelekea.

Kwa mujibu wa Gazeti la The Sun, Real imesema kwamba watalipa kiasi cha pauni milioni 90 tu kwa ajili ya kumsajili Pogba, ingawa United wanataka walipwe kiasi cha pauni milioni 150.

'Los Blancos' hao wamebainisha kwamba hawawezi kulipa zaidi ya kiasi hicho na hawataweza kufikia bei ambayo Man United wanaitaka.

Pogba mwenyewe tayari ameanza kuwaaga mashabiki, wachezaji wenzake pamoja na maofisa wa klabu hiyo na kwamba sasa safari yake ya kwenda Real Madrid imekaribia.

Hata hivyo, Gazeti la Daily Mail limeripoti kwamba, United inapanga kumpa ofa kubwa Pogba ya mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki ikiwa ni sehemu ya kumshawishi abakie hapo Old Trafford.





# LAMPARD

## KUPEWA MIAKA MI3 CHELSEA

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea imeripotiwa kwamba inakaribia kumalizana na kocha wa Derby County, Frank Lampard wiki hii na watampa mkataba wa miaka mitatu kuchukua mikoba ya Maurizio Sarri, kwa mujibu wa ESPN FC.

Kuondoka kwa Sarri ambaye amekwenda kuchukua mikoba kule Juventus kulithibitishwa Jumapili, huku Mkurugenzi wa Chelsea, Marina Granovskaia akisema kwamba Muitaliano huyo mwenye umri wa miaka 60, aliomba kurudi Italia ili kuwa karibu na familia na marafiki zake.

Lampard ametajwa kuwa ndiye chaguo sahihi kuchukua mikoba ya Sarri pale Chelsea ambapo atakuwa pamoja na Jody Morris na Chris Jones kama wasaidizi wake.

Derby walitaka kumbakisha Lampard baada ya kuwa na msimu mzuri na ilikaribia kupanda Ligi Kuu.

Chelsea italazimika kulipa kiasi cha pauni milioni nne kwa Derby kama fidia ili waweze kumuachia Lampard na wana uhakika wa kupata kiasi hicho baada ya Chelsea kupata pauni milioni tano kutoka Juventus ikiwa ni fidia ya kumchukua Sarri.

"Hakuna cha kubadilika, kwa sasa tunatarajia Lampard atajiunga na Chelsea na hataendelea kuwa kocha wetu," alisema mmiliki wa Derby, Mel Morris akinukuliwa na Gazeti la Daily Mail.

# Neymar sasa kurudi Barca

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona ipo 'siriazi' kumrudisha Neymar katika dimba la Camp Nou msimu ujao, kwa mujibu wa ESPN FC.

Barca kwa sasa wapo kwenye mazungumzo na Paris Saint-Germain kuhakikisha kwamba wanamchukua mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kutoka kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

"Kumsajili Neymar ndilo litakuwa jambo rahisi zaidi," kimesema chanzo kimoja kutoka ndani ya Barcelona kikiiambia ESPN FC.

Kwa mujibu wa taarifa za nchini Hispania, mabingwa hao wa La Liga wamefanya mazungumzo ya moja kwa moja na watu wa Neymar na mchezaji mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kurudi Barca.

Neymar alijiunga na PSG kutoka Barca kipindi cha majira ya joto mwaka 2017 kwa euro milioni 222, na kumfanya kuwa mchezaji ghali zaidi duniani.

Sababu kubwa ya Barca kutaka kumrudisha mchezaji huyo ni kwa sababu wachezaji wenzake ndani ya Barcelona pia wanamhitaji kwenye kikosi hicho.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil ni rafiki mzuri na Lionel Messi na Luis Suarez kwa pamoja.

Na Messi hivi karibuni alielezea kwamba amekuwa akizungumza mara kwa mara na Neymar kupitia kundi lao la WhatsApp walilolipa "Watatu wa Amerika Kusini."



## HABARI MICHEZO



# TERRY
## KUCHUKUA MIKOBA YA LAMPARD

**LONDON, England**

JOHN Terry ni miongoni mwa watu wanaotajwa kwamba wanakwenda kuwa kocha mpya wa Derby, kuchukua mikoba ya Frank Lampard.

Terry amekuwa kwenye benchi la ukocha la Aston Villa tangu Oktoba na aliisaidia timu hiyo ya kocha, Dean Smith kufuzu kucheza Ligi Kuu.

Terry mwenye umri wa miaka 38, amekuwa hapo Villa na ameweza kuwaimarisha wachezaji kama Tammy Abraham, Tyrone Mings na Axel Tuanzebe.

Nahodha huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya England, anaonekana kwamba ndiye anayefaa kuchukua mikoba ya kuinoa Derby kuchukua nafasi ya mchezaji mwenzake wa zamani pale Chelsea, Lampard.

Derby bado haijapokea ofa rasmi kutoka kwa Chelsea kwa ajili ya Lampard, lakini inatarajiwa kutumwa ndani ya saa 48 zijazo.

Lampard amebakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake na yeye mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kwenda pale Stamford Bridge.

## KIPA ANAYEWANIWA ARSENAL KUTUA SCHALKE

**LONDON, England**

GOLIKIPA ambaye alikuwa akiwaniwa na Klabu ya Arsenal, Markus Schubert, sasa anajiandaa kujiunga na Schalke.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 21, kutoka Klabu ya Dynamo Dresden alikuwa kwenye mazungumzo ya muda mrefu na 'Washika Bunduki' hao kwa ajili ya kujiunga nao ili kusaidiana na Bernd Leno.

Kocha wa Arsenal, Unai Emery amekuwa sokoni kwa ajili ya kumtafuta kipa mpya baada ya Petr Cech kustaafu mwishoni mwa msimu huu.

Arsenal hadi sasa haijafanya usajili wowote mkubwa na kipa huyo ndiye alionekana kama angetua kwa miamba hao wa jijini London.

Hata hivyo, Arsenal watamkosa kipa huyo, Schubert na sasa anapanga kuhamia kwa miamba hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Kipa huyo anakwenda Schalke kuzidisha ushindani dhidi ya Alexander Nubel, ambaye naye amekuwa akiwaniwa na Klabu ya Bayern Munich.

Miamba hao wa Ujerumani wanaonekana kuwa wamekuwa wakimwania kipa huyo namba moja wa Dynamo Dresden kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao na sasa ni wazi safari yake ya kwenda kule Emirates itashindikana.



# Chelsea yazikatalia Barca, Atletico Madrid kwa Willian

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea imeripotiwa kwamba, imekataa ofa ya pauni milioni 35 kutoka kwa Barcelona na Atletico Madrid kwa ajili ya kumuuza Willian.

Wiga huyo wa Brazil hivi karibuni ataingia mwaka wa mwisho katika mkataba wake wa sasa pale Stamford Bridge na bado hajakubali kusaini mkataba mpya na 'Blues' hao kwa mujibu wa Sky Sports.

Chelsea inataka kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kipindi cha majira ya joto, hasa wakati huu ambapo wamefungiwa kufanya usajili na Shirikisho la Soka la Kimataifa, Fifa.

Hata hivyo, wanakabiliwa na uwezekano wa kumpoteza Willian kama mchezaji huru kama watashindwa kufikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na mchezaji huyo.



Willian amekuwa hapo Stamford Bridge tangu mwaka 2013, wakati alipojiunga nao akitokea Klabu ya Urusi ya Anzhi Makhachkala.

Amecheza mechi 292 kwa Blues hao, akifunga mabao 52 na kutoa pasi za mwisho 53.

Majaliwa yake yamekuwa kwenye wakati mgumu hapo Chelsea ambao kwa sasa hawana kocha.

Frank Lampard anatarajia kufanya mazungumzo ya uso kwa uso na mmiliki wa Chelsea, Roman Abramovich na mapema wiki hii anajiandaa kuchukua mikoba ya Maurizio Sarri, ambaye amejiunga na Juventus.

Bilionea huyo wa Urusi anatarajia kumpa mkataba wa miaka mitatu kocha wa Derby County, Lampard na anatarajia kumwaga wino ndani ya saa 48 zijazo.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SUAREZ AMTAKA NEYMAR, AMPOTEZEA GRIEZMANN

Yeye ni mchezaji bora, lakini ni wa Atletico na sipendi kutoa maoni yangu, nani ambaye hataki....

**RIO, Brazil**

Luis Suarez ameongeza hofu juu ya matarajio ya Antoine Griezmann kujiunga na Barcelona kwa kupuuza kutoa maoni yake kuhusu uhamisho huo, huku akionyesha ishara ya kuunga mkono kurejea kwa Neymar.

Griezmann anadhaniwa kuwa njiani kutua Camp Nou baada ya kutangaza uamuzi wake wa kuondoka Atletico Madrid, lakini Rais wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu amedai 'Blaugrana' hao hawajazungumza na mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 28.

Alipoulizwa matarajio yake ya kupangwa sambamba na Griezmann katika msimu wa 2019-20, Suarez alirejea maoni yake ya Desemba 2017 wakati alipogeukia kuelezea kushinda Kombe la Dunia kama "mchezaji wa daraja la juu", lakini akisita kuunga mkono uhamisho huo.

Suarez aliiambia RACI: "Ninachosema, kama nilivyosema mwaka jana, yeye ni mchezaji bora.

"Lakini ni mchezaji wa Atletico na sipendi kutoa maoni yangu katika hili."

Na taarifa zinazomhusisha nyota wa Brazil, Neymar kurejea Barcelona kufuatia kuwa na msimu wa pili mbaya pale Paris Saint-Germain, Suarez alifunguka kuwa atamkaribisha tena kwa mikono miwili, akisema: "Ni nani ambaye hatataka kufurahia wachezaji kama Ney?"

Suarez atafikisha miaka 33 Januari mwakani na amesema anakubali klabu itakuwa ikitazama mfungaji wa mabao ambaye anaweza kurithi mikoba yake.

"Mchezaji wa Barca anapaswa kujiandaa kwa mashindano na klabu kuleta mchezaji mnayeelewana ambaye anaweza kukuiga wakati wowote. Wote tunataka kuisaidia klabu," aliongeza.

"Sitasema yupi wa kumleta ama wa kutomleta hapa.

"Nilichukua msimu uliopita na nadhani kwa miaka michache ijayo klabu hii italeta mchezaji kinda, namba tisa, si tu kushindana na mimi bali kwa mustakabali wa siku zijazo kwa klabu, kwa sababu mimi pia nataka kilicho kizuri kwa siku zijazo kwa klabu.

"Nadhani kuhusu majukumu yangu kwa sababu nina miaka 32 na ninaelekea kutimiza 33."

## KWA UFUPI

**POGBA KUONGEZWA MSHAHARA**

Manchester United itampa kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26, ofa ya mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki wakati huu saini yake ikisakwa na Real Madrid na Juventus. ***(Mail)***

**BAYERN BADO KUMFUATA BALE**

Bayern Munich haijatoa ofa yoyote kwa winga wa Real Madrid, Gareth Bale, 29, amesema nyota huyo wa kimataifa wa Wales. ***(ESPN)***

**LAMPARD, ABRAMOVICH KUTETA**

KOCHA wa Derby, Frank Lampard anajiandaa kukutana na mmiliki wa Chelsea, Roman Abramovich kwa lengo la kujadili uwezekano wa kurithi mikoba ya Maurizio Sarri. ***(Sun)***

**MBAPPE AWAPAGAWISHA LIVER**

MASHABIKI wa Liverpool wanatumai mshambuliaji wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe anaweza kusaini kuichezea timu hiyo baada ya mchezaji huyo kuwajongea wachezaji wachache wa klabu hiyo kwenye mtandao wa kijamii wa Instagram. ***(Express)***

**BENFICA YAIKANA ATLETICO KWA FELIX**

Benfica imepuuzia taarifa kuwa Atletico Madrid inajiandaa kuipiku Manchester City kwa dau la pauni 107 kumsajili mshambuliaji MrenoJoao Felix, 19, ikiziona kama "taarifa za uongo". ***(AS)***

**WILLIAN AGOMEWA KUTUA BARCA**

Chelsea imekataa ofa ya pauni milioni 35 kutoka Barcelona na Atletico kwa mshambuliaji Mbrazil Willian, 30. ***(Sky Sports)***

**COUTINHO ASUBIRIWA PSG**

Paris St-Germain inataka kumaliza dili na Barcelona la kumsajili mshambuliaji Mbrazil Philippe Coutinho, 27, baada ya michuano ya Copa America. ***(AS)***

**TERRY KUKALIA KITI CHA LAMPARD**

KOCHA msaidizi wa Aston Villa, John Terry ni miongoni mwa wanaowania kuwa kocha mkuu wa Derby kama Frank Lampard atajiunga na Chelsea majira haya ya joto. ***(Mail)***

**LIVER YAITIWA DEMBELE BARCA**

Liverpool imeambiwa na Barcelona kuwa inaweza kumfuata mshambuliaji Mfaransa Ousmane Dembele, 22, lakini ni endapo tu itakubali kulipa zaidi ya pauni milioni 90. ***(Teamtalk)***

**WAN-BISSAKA AITESA UNITED**

Manchester United imetoa ofa iliyoongezeka hadi kufikia pauni milioni 50 kwa beki wa kulia wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka, 21, lakini hata hivyo imekataliwa. ***(Sky Sports)***

**MARTINEZ KUMUONDOA LUKAKU UTD**

MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, 26, ameambiwa na kocha wake wa timu ya Taifa, Roberto Martinez kuwa "anapaswa kuondoka Manchester United". ***(Het Laatste Nieuws - in Dutch)***

**LEIGHTON KUSAINI EVERTON**

Everton inaamini beki wa kushoto wa England, Leighton Baines, 34, atasaini mktaba mpya. ***(Liverpool Echo)***



HABARI MICHEZO

# MATOLA AHITAJI 10 WAPYA KUIPAISHA POLISI TANZANIA

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA mpya wa Polisi Tanzania, Selemani Matola, amesema anatarajia kusajili wachezaji wapya wasiopungua 10 katika kikosi hicho ili waweze kufanya vema katika msimu ujao wa 2019/20 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Matola, alisema ameshaanza mazungumzo na Kamati ya Usajili ya timu hiyo, na anaamini usajili huo ukitekelezeka kwa asilimia 100, Polisi Tanzania itakuwa na kikosi imara.

Matola alisema ili timu hiyo iliyopanda daraja msimu huu iweze kushindana Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA, ni lazima afanye maboresho katika kikosi hicho.

"Polisi Tanzania ndiyo timu iliyoisumbua Lipuli katika mashindano ya Kombe la FA, ulikuwa mchezo mgumu sana mwanzo mpaka mwisho, ndio maana nasema sio kama wana kikosi kibaya, lakini kuboresha kikosi ni jambo lisiloepukika, tunatakiwa kuwa imara zaidi kwa sababu tunatarajia kufanya makubwa," alisema Matola.

Kocha huyo ambaye alipoteza mchezo wake wa Kombe la FA dhidi ya Azam FC ya jijini, alisema pia tayari ili kujiweka sawa, atapenda kuona anapata mechi za kirafiki dhidi ya timu ngumu au za nje ya Tanzania kuelekea msimu mpya.

"Usipojipanga mapema mambo yatahaaribika, inapaswa kuanza msimu na kikosi ambacho kimeshakuwa tayari, ukisubiri wachezaji wafahamiane na kuzoeana katikati ya ligi, mambo ya Play Off yanaweza kukukumba," Matola, kiungo na nahodha huyo wa zamani wa Kagera Sugar, Simba na Supersport ya Afrika Kusini alisema.

Mbali na Polisi Tanzania ambayo inatumia Uwanja wa Chuo cha Polisi Moshi mkoani Kilimanjaro, timu nyingine iliyopanda daraja ni Namungo FC ya Ruangwa, Lindi.

BINGWA...



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akionyesha Kombe la Ushindi baada ya kukabidhiwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa pili kushoto) kufuatia timu ya mpira wa miguu ya CRDB kuifunga timu ya Bunge FC kwa mikwaju ya penalti 3-1 katika Bonanza lililofanyika Jumamosi kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Netiboli kuchuana vikali Dodoma

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha mchezo wa Pete 'Netball' Tanzania (Chaneta), kinajiandaa na mashindano ya Klabu Bingwa yatakayoanza kutimua vumbi jijini Dodoma kuanzia Agosti 29 hadi Septemba 5, mwaka huu, huku yakishirikisha timu zote za mikoa zilizopanda daraja katika mashindano yaliyopita.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Chaneta, Devota John, alisema michuano hiyo itakayoshirikisha jumla ya timu 13, mwisho mwa kuthibitisha ushiriki itakuwa Julai 30, mwaka huu.

"Maandalizi kwa ajili ya mashindano yetu ya klabu bingwa yanaendelea vizuri kila kitu kinakwenda sawa, huku tukiendelea kufanya mawasiliano na timu ambazo zinatarajia kushiriki," alisema Devota.

Devota alisema mashindano hayo yanatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa na kwamba wamekuwa wakipokea taarifa kutoka kwa timu mbalimbali zikieleza zinafanya maandalizi makubwa kuelekea michuano hiyo.

"Tunaomba mdau yeyote anayetaka kutusaidia msaada wowote ajitokeze mapema ili tuweze kufanikisha mashindano yetu hasa ukizingatia tunakwenda kufanya kwenye mkoa ambao kwa sasa umefanikiwa kuwa na watu wengi," alisema kiongozi huyo.

# Dula Mbabe atamba kumkalisha Mmalawi

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini Abdallah Shabani 'Dula Mbabe', ametamba vikali kumfumua mpinzani wake kutoka Malawi kwenye pambano lao la kuwania mkanda wa UBO Afrika katika uzito wa kilo 76, litakalofanyika Julai 27, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Dula Mbabe alisema ingawa bado hajatajiwa jina la mpinzani wake huyo kutoka Malawi, yeye anaendelea kujifua kuelekea pambano hilo kwa kufanya mazoezi kila siku asubuhi na jioni akiwa chini ya mwalimu wake Omari Dame.

**"Nimejipanga vizuri kwa ajili ya pambano langu dhidi ya Mmalawi, nawaahidi mashabiki wangu kuibuka na ushindi siku ya pambano kutokana na mazoezi ya nguvu ninayopewa na mwalimu wangu, Omari," alisema Dula Mbabe.**

Bondia huyo alisema licha ya pambano kuonekana kuwa na ushindani mkubwa, atatumia mbinu anazoendelea kupewa na mwalimu wake ili zimlinde atakapokuwa amepanda jukwaani.

"Nazifanyia kazi mbinu ambazo ninaendelea kupewa na mwalimu wangu ili zinisaidie siku ya pambano ambalo natarajia litakuwa na ushindani mkubwa, naomba Watanzania wenzangu wazidi kuniombea nifanye vizuri," alisema bondia huyo.

Aidha, Dula Mbabe, aliwataka vijana wasiuogope mchezo huo na kudai ni mchezo wa kawaida kama ilivyo michezo mingine kuliko kukaa mitaani bila kujishughulisha na shuhuli yoyote ambayo itawaingizia kipato huku ikilitangaza taifa.

# Nado: Kilichonileta Azam hiki hapa

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI mpya wa Azam FC ya jijini Dar es Salaam, Iddi Selemani "Nado" kutoka Mbeya City, amesema sababu kubwa iliyomfanya ajiunge na klabu hiyo ni kiu ya kushinda makombe aliyo nayo.

Msimu uliomalizika Azam FC imeshinda Kombe la Mapinduzi, Kombe la Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame na Kombe la FA ambalo limeipa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Nado aliliambia gazeti hili kuwa amekuwa na ndoto ya kushinda mataji mbalimbali, na anashukuru Mungu kupata nafasi ya kujiunga na Azam FC ambayo inaweza kutimiza ndoto zake.

"Unaweza ukacheza vizuri sana, ukaisaidia timu yako kufanya vizuri, lakini kama hujashinda kikombe chochote, roho huumia, naamini hapa ndoto zangu zinaweza kutimia," alisema mshambuliaji huyo.

Aliongeza kuwa anatarajia kuendelea kujituma ili ajihakikishie namba katika kikosi cha kwanza cha timu yake hiyo mpya ambayo ina wachezaji wengi wa kigeni tofauti na ushindani aliokuwa anaupata Mbeya City.

Nado amepewa mkataba wa miaka miwili na atakutana na Kocha Etienne Ndayiragije ambaye naye ametua klabuni hapo akitokea KMC FC baada ya Hans van der Pluijm kutimuliwa kabla ya msimu uliopita haujamalizika. Klabu hiyo ambayo ilimaliza nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika, imeshawapa mikataba mipya baadhi ya nyota wake wa zamani ambao ni pamoja na Mwadini Ally, Yakubu Mohammed, Benjamin Haule na Braison Raphael.

# Michezo

Jumatano Juni 19, 2019

Nipashe




Suarez amtaka Neymar, ampotezea Griezmann HABARI UK 30

MTIFUANO...



Kiungo mshambuliaji wa Japan, Takefusa Kubo (kushoto) katika harakati za kuwania kumiliki mpira dhidi ya kiungo mkabaji wa Chile, Arturo Vidal, kwenye mechi ya michuano ya Copa America iliyopigwa jana nchini Brazil. Chile ambao ni mabingwa watetezi wa michuano hiyo, walishinda kwa mabao 4-0: **PICHA MTANDAO**

# MSOLLA ATOA MKAKATI MABADILIKO YANGA SC

●●● Mwisho wa timua timua ya makocha, Zahera kuanza kunufaika, wapiga dili wa asilimia 10 kwishne, shughuli sasa...

**Na Somoe Ng'itu**

HAITATOKEA! Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, amesema chini ya uongozi wake ndani ya klabu hiyo, suala la "timua timua" ya makocha halitakuwapo kwa sababu uamuzi huo ni moja ya sababu kuu zinazochangia timu kufanya vibaya katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano yote wanayoshiriki.

Msolla, kocha wa zamani wa timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), alikabidhiwa mikoba ya kuiongoza Yanga yeye pamoja na wenzake, katika uchaguzi wa klabu hiyo uliofanyika Mei 5, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Bwalo la Maofisa wa Polisi, Oysterbay jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu jana, Msolla alisema kwa muda mrefu Yanga na timu nyingine za Tanzania zimekuwa zikifanya vibaya katika mashindano ya kimataifa kwa sababu ya kuwa na misingi mibaya hapa nyumbani. Msolla alisema kuwa mchezo wa soka katika ngazi zote unahitaji uwekezaji, na hakuna njia ya mkato, hivyo anawataka viongozi wenzake wabadilike katika utawala wao kama kweli wanataka kufikia maendeleo wanayoyahitaji.

"Timua timua imeturudisha nyuma sana, mimi nina miaka 40 katika mpira wa miguu, naamini ili timu iweze kupata matokeo mazuri ni lazima iwe pamoja kwa kipindi cha kuanzia miaka mitatu, hapa utapata na utaona kitu unachokihitaji, chini ya hapo ni kubahatisha," alisema Msolla.

Kiongozi huyo alisema pia usajili mbovu na viongozi kutowajibika ni sababu nyingine zilizochangia kurudisha nyuma klabu za Tanzania ambapo matokeo yao huonekana pia katika timu ya taifa.

"Usajili mbovu unaoendana na asilimia 10 ni sababu nyingine inayotuumiza, makocha hawapewi mahitaji yao kikamilifu, viongozi hawawajibiki na matokeo yake baada ya timu kufanya vibaya, mzigo anatupiwa kocha, katika uongozi wangu hili halitajitokeza, ninaahidi kulimaliza," Msolla alisema.

Aliongeza kuwa uwekezaji katika soka la vijana ni jambo lisilokwepeka kwa kila klabu, kwa sababu hii itasaidia kuzalisha wachezaji wenye "mapenzi" na klabu wali-yokulia na vile vile utasaidia kupunguza bajeti ya usajili kila msimu unapomalizika.

"Ile Mirambo ambayo ilikuja kusumbua, ni mimi ndiye niliyeiandaa na kutoka nayo kuanzia chini, hata Reli ya Morogoro iliyowatoa kina Ulimboka (Mwakingwe- winga wa zamani wa Simba) niliitengeneza mimi, hakuna kisichowezekana kama watu tukiamua kuweka," aliongeza mwenyekiti huyo.

Alisema pia chini ya uongozi wake atahakikisha kila mtu anafanya majukumu yake na ndio maana wameshatangaza nafasi za kazi kwa ajili ya kupata watumishi mbalimbali watakaofanya kazi za kila siku za klabu na viongozi wa kuchaguliwa wabaki kwenye nafasi zao kwa mujibu wa katiba inavyoeleza.

"Harambee ya Kubwa Kuliko imefanikiwa kwa zaidi ya asilimia 90, na huu ni mchakato endelevu, mambo mengi yalichangia Yanga ikafanya vibaya katika msimu uliomalizika, kama mchezaji halipwi mshahara wake, hawezi kukupa matokeo mazuri, hili tutaliweka sawa na Yanga yenye ushindani itarejea," alisema kocha huyo wa zamani wa Mirambo ya Tabora na Reli ya Morogoro.

Pia Msolla aliwataka wanachama wa timu hiyo kujiandaa kuichangia klabu yao kwa ajili ya kupata fedha za kujiendesha na hatimaye kupata matokeo mazuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki hivi karibuni.

## Stars waahidiwa mamilioni TFF

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI Watanzania wakihimizwa kuichangia timu ya Taifa (Taifa Stars), Shirikisho la Soka nchini (TFF), limesema litatoa kiasi cha Dola za Marekani 5,000 sawa na Sh. milioni 11.4 za Tanzania kwa kila mchezaji wa timu hiyo kutokana na kufanikiwa kukata tiketi ya kufuzu kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 zinazotarajiwa kuanza Ijumaa wiki hii huko Misri.

Jumla ya Dola za Marekani 180,000 sawa na Sh. milioni 412.4 za Tanzania zinatarajiwa kutumika kulipa wachezaji hao pamoja na benchi la ufundi ambao walipambana kuhakikisha timu hiyo inafuzu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema kiasi hicho cha fedha kitatokana na awamu ya pili ya fedha kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF). Kidao alisema kila nchi hupata kiasi cha Dola za Marekani 500,000 sawa na Sh. bilioni 1.14 za Tanzania kutoka CAF na tayari nusu ya fedha hizo walishazipokea kwa ajili ya maandalizi ya kushiriki fainali hizo ambazo zitaanza keshokutwa hadi Julai 19, mwaka huu nchini Misri.

Alisema kuendesha Timu ya Taifa ni gharama sana na kuna wakati inafika shirikisho linatumia fedha nyingine za miradi ya maendeleo ili kuhakikisha mambo yanakwenda sawa.

"Awamu ya pili ya fedha hizo za CAF ambazo ni Dola za Marekani 250,000, zilipaswa zielekezwe katika programu za vijana, lakini sisi tutazitumia kwa timu hiyo hiyo ya Taifa, niwaeleze tu kwa mfano kulipia gharama za tiketi za wachezaji wanaotoka nje zinafika hadi Dola za Marekani 80,000 (Sh. milioni 183.3)," alisema Kidao.

Alieleza pia shirikisho linapokea kiasi cha Sh. milioni 700 kwa mwaka kutoka kwa wadhamini wa timu hiyo ambao ni Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), lakini walitumia karibu Sh. milioni 400 kujiandaa na mchezo mmoja wa ugenini dhidi ya Cape Verde. "Kwa mfano mechi ile (dhidi ya Cape Verde) tuliita wachezaji 11 wanaocheza nje, kwa kifupi maandalizi ya mechi mbili, tunakula hela ya mwaka," Kidao, Mwenyekiti wa zamani wa Chama cha Makocha Tanzania (TAFCA) alisema.

Aliongeza kuwa baada ya timu hiyo kurejea nchini, TFF itaanza tena maandalizi mengine mwezi ujao kwa ajili ya mechi mbili (nyumbani na ugenini) dhidi ya Sudan ili kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042